

KUTHIBITISHA NENO LAKE



Hebu tuendeleo kusimama na kuinamisha vichwa vyetu. Bwana Yesu, tuna shukrani kwako asubuhi hii kwa ajili ya majaliwa ya kuingia katika Uwepo Wako katika nyumba Yako, ambamo watu Wako wamekusanyika katika Jina Lako. Na wote ni Wako, Bwana. Tunajikabidhi sasa Kwako kwa ajili ya tumaini lililomo mioyoni mwetu kwa ajili ya i—ibada kwa wale wasio na Mungu na wasio na Kristo, wapate kuokolewa, na walio wagonjwa wapate kupona, na watakatifu watabarikiwa. Tujalie, Bwana. Kisha hatimaye, tutaviinamisha vichwa vyetu katika unyenyekevu na kukupa sifa kwa ajili ya yote utakayotenda kupitia kwetu leo. Kwa kuwa ni katika Jina Lake Yesu tunaomba. Amina. (mnaweza kuketi)

² Nina shukuru sana kwa majaliwa ya kuwa hapa tena leo, na kwenu ninyi wote ambao mmesafiri toka mbali sana kuja kwa ajili ya Ujumbe huu kwa ajili ya ibada asubuhi ya leo. Najua hamkuja kuniona tu na kunisikiza mimi, mlikuwa kukutana na Bwana Yesu. Na kwa hivyo ninatumaini ya kwamba Yeye atawapa hamu ya mioyo yenu.

³ Sasa nime—nimerudi, nimekuja tena, nilipeleka jamaa yangu huko Tucson kisha nikarudi. Nimechoka na kudhoofika. Nami nimekuwa nikisafiri majira yote ya kiangazi, tangu Januari iliyopita, na sasa nimekuja kusudi nishuke kwenda Kentucky juma hili, kwenda kuwinda pamoja na marafiki wachache, kujaribu kujiburudisha kidogo. Lanipa wasiwasi sana, mwajua, kwa hivyo nina. . . Mimi pamoja na Billy tuko karibu kwisha, kwa hivyo tu—tunaomba ya kwamba Mungu atatusaidia kupumzika juma hili.

⁴ Bwana akipenda, nataka kurudi humu tena Jumapili ijayo Bwana akipenda. Nami nataka ibada maalum Jumapili ijayo. Nataka kufanya jambo lisilo la kawaida. Sasa, nasema hili kusudi watu ambao. . . ambao hawana hamu si lazima waje, lakini sisi kila mara huwaomba wagonjwa, Bwana akipenda, watu wajapo. Jumapili ijayo nataka kuona nini kilicho mioyoni mwenu wote. Na—nawatakeni muandike, leo, mtakapoondoka, na muyaweke kwenye dawati, naye Ndugu Neville atayakabidhi kwa Billy Paul, naye atanipa mimi, kile kilicho moyoni mwako. Sema tu. . . iwapo ni swali la Biblia, kwa kawaida mimi hufanya hivyo. Nitaifafanua kidogo sasa, labda una shida fulani moyoni mwako ambayo—ambayo wewe—huwezi kuitatua kwa vyo vyote, kama tuseme una, ee, labda shida ya kinyumbani. Si lazima uandike jina lako humo, lakini tu, “Mume wangu hufanya hivi na vile na kunizuia.” “Mke wangu hufanya hivi na vile.” “Na—na kuna—kuna jambo fulani linalotendeka maishani,” ama—ama cho chote kile, mwajua, lile tu lililo moyoni mwako,

jambo linalokutatiza. Nadhani hilo lingekuwa zuri. Nanyi je? Basi chunguza tu mle, na labda utauliza swali nami huenda nikamjibia mtu mwingine. Unaona, huenda wakawa na shida ile ile. Na kile tu kilicho moyoni mwako, lifanye fupi tu iwezekanavyo, kama vile, “Nina mtoto ambaye yaonekana kama kwamba anaharibika, nifanyeje?” “Nina mume ambaye haji kanisani pamoja nami. Yeye ana kiburi kwangu, nifanyeje?” ama mke vile vile. Au—au, wajua, “Biblia inasema hivi mahali pamoja na hivi mahali pengine, sielewi na hilo. Haya, ningetaka kujua maana yake.” “Basi nifanyeje, nikiwa Mkristo, ninapofanya kazi afisini na bosi wangu aseme hivi na vile, na ananiambia niende naye kwenye karamu, na kwenye karamu hii wao hunywa pombe, nifanyeje?” Unaona, basi, mwajua, mambo kama hayo yaliyo katika mawazo ya mwanadamu. Tunawatakeni mfanye hivyo.

⁵ Na, kwa hivyo, ndipo si—sina budi kurudi kule basi, baada ya hayo, huko Arizona. Nami nilidhani ni—ningepata nafasi ya kuwasaidia kufahamu, na vizuri niwezavyo. Ningetaka kupata mengi niwezayo kuweka mimbarani kabla hamjaondoka. Andikeni tu na kuyaweka hapa, na—na Ndugu Neville ama mmoja wao atanipatia. Na juma hili, kule mlimani, nitapata na—nafasi kuyasoma na—na kuyaombea, na kuwatafutia majibu ya Kimaandiko kwa cho chote kile niwezacho kuwasaidieni. Kwa kuwa hiyo ndiyo sababu tumekusanyika hapa, ni kusaidiana. Mnaona? Mnanisaidia kwa kuniombea, nami natumaini ninaweza kuwasaidieni. Basi, msisahau ya kwamba hiyo itakuwa Jumapili ijayo asubuhi.

⁶ Na sasa, leo, sisi. . . tuna wageni, kama kawaida. Na ni wangapi wametoka umbali wa maili mia moja, inueni mikono yenu? Hao ni asili mia tisini na tisa ya kusanyiko. Jumapili chache zilizopita, nilisema, “Wangapi wanatoka *umbali fulani*,” ama cho chote kile, nami sikuona mikono toka Jeffersonville. A! Siku iliyofuata nikaipata, hata hivyo wao walisema, “Ndugu Branhan, Wageni wote huingia,” kasema, “tunawaachia nafasi zetu kanisani.” Kwa hivyo walisema wao huja, mia kadha huja na hawawezi kuingia, kasema, “Kwa sababu tuliwaona wageni, unaona.” Naam, hilo ni jema kwa watu wa Jeffersonville hapa. Sisi—tuna—tunashukuru, Jeffersonville na New Albany, na majirani. Tunashukuru kwa hilo. Wangapi wanatoka zaidi ya umbali wa maili elfu? Jamani! Wangapi wanatoka zaidi ya umbali wa maili elfu, inueni mikono yenu? Lo, salala! Hilo ni jema. Hilo ni. . .

⁷ Jumapili iliyopita, ilikuwa juma moja lililopita, nilinena juu ya somo, “Makao ya Baadaye ya Bibi-Arushi na Bwana Arushi,” nami nadhani tulitoka umbali wa maili elfu moja na mia tano mraba. Na ikawa, hicho ndicho kilikuwa kipimo hasa cha Mji ule niliokuwa nikinena habari zake, maili elfu moja na mia tano mraba. Nimekuwa nikijilisha hilo tangu wakati huo, nikijua ya

kwamba maisha haya yatakapokwisha, ninaelekea kwenye huo Mji. Naenda zangu kwenye Mji huo, na sijali mambo mengine. Je kama jua halitaangaza leo, ama kesho haiji, inaleta tofauti gani? Tuna Makao, Mahali pa kupumzikia. Tuchoke tusichoke, tungali tuna Mahali hapo pa kupumzikia. Mnasema, “Hiyo ni ndoto ya mzee.” La, sivyo, Sivyo. Ni Ukweli wa Biblia.

⁸ Usiku mmoja baada ya kuzungumza hapa na palikuwa, mtu mmoja aliyekuja mbio hapa nyuma ya jukwaa, nilipokuwa natoka mlangoni na wakijaribu kunichukua kwenye gari. Basi huyu kijana mwanamume akasema, “Nataka kukwambia tu neno moja.” Billy na ndugu wengine wakijarib kunipeleka kwenye gari. Akasema, “Naweza kusema hilo neno moja?”

Nikasema, “Endelea kusema, bwana.”

⁹ Naye akasema, “Ulikuwa ukiongea usiku wa leo, juu ya kuwakemea hao wanawake kwa ukali, jinsi walivyokuwa wanavalia, wakivalia hizo nguo.” Kasema, “Mtu wa umri wako angaliwazia hayo, bali ungalikuwa na umri wangu ungaliwaza tofauti.”

Nikasema, “Una umri gani?”

Akasema, “Nina umri wa miaka ishirini na saba.”

¹⁰ Na kikasema, “Nilipokuwa mdogo kuliko wewe kwa miaka kumi, kumi na mitano, nilikuwa nikihubiri jambo lile lile. Waona?” Nilisema, “Ni kile kilicho moyoni mwako, kijana. Macho yako yanaona kupitia moyoni mwako.” Naye akakiinamisha kichwa chake akaondoka. Nadhani hamna jibu jingine zaidi kwa hilo. Waona, inategemea ni nini kilicho ndani *humu* ndicho kitakachotokea *hapa* na *hapa*. Waona, Yesu alisema, “Ukisema kinyume cha yale yaliyomo *humu*, basi unakuwa mnafiki.”

¹¹ Nina furaha asubuhi ya leo, mahali fulani katika kusanyiko hili kuwa na ra—rafiki mpendwa sana, ndugu, Kasisi Eddie Byskal na mkewe na watoto wake. Nadhani wao waliingia mkutanoni asubuhi ya leo. Eddie, uko hapa? Ni—nilidhani. . . Vema, huenda ikawa hakuweza kuja. Ndugu, lo, naam, pale. . . Sasa, hiyo siyo kona ya “amina,” Eddie. Umekaribishwa humu jukwaani pamoja nasi, wahudumu, ukitaka kuja. Ndiposa tumekuwa juu ya. . .

¹² Ndugu Eddie alikuweko wakati Bwana aliponipa lile ono kuhusu yule dubu na kulungu. Ile. . . Wangapi wanakumbuka hayo nilipowaambia? Vema, yeye alikuweko. Ndiye yule kijana aliyekuwa na shati lenye mirabamiraba Ndugu Eddie Byskal. Naye akasimama pale ambapo. . . na nikauliza. . . Ni—niliwauliza iwapo walikuwa na shati lenye mirabamiraba ye yote wao. “La,” hamna aliyekuwa nalo. Nikasema, “Vema, huenda ikawa. . . haina budi kuwa shati lenye mirabamiraba. Kutakuweko na dubu mkubwa wa rangi ya fedha, na—na mnyama fulani mwenye pembe zenye urefu wa inchi arobaini na

mbili, *hivi*, aliyefanana na paa.” Na hiyo ilikuwa yapata miezi sita, nilisema hapa, mwajua, kabla haijatendeka; wakati kama huu, lo, mapema kuliko hivi mwakani.

¹³ Ndipo nilialikwa kule juu kwa mtu huyu, kwenda kuwinda. Sijapata kurudi tena nchini humo, kule tulikoenda, nami nikasema hivyo. Bali huo mkondo mdogo, huko ni kule juu kabisa kwenye barabara ya Alaska, ambako hamna kitu ila misitu na milima na wanyama. Na usiku huo kwenye gari la kukokotwa na lingine nilipokuwa nikiwambia Ndugu Byskal nyuma kule na—na Ndugu Southwick, akasema, “Vema, mimi—mimi. . . Tunakwenda katika nchi Ya kondoo,” kasema, “haitakuweco kule juu.”

¹⁴ Nami nikasema, “Naam,” nikasema, “ilikuwa kwamba mmoja wa vijana waliokuwa pamoja nami alikuwa amevalia shati lenye mirabamiraba.” Hamna ye yote aliyekuwa na shati lenye mirabamiraba, Ndugu Byskal hakuwa nalo, wala wengine wetu hawakuwa nalo.

¹⁵ Usiku wa pili, tulikuwa tumemwona, kondoo dume mwenye madoadoa kule juu sana ambako hamna miti. Naam, huko ni juu sana ambako miti hata haikui, ambako hamna kitu ila kulungu na kondoo, nasi tulikuwa—tumewaona wengine kule juu sana. Basi tulipokuwa tukitelemka adhuhuri hiyo, Ndugu Byskal alijikwaa akatumbukia majini na kulowa maji.

¹⁶ Asubuhi iliyofuata tuliamka mapema tukaanza kuwawinda kondoo dume ambao tulidhania tungewapata. Na juu yake. . . Tulifika juu pale nasi tulikuwa. . . tayari tumekula chakula chetu cha jioni, nasi hatungaliwapata wale kondoo dume, naye Ndugu Byskal ndiyo kwanza amemuua kulungu. Basi mimi, nikitazama hapa na pale, nasi tukapanda juu, Ndugu Southwick akaniambia mimi, akasema, “Naamini tuta. . . mkitaka kutembea vizuri, Ndugu Branham, tutapanda mlima huu, kisha tutelemke kwenye lile bonde, hao kondoo dume huenda wamekwenda kule,” ambao ni mwendo mrefu wa miguu. Bali hakuwi giza hadi labda usiku sana, labda saa nne au saa tano za usiku wakati mwingine.

¹⁷ Na ni mwendo wa miguu mrefu sana katika hiyo milima ya miamba. Kwa hivyo mimi napenda kutembea, na kwa hivyo tulisimama tu pale huku tumekumbatiana, ndevu zetu wote zikipata mvi, tumekumbatiana, tukilia na kujua, nikasema, “Ndugu Bud, natumaini siku moja, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, naweza kutembea kwenye milima ile yote pale.”

¹⁸ Yeye akasema, “Natumaini nitakuwa pamoja nawe, Ndugu Branham.” Nasi tulikuwa tumesimama pale, tukifurahi katika Bwana. Nami naipenda ile milima sana!

¹⁹ Kisha tukashuka. Hapo ndipo Ndugu Byskal alipomuua yu—yu—yule kulungu. Kwani, yeye ni mumishenari kwa Wahindi, naye alitaka kuwalisha huyu Wahidi wake. Kwa hivyo

tukatelemka, tukala chakula chetu, tukamchuna yule kulungu kisha tukarudi.

²⁰ Mimi na Bud tulikuwa tunapitia kule milimani, nasi tulipotazama, kwa mbali, tukitumia darubini yangu, nilimwona mnyama huyu niliyekuwa nimemwona, akipitishwa taratibu machoni, kama nilivyowaambia ninyi hapa. Ndugu Byskal pale, akisimama karibu sana nami. Kwa hivyo nikasema, “Mnyama ndiye yule.”

²¹ Naye akaweka darubini machoni, akasema, “Ni kulungu dume, mnene, mkubwa mno.”

²² Nami nikasema, “Sijapata kumwona, nilidhani walikuwa na pembe kama kibao.” Bali huyu alikuwa na pembe zilizochongoka, alionekana mnyama wa kigeni sana, kama tu vile nilivyoona katika lile ono. Sikuwa nimepata kumwua kulungu hapo kabla kwa bunduki.

²³ “Kwa hivyo, vema,” yeye akasema, “iwapo Bwana alikupa wewe huyo,” akasema, “basi. . .”

²⁴ Nikasema, “Ndiyo sharti awe ndiye huyo. Jambo pekee linalonishangaza ni hilo shati lenye mirabamiraba.” Nami nikatazama hapa na pale, naye Ndugu Eddie, hapana shaka mkewe aliliweka, alikuwa kule pamoja naye, lazima aliliweka katika mfuko wake wa kubebea nguo. Alipolowa maji siku iliyotangulia, alikuwa amebadilisha mashati, na kulikuweco na shati lenye mirabamiraba. Nikasema, “Ndilo hilo.”

²⁵ Nilipokwenda pale nikampata huyo kulungu, yeye, Bud, akaniambia, kasema, “Sasa, Ndugu Branham, unasema pembe hizi ni inchi arobaini na mbili?”

Nikasema, “Hivyo ndivyo zitakavyokuwa.”

Yeye akasema, “Zinaonekana kama tisini na mbili kwangu.”

Nikasema, “La. Hizo ni inchi arobaini na mbili.”

²⁶ Akasema, “Sasa, kulingana na yale uliyoniambia, kabla hatujamfikia yule kijana kule chini mwenye shati lenye mirabamiraba, Eddie,” (ambapo wangekutana nasi kule chini ya mlima, maili kadha), kasema, “utamua dubu mwenye rangi ya fedha.”

Nikasema, “Hayo ni BWANA ASEMA HIVI.”

²⁷ Akauliza, “Ndugu Branham, atatoka wapi? Naweza kuona maili hamsini mzunguko.”

²⁸ Nikasema, “Yeye yu angali Yehova-Yire. Mungu anaweza kujipatia, unaona. Yeye aweza kuwafanya kindi wawepo. Iwapo anaweza kumfanya kondoo mume awepo, ikiwa amenena hayo kuhusu dubu, dubu anaweza kuwepo.”

²⁹ Huku tukijaribu kumbeba huyu kulungu mzito, lile kumbukumbu, tukitelemka mlimani, nami nilibeba bunduki sehemu ya muda, kisha yeye angeibeba hiyo bunduki, na

kadhhalika. Basi tulipofika karibu na mto mkubwa wa barafu, naam, tukafika chini kule. Ilikuwa joto kidogo, tukafika kwenye ule mto wa barafu, tukaketi pale muda mchache tupate baridi. Yeye akasema, “Wajua, Ndugu Branham, hatuko zaidi ya maili moja toka ambapo Eddie na Blaine, hao vijana wawili, watakuwa wamesimama. Heri maskini huyo dubu aanze kujitokeza.”

Nikasema, “Bud, naamini unatilia shaka.”

³⁰ Yeye akasema, “Ndugu Branham, ndugu yangu alikuwa na kifafa kwa miaka mingi sana. Nawe ukaniambia wakati mmoja, mara ya kwanza humu, tulipoenda mahali pengine, ukaniambia jinsi huyo kijana alivyoonekana.” Naye Eddie alikuwa amepanda farasi karibu sana nami, amepanda farasi, wakati Bwana alipotoa hilo ono. Nami nikawaambia watakachomfanyia huyo mvulana, kifafa kikaisha. Basi akasema, “Siwezi kulitilia shaka.”

³¹ Nikasema, “Bud, sijui atakakotoka huyo dubu.” Lakini nilikuwa na umri wa yapata miaka hamsini, nina hamsini na mitano sasa, kwa hivyo hiyo imekuwa yapata miaka mitatu iliyopita. Nilikuwa na kama hamsini na miwili au hamsini na mitatu. Nikasema, “Sijalionia likikosea. Mungu atanipa huyo dubu wa rangi ya fedha kabla sijawafikia hao vijana.” Nasi tulikuwa karibu sana kufikia pale chini ambapo misonobari midogo na miti ya mbao ilipoanzia.

³² Chini kidogo ya kile kilima, tulikuwa karibu kuingia mwituni, akaketi chini. Yeye ndiye aliyekuwa amembeba yule mnyama wakati huo, nami nilikuwa na bunduki. Basi akasema, “Maskini dubu huyo heri aanze kujitokeza, sivyo?”

Nikasema, “Yeye atakuwepo. Usijali.”

Akasema, “Naweza kuona kila kilima.”

³³ Nikasema, “Mimi . . . Bali mimi ninaiona ile ahadi!” Waona? Waona, Yeye aliahidi. Nikasema, “Yeye . . .” Nikasema, “Bud, ni nini kile kinaketi pale?”

³⁴ Akaangalia, kasema, “Ni dubu mkubwa mwenye rangi ya fedha.” Kasema, “Ndiye huyo.” Tulipompata huyo mwenye rangi ya fedha na kurudi . . . nilikumbuka katika lile ono nililowaambia, niliigopa ile bunduki. Ilikuwa ndogo yenye ukubwa wa .270, risasi ndogo, mwaona. Imenaswa kwenye kanda. Nami nikampata yule dubu, yapata karibu yadi mia tano, kama ilivyosemwa. Bud akasema, “Afadhali umpige risasi yule dubu mgongoni.” Akasema, “Je, umepata kumuua dubu wa rangi ya fedha hapo kabla?”

Nikasema, “La.”

³⁵ Yeye akasema, “Lo, hawajui mauti ni nini!” Nilipata kujua hayo baadaye. Kwa hivyo akasema, “Hawaangamizwi kwa kugutuliwa,” kasema, “yakupasa umpige risasi.”

Nikasema, “Kulingana na lile ono, nilimpiga risasi moyoni.”

³⁶ Akasema, “Vema, kama hilo ono lilisema hivyo, nitakuunga mkono.”

³⁷ Nami nikasema, “Haya twende.” Nasi tukakaribia, nami nilipoinuka, huyo dubu akaniona. Hilo ndilo alilotaka, kushambulia. Nami ni—nikampiga huyo dubu risasi, hata haikuonekana kama kwamba aliiumizwa. Huyu yuaja! Na kabla sijatia risasi nyingine kwenye ile buduki, yule dubu akafa yapata yadi hamsini kutoka kwake.

³⁸ Bud alikuwa mweupe mdomoni, akasema, “Ndugu Branham, sikumtaka pajani mwangu.”

Nikasema, “Hata nami pia.”

³⁹ Kasema, “Nina furaha kwamba hilo ono lilisema ulimpata.” Akasema, “Basi, ikiwa hizo, kama hizo pembe ni inchi arobaini na mbili, nitashikwa na . . .” Nitasema jinsi alivyosema, kasema, “Nitashikwa na ugonjwa wa kupiga ukelele.”

⁴⁰ Nikasema, “Vema, shikwa nao sasa hivi, kwa sababu hivyo ndivyo zitakavyokuwa.”

⁴¹ Tulipomfikia Ndugu Eddie, nilimwambia Ndugu Eddie . . . Tuliwafunga farasi mbali, wao wanaogopa dubu. Kisha, lo, jamani, walikuwa wamepata harufu yake. Hatukuweza kumchuna, ilikuwa usiku sana; ilitupasa kurudi siku iliyofuata. Kisha tulikata ile kamba karibu mara kumi, na farasi wakikimbia kila mahali. Kwa hivyo basi tulipofika kule chini, yeye akasema . . . Akaenda akachukua utepe wa kupimia toka kwenye mfuko wake wa kufungiwa tandikoni, kasema, “Blaine.”

⁴² Nikamwambia Ndugu Eddie, nikasema, “Tazama huo mkono mdogo sasa, kulingana . . .” Nilidhani huenda ikawa ni Billy Paul, mikono midogo iliyoshika ule utepe wa kupimia kuzunguka ile pembe. Nikasema, “Tazama ule mkono mdogo,” nikampiga ngumi Ndugu Eddie. Tukarudi nyuma. Akaiweka sawa sawa kama *hivyo*, ilikuwa sawa sawa kabisa, inchi arobaini na mbili. Angalia, sawa kabisa hivyo hasa. Yesu hashindwi kamwe! Neno hilo halitakosa kutimia mradi tu linatoka kwa Mungu.

⁴³ Niliwaona kati yetu, Ndugu na Dada Jackson kutoka Afrika Kusini. Nafikiri wamekwisha kujulishwa kwenu. Je, m—mmejulishwa, Ndugu Jackson? Asubuhi ya leo, simama, wewe na Dada Jackson. Nataka waone. Ndugu yangu, Eddie, ndiye huyu hapa mwindaji mwenzangu wa zamani kutoka Afrika Kusini, pia, chini huko. Bwana awabariki, Ndugu Jackson na Dada Jackson, tuna furaha kuwa pamoja nanyi hapa. Hebu wahudumu wote waliomo humu jengoni inueni mikono yenu, wote walio katika huduma. Vema, hilo ni nzuri na ni sawa kabisa, vema. Bwana awabariki. Tuna furaha kuwa pamoja nanyi nyote hapa. Nitafanyiza mstari wa maombi katika dakika

chake, ili ni—nisi. . . Laiti ninyi nyote mngalisimama mje humu mkahubiri badala yangu. Tuna furaha sana kuwa pamoja nanyi, kila mmoja wenu.

⁴⁴ Ninapowazia juu ya uaminifu wenu, na—nanyi mkitoka kila mahali nchini, na kadhalika, kunisikia nikinena habari za mpindwa Bwana Yesu, tumaini lenu mlilo nalo kwamba Yeye huyasikia maombi yangu. Nilikuwa nikiongea muda mfupi uliopita kwenye mahojiano ya kibinafsi na mshiriki fulani wa kanisa hili, hazijapita dakika arobaini na tano, mama aliyevunjika moyo. Mara nilipoanza kumwambia huyo mwanamke jambo fulani, (sijui kama yeye angetaka niseme yeye ni nani au hangetaka), kukaja Nuru ile ile mnayoiona katika ile picha. Ilikwisha, akaenda zake kwa furaha. Tunafuraha tele, leo, katika wakati huu wa kigeugeu tunaishi, ambapo ni vigumu kuweka matumaini yako katika kitu cho chote, tuna Ufalme ambao hauwezi kugeuka, hauwezi kutikisika. Usiotikisika! Si ule mwamba wa Gibraltar, bali imani yetu inaweza kutulia kabisa juu ya Mwamba wenye Imara, juu ya Yesu Kristo, Mwamba usiotikisika wa wokovu.

⁴⁵ Nataka kumshukuru yule dada aliyemletea mke wangu aliye hapa kile kijisanduku chenye pembe tatu, kikiwa na Biblia ndani. Alikuwa amefanya agano na Bwana juu ya kijisanduku hiki. Yeye alikithamini sana. Kina baadhi ya . . . kama picha za nyakati za kale mle ndani. Naye alimsihi Bwana . . . Yeye alikuwa amekithamini hicho kijisanduku kupita kiasi, labda. Kijisanduku cha kawaida tu katika mfano wa piramidi. Naye akakileta kwa mke wangu pamoja na Biblia. Asante, dada. Kila moja ya zawadi zenu dogo na kadhalika mnavyompa Billy Paul na wengineo hunifikia. Nashukuru kwa kila kitu. Mungu awe pamoja nanyi.

⁴⁶ Msisahau sasa, Jumapili ijayo asubuhi. Mara tu ibada itakapokwisha leo, andika swali lako. Ikiwa hauwezi, lilete jumapili ijayo asubuhi. Nitakuja mapema kidogo, ndipo basi watayaleta chumbani, kusudi nipate nafasi ya kuyapa msingi wa Kimaandiko. Nasi tutayajibu maswali hayo Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda.

⁴⁷ Sasa, kuna leso nyingi zilizo hapa. Nami nimezisukuma nyuma, kusudi tu nipate kuweka maandishi ya—yangu hapa chini, na . . . pia Biblia yangu, ili, Biblia yangu na maandishi yangu, hasa, kusudi nipate nafasi kidogo. Bali mimi . . . nitamwomba kila mmoja.

⁴⁸ Nitaandika maandiko yangu, nina wakati mfupi tu. Sitawakawisha kama nilivyofanya wakati uliopita nilipokuwa hapa, karibu masaa manne. Nilijitolea ahadi, nikinasa sauti tena hivyo, ningezinasia hapa peke yangu, ama cho chote kile, kusudi nisiwakawishe sana.

⁴⁹ Je, Dk. Lee Vayle yuko asubuhi ya leo? Nilitaka kuuliza kama Dk. Lee Vayle. . . Uko hapa, Ndugu Vayle? Inua mkono wako ikiwa uko. Je, yuko huko nyuma? Vema, asante, Ndugu Roy. Nami nataka uhakikishe umechunguza maandishi hayo, Ndugu Vayle. Uko mahali fulani makutanoni nyuma kule ambako siwezi kuona, au sebuleni. Yatupasa tujihadhari, hatuwezi kuwaruhusu watu wengi sana wasimame, na mkuu wa wazimamoto hataturuhusu kufanya hivyo, mwaona, na ndivyo tulivyo. Nakutaka uchunguze ufunuo wangu juu ya Uzao wa Nyoka, uwekwe kwanza katika, Wakati wa Kanisa la Efeso ambao yeye anaandika, kunifuatishia sarufi. Kimeandikwa vizuri sana! Nami nakutaka uchunguze haya na acha mtu ye yote aseme neno juu ya ule Uzao wa Nyoka sasa (kama ulikuwa sahihi ama sivyo)! Kwa hivyo Bwana alinipa huo jana, waona. Lo, inapita yote! Jinsi ninavyopata jumbe nitakuwa nikitembea na kitu fulani kitanigusa. Kisha. . . Na kama ninajua ni Mungu, nitayachukua na kuyachunguza katika Maandiko. Ndipo nina. . . Haijakosea bado, bali, tangu Mwanzo hata Ufunuo, huwa ni kweli, haidhuru watu wanawazia nini juu yake. Na imekuwa zaidi ya hapo awali tangu zile Muhuri Saba. Mnaona, ilifanya hivyo wakati huo. Kwa hivyo Bwana awabariki sasa tunapojifunza. Basi kwa heshima ya Neno. . .

⁵⁰ Nami naamini mtu fulani, fundi wa mitambo, ama ye yote yule anayehusika, inaanza kurudisha sauti hapa kwenye vipaza sauti. Sasa mnaweza kusikia huko nyuma, vizuri? Inueni mikono yenu kama mnaweza. Sawa!

⁵¹ Sasa hebu tufungue katika Biblia, mahali pawili katika Maandiko, nami nitajaribu kuuhubiri ujumbe huu kisha tufumukane kwa wakati, Bwana akipenda. Na sasa hebu tufungue Marko, sura ya 5, na I Wafalme, sura ya 10; Marko sura ya 5, I Wafalme, sura ya 10.

⁵² Sasa, bali kwa mgeni ambaye huenda akawa ndani milango yetu, hili, tunaweka shule yetu ya Jumapili katika darasa moja kubwa. Na hilo ni darasa hili hapa, kwa sababu vyumba vyote vimejaa watu nasi hatuwezi kuwa na madarasa mbalimbali ya kawaida, nasi tunajifunza juu ya Neno kwa muda mchache, kuwa na ushirika wa pamoja. Sisi si. . . Sisi si dhehebu lo lote. Hatuna dhehebu. Sisi ni huru katika Bwana, nasi si kundi la washupavu wa dini. Tunafundisha Biblia tu, Hiyi pekee. Na Bwana ni mwema sana kwetu, hata Yeye huiunga mkono na kuonyesha kwamba ni kweli. Nayo inatupa faraja kuu.

⁵³ Na sasa mme—mmekaribishwa kuwa kati yetu wakati wo wote. Sasa, mimi siko humu wakati wote, bali tuna wachungaji bora hapa; Ndugu Neville, mmoja wa wachungaji wetu; Ndugu Capps, mwingine wa wachungaji wetu; na Ndugu—na Ndugu Collins, Wilbur Collins, mwingine, wachungaji wetu. Kisha tuna wengine mbalimbali kutoka mahali mbalimbali, makanisa yetu madogo tunaoshirikiana. Kama uko karibu na—na Texas, wana

wa Martin hapa, na Ndugu. . . Ndugu anayekuja pamoja nanyi huku anaitwaje? Siwezi kumwona Ndugu Blair asubuhi ya leo. Lo, Ndugu Blair, sikukuona, Ndugu Blair. Ndugu Ruddle, humu nyuma kabisa, moja ya makanisa kwenye 62, moja ya makanisa tunaoshirikiana hapa. Ndugu Junior Jackson, anayeketi papa hapa karibu na Ndugu Blair, ninamwona sasa, lingine la makanisa yetu tunaoshirikiana. Nasi tuna makanisa kote nchini toka kila mahali.

⁵⁴ Ndugu Jack Palmer, alipokuwa akija, nafikiri walikuwa wakienda mbio kidogo, katika lile gari mpya la mwanawe, ikawa, mwajua, walikuwa wakipitisha spidi inayoruhusiwa, wakapata ajali. Aliumiza shavu lake, naye hakuweza kuja, akarudi nyumbani. Kwa hivyo yeye anapata nafuu. Naye Ndugu Ben hapa, mmoja wa ndugu zetu hapa Kentucky, alimpigia simu asubuhi ya leo kuona kama wao walihitaji fedha ama cho chote ambacho kanisa lingeliwasaidia nacho, yeye akasema kila kitu ni sawa. Naye alikuwa akipiga kona kasi sana, akagonga kokoto, nayo ikamvunja shavu au kitu fulani. Nao walinipigia simu kutoka kule chini, alipoliendesha gari lake likagonga kikingi ama cho chote kile, ki—kisha akapiga simu aombewe.

⁵⁵ Ndugu Billy Collins pia, twajua, alipondaponda kidole chake vibaya sana, akavunja mfupa wake, nasikia, nao iliwabidi kukiganga. Kwa hivyo tunataka kumkumbuka kwa maombi.

⁵⁶ Na sasa sababu tunasimama. Tunapoonyesha uaminifu wetu, bendera inapopitishwa karibu nasi, ama cho chote kile, sisi kila mara husimama wima, au kupiga saluti, au kusimama, angaa, kutoa heshima kwa taifa letu, ambayo yatupasa kufanya, na kwa bendera yetu. Basi na Bwana wetu je, tunaposoma Neno Lake? Hebu tusimama sasa tunaposoma Marko Mt. 5, kuanzia kifungucha 21. Tazameni kwa makini sasa tunaposoma:

Yesu alipokwisha kuvika kurudia ng'ambo katika kile chombo, wakamkusanyikia mkutano mkuu; naye alikuwa kando ya . . . bahari.

Akaja mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo; hata alipomwona akaanguka miguuni pake,

Akamsihi sama, akisema, Binti yangu mdogo yu katika kufa; nakuomba uje, uweke mkono—mikono yako juu yake, apate kupoma, na . . . kuishi.

. . . Yesu akaenda pamoja naye, mkutano mkuu wakamfuata, wakimsongasonga.

Na mwanamke mmoja mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili,

. . . na kuteswa mengi kwa mikono ya matabibu wengi, amegharimiwa vitu vyote alivyokuwa navyo, kusimfae hata kidogo, bali hali yake ilizidi kuwa baya;

Aliposikia habari za Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi lake;

Maana alisema, Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona.

Mara chemchemi ya damu yake ikakauka, naye akafahamu mwilini mwake kwamba amepona msiba ule.

Mara Yesu, hali akifahamu nafsini mwake kwamba nguvu zimemtoka, akageuka kati ya . . . ya mkutano, akasema, Ni nani aliyenigusa mavazi yangu?

Wanafunzi wake wakamwambia, Je! wawaona wanavyokusonga-songa, nawe wasema . . . Nani aliyenigusa?

Akatazama pande zote ili amwone yule aliyelitenda neno hilo.

Na yule mwanamke akaingiwa na hofu na kutetemeka, akijua lililompata, akafa akamwangukia, akamweleza kweli yote.

Akamwambia, Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena.

Hata alipokuwa katika kunena, wakaja watu kutoka kwa yule mkuu wa sinagogi, wakisema, Binti yako amekwisha kufa; kwani kuzidi kumsumbua mwalimu?

Lakini Yesu, aliposikia lile neno likinenwa, akamwambia mkuu wa sinagogi, Usiogope, amini tu.

Wala hakumruhusu mtu afuatane naye, ila Petro, . . . Yakobo, . . . Yohana nduguye Yakobo.

Wakafika nyumbani kwa yule mkuu wa sinagogi, akaona ghasia, na wakati . . . na wakilia, wakifanya maombolezi makuu.

Alipokwisha kuingia, akawaambia, mbona mnafanya ghasia na kulia? Kijana hakufa, bali amelala tu.

Wakamcheka sana. Naye alipokwisha kuwatoa nje wote, akamtwaa babaye yule na mamaye, wa yule kijana (hasa), na kisha wale walio pamoja naye, akaingia ndani alimokuwamo yule kijana.

Naye akamwambia yule kijana, Naye . . . (samahani) . . . akamshika mkono kijana, akamwambia, Talitha, kumi; tafsiri yake, msichana, nakumbia, inuka.

Mara akasimama yule kijana, akaenda; maana alikuwa amepata . . . umri wa miaka kumi ma miwili. Mara wakashangaa mshangao mkuu.

Akawaonya sana, akasema, mtu asijue habari ile; akaamuru apewe chakula.

57 Katika Kitabu cha I Wafalme, sura ya 10, tunasoma vifungu hivi vitatu:

Na malkia wa Sheba aliposikia habari za Sulemani juu ya jina la BWANA, alikuja ili amjaribu kwa maswali ya fumbo.

Akaingia Yerusalemu na wafuasi wengi sana, na ngamia wachukua manukato, . . . dhahabu nyingi sana, na vito vya thamani; alipomfikilia Sulemani, a . . . akazungumza naye mambo yote aliyokuwa nayo moyoni.

Naye Sulemani aka—akamfumbulia maswali yake yote; wala hakukuwa na neno alilofichiwa mfalme asimwambie.

58 Na tuombe. Bwana Yesu, tunaposoma hadidhi hizi za Biblia, mioyo yetu inaruka kwa furaha. Kwa kuwa tunajua kuwa Wewe u Mungu, nawe hubadiliki. Hubadili mtindo Wako, hubadili kamwe njia Zako, unadumu Mungu milele. Nasi twaomba, Mungu, ya kwamba utatuletea fasiri asubuhi ya leo, ya Maandiko haya ambayo ungetutaka tuyajue, kusudi mioyo yetu ipambanuliwe, Roho Mtakatifu aliye mkuu angekuja kati yetu leo na kupambanua nia zetu na mioyo yetu. Na kusiwepo lo lote lililosalia, ambalo mioyo yetu haita- . . . tuwe na furaha tele tuondokapo hapa hata tuseme kama wale waliotoka Emau usiku ule, “Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani!” Wewe wadumu Mungu daima, nasi ni watoto wako wenye njaa waliokusanyika asubuhi hii. Maana imeandikwa, “Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.” Tubariki katika kukusanyika kwetu pamoja na watu hawa wote, Bwana, ambao wamekuja toka mamia, naam, maelfu ya maili. Twaomba, ya kwamba warudipo makwao, mioyo yao itaridhika na mambo mazuri ya rehema na neema za Mungu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

59 Somo dogo geni sana, maneno matatu ninayotaka kuyazungumza toka katika Maandiko hayo yote. Huenda mkasema, “Hilo ni jambo ndogo sana, maneno matatu toka kwa yote uliyosoma, sehemu ya sura mbili za Biblia.” Bali ni—nilifanya hivyo nipate msingi wa kuyachukua maneno haya matatu: *Kuthibitisha Neno Lake.*

60 Mwajua, kuna Andiko katika Biblia, katika I Wathesalonike 5:21, ambamo imeandikwa, “Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema.” Jambo lo lote linapojaribiwa, au litathibitishwa “kweli” au “si kweli.” Na kukiwepo neno linalotiliwa shaka, sharti lijaribiwe hata utakapotambua ukweli. Kisha utakapopata lililo kweli, Lilisema, “Lishikilieni.” Kwa maneno mengine, “Likamateni sana, msiliachilie. Lishikeni!” Kwa maneno mengine, “Lishikeni kwa dhati, lisije likaponyoka.” Lishikeni lililo jema, baada ya kuthibitishwa kuwa “kweli.”

Na lo lote lililothibitishwa kuwa “si kweli,” basi liachilie upesi uwezavyo, likimbie. Usishikilie kamwe jambo lisilo sahihi.

⁶¹ Sasa, inawezekana kuwa Wakristo waaminifu, watu wazuri, wakati mwingine hushikilia, hushikilia jambo lisilo sahihi, wakidhani ni sahihi. Lakini basi mambo haya sharti yathibitishwe, kama ni “kweli” au “si kweli.” Na ni wajibu wetu sote, kwa kuwa tunatarajia kwenda Mbinguni Yesu ajapo. Na ni wajibu wa kila mhudumu, swali lo lote likiletwa, kwamba atalitatu hili, kisha alithibitishwe mbele ya watu, wapate kuelewa, kwa sababu hamna mtu anayetaka kupatikana “amekosea,” akishikilia jambo lisilo kweli.

⁶² Kwa hivyo tuna Andiko (na Yesu alisema, “Maandiko yote hayana budi kutimizwa”) ya kwamba hatuna budi kuthibitisha mambo yote. Ndiposa, “shikilieni,” ama, “shikeni sana, likamate kufa na kupona. Na msiliachilie, lishikeni lililo jema.”

⁶³ Nakumbuka shuleni, nilijifunza jambo fulani, na wengi wenu mlifunza somo lile lile. Ukisha tatua hesabu, ukisha ifanya, unaweza kuchukua jawabu na kuithibitisha kwa ile hesabu. Wangapi walifanya hivyo? Ninyi nyote, bila shaka. Ndipo—ndipo huna haja ya kuwa na wasiwasi au jawabu lako ni sahihi au la, jibu la hiyo hesabu limethibitishwa na hesabu yenyewe. Kwa hivyo, unajua umepata jawabu sahihi. Kama kila moja yako kwenye ubao ama karatasi imethibitishwa, jawabu likathibitishwa kwa . . . jawabu likathibitishwa kwa hesabu, basi umeipata. Hamna anayeweza kusema si sahihi, huna budi kupata . . . Na ukifanya kazi yako vizuri na barabara, na jinsi upaswavyo kufanya, na jawabu lako limethibitishwa, unaweza kuketi kitako na ustarehe ukiwa na hakikisho ya kwamba utapata A katika hilo, kwenye karatasi hiyo utakayoipeleka, kwa sababu tayari imekwisha kuthibitishwa, kuthibitishwa kwa ile hesabu.

⁶⁴ Sasa, pia kuna methali ya kale isemayo, “Ithibitishwe, nami nitaamini.” Naam, wana moja ya majimbo yetu, moja ya majimbo yetu katika taifa hili, wana msemu, “Nimetoka Missouri, nionyeshe.” Waona, kwa maneno mengine, “Nithibitishie, nimetoka Missouri.” Bali hili halitendeki kila mara, kwa sababu Mungu, katika kila wakati ametimiza na kuthibitisha kazi ambayo ameitenga kwa ajili ya wakati huo, na kuina katika Neno Lake. Na kila wakati ambapo Neno la Mungu limethibitishwa, katika wakati huo, wingi wa watu umelikataa. Kwa hivyo, “Nithibitishie, nami nitaliamini,” si sahihi. Unaweza tu kuwa na imani jinsi Mungu anavyokupa imani. Imani ni karama ya Mungu. Haidhuru wewe ni wa kidini vipi, hata hivyo haina budi kuchukua . . . huna budi kuwa na imani. Na imani yako inaweza tu kutulia, iwapo wewe ni Mkristo, juu ya Neno la Mungu lililothibitishwa.

⁶⁵ Basi, kumbukeni, Mungu alitenga Neno kwa kila wakati, na akatabiri yale yatakayotendeka katika wakati fulani huu aliokuwa akinena habari zake. Naam, kama Musa angelikuja na ujumbe wa Nuhu, haungalifaa kitu. Kama Yesu angelikuja na ujumbe wa Musa, haungalifaa kitu. Ama mmoja wa manabii angalikuja na ujumbe wa nabii mwingine, haungalifaa kitu. Bali kupitia kwa manabii Wake, Yeye amefunua utimilifu Wake wote pamoja na mpango Wake. Kwa hivyo Biblia haiwezi kuwa neno moja lililoongezwa Kwake wala Neno moja lililoondoshwa Kwake.

⁶⁶ Kwa hivyo ukithibitisha swali lako kwa...jibu lako kwa swali lako, basi mbona usithibitisha ji—jibu tunalopata sasa kwa Neno la wakati huu. Kama Biblia inanena ya kwamba jambo fulani litatendeka katika wakati huu, liko katika Biblia na litatendeka. Ndipo jibu lako unalojaribu kuwaambia watu, ikiwa limethibitishwa kwa kile Kitabu, basi ni kweli, ni kweli. Kama siyo, si kweli.

⁶⁷ Sasa tunaona mwingine, ndiposa ninyi, hapana shaka, mmewasikia wakisema, “Kuona ni kuamini.” Hiyo ni methali nyingine ya kale tuliyo nayo hapa, bali hiyo haifai kitu pia. Haifai kitu kwa sababu mwanadamu anaweza kuketi na kutazama cho chote moja kwa moja na hawatakiona. Neno “see” (ona), neno la Kiingereza “see” lina maana nyingi mbalimbali. Sea laweza kumaanisha “bahari ya maji.” Kisha see laweza kumaanisha “kufahamu.” See laweza kumaanisha “kuitazama.” Basi, lo, kuna namna nyingi za maneno unayoweza kutumia. Bali unaposema, “kuona ni kuamini,” umekosea.

⁶⁸ *Unapolifahamu*, unaliamini. Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi *kuuona* Ufalme,” kwa maneno mengine, “*kuufahamu* Ufalme,” kwa maana ule Ufalme ni Roho Mtakatifu ndani yako. Kwa hivyo huna budi hufahamu nini kilicho ndani yako. Na njia pekee utakayofahamia, ni kulinganisha yale kinachokufanya utende na yale Biblia inasema kitakufanya utende. Ndipo shida yako imetatuliwa, mnaona. Kisha, basi, Yeye ni huyo Roho Mtakatifu.

⁶⁹ Kwa hivyo, kuona si kuamini. Naweza kuthibitisha hilo kwa hisi za mwili, mnaona, ya kwamba kuona si kuamini. Siwezi kuona hii chupa ya mafuta. Singeiona kwa sababu iko nyuma yangu, bali nina hisi ya—ya kupapasa ambayo inianiambia nimeishika kwa mikono yangu. Mnaona? Sasa, singeiona, haiwezekani. Na sasa siwezi kuifikia, haiwezekani, hata hivyo naamini. *Huku*, kuona ni kuamini; *huku*, kugusa ni kuamini. Sasa nafumba macho yangu, singeiona wala kuigusa, bali nikiileta karibu ningesikia harufu, ningali naamini iko pale. Kwa hivyo, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana,” si kuona, kuonja, kugusa, kunusa wala kusikia. Unaliamini! Nayoy imani sharti ipate mahali pa kutulia. Na cho chote kilicho dhidi ya Neno la Mungu, imani katika Mungu

haiwezi kupata mahali pa kutulia isipokuwa iwe ni ahadi ya Mungu. Na hapo inachukua msimamo wake wa Milele.

⁷⁰ Bali na haya yote yasi...nyakati zenye mashaka na mambo ambayo tumekwisha kupitia na tunaishi katika hayo leo, mabaya zaidi ya yote, dhidi ya shaka hizi zote, Mungu yuaendelea kuthibitisha maneno Yake kuwa kweli, kama anavyofanya katika kila wakati. Yeye...Kutokuamini hakumkomeshi Mungu, hakumzuii. Sijali jinsi ulimwengu usivyoamini, ingali itatendeka tu. Kutokuamini hakufanyi cho chote ila kumhukumu yule asiyeamini. Kutokuamini kutapeleka asiyeamini Kuzimuni. Kutamnyang'anya kila baraka ambayo Mungu alimwahidi, bali hakumzuii Mungu kuendelea mbele na mwamini. Mnaona, kutokuamini hakumzuii Mungu, humzuia tu asiyeamini.

⁷¹ Mnasema, "Mimi...Jua halitaangaza kesho, nitalikomeshi." Jaribu. Unaona? Vema, huwezi kufanya hivyo. Mungu ameliweka katika taratibu na kusema lingeangaza, nalo litaangaza, hivyo tu, Yeye alisema lingefanya hivyo. Huenda kukawa na mawingu chini yake, bali lingali linaangaza sawasawa. Nawe huwezi kumzuia Mungu kwa hayo. Yeye, ambacho...

⁷² Yeye huwajulishaje watu Neno Lake? Kwanza, Mungu akijua ya kwamba kungekuwako na wasioamini...Sasa tazama hekima ya Mungu. Akijua kungekuwako na wasioamini, na jinsi wingi wa watu ungekuwa wasioamini. Yeye, kwa kujua Kwake tangu awali, alichagua tangu awali mbengu kwa kila wakati, ambayo ingeliamini. Sasa ukichunguza mle ndani, kwa kuwa kila wakati huendelea moja kwa moja na Neno Lake, kila kitu kwa wakati wake kabisa, hamna cho chote kinachomzuia Mungu. Yeye huendelea moja kwa moja, na kila mlilo wa saa unaendelea tu vema. Tunadhania, wakati mwingine, haitaendelea kufanya vema. Bali usiwe na wasiwasi, saa Yake hupima saa hata kwa nukta moja, na kila kitu kinatenda kazi barabara kabisa.

⁷³ Ninapotazama pande zote wakati mwingine na kuwaona hawa Wahuni na Hawara tulio nao siku hizi, na barabarani, na jinsi kila kitu kinavyoendelea, nawazia, "Ee Mungu!"

⁷⁴ "Ngoja kidogo," Yeye asema, mnaona, "Saa yangu inazunguka barabara kabisa. Sina budi kukuweka katika msingi ule ule nilivyomweka yule mtu wa kwanza, siku hizo. Nami nalikuweka katika msingi ule ule wa Luther, na kwa msingi ule ule wa Wesley." Kwa sababu, mwaona, dhambi haikujulikana wakati huo kama ilivyo sasa. Na tunapopata maarifa mengi sasa kuliko tulivyokuwa nayo wakati huo, kisha adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Mungu humwinulia beramu dhidi yake. Mnaona? Basi sasa siku hizi, tuna maarifa mengi, ufahamu mwingi zaidi, kwa hivyo mito ya kutokuamini inatiririka kasi,

bali Mungu huinua beramu dhidi yake. Bali, kumbuka, Yeye kila mara . . . Sababu yake—yake ya kuchagua tangu asili kwamba mambo haya yatendeke, Yeye aliyatabiri kwa manabii Wake ya kwamba yangetendeka. Na wenye haki wanapoonamambo haya yakithibitishwa, ndipo wao wanajua ni kweli. Bila kujali yale mtu ye yote asemayo, wao wanajua ni kweli.

⁷⁵ Tunaona kule katika—katika—katika, naamini, ni katika I Wathesalonike, Yeye alisema, “Yeye alituchagua tangu asili kufanywa wana katika Yesu Kristo.” Mungu, si kusema, “Nitawachagua ninyi, na sitawachagua ninyi,” bali kujua Kwake awali kulijua kile ungetenda. Kwa hivyo kwa kujua Kwake tangu awali Yeye anaweza kuweka katika utaratibu, Naye amefanya kila kitu kitendeke kwa manufaa Yake, na kwa manufaa yenu.

⁷⁶ Katika Mwanzo, Mungu alimwambia Adamu na Hawa nini kingetendeka walipoacha kuamini Neno Lake. Naam, aliweka mema na mabaya mbele yao, kisha akasema, “Siku mtakapoyala, siku hiyo mtakufa.” Na Mungu alimaanisha aliyosema hasa. Kila mara Yeye hufanya hivyo, humaanisha anachosema.

⁷⁷ Shetani alimfanya asiliamini, kwa kuwa Shetani mwenyewe hakuliamini kamwe. Yeye haliamini, kwa hivyo alimwelekeza Hawa asiliamini. Naye angali anatenda jambo lile lile, na kufundisha wengine jambo lile lile, nao hukosa kuliamini kama vile Hawa alivyofanya. Mungu aliwakinga watu Wake kwa Neno Lake, huo ndio ulinzi wako wa pekee. Si dhehebu lako, si baba yako ama mama yako, ni sawa, lakini nyuma ya Neno la Mungu. Hapo ndipo mahali ambapo mwamini hulindwa, nyuma ya Neno. Wakati hiyo njia ndogo ilipovunjwa pale, kwa msemo mdogo wa “nashangaa iwapo ni kweli ama si kweli? Haingaliwezekana,” kujadiliana kukaingia na kuchukua mahali pa imani, wakavunja zile kinga. Naye Mungu akatimiza Neno Lake, akalitenda. Shetani alijaribu kumfanya aamini . . . asiliamini.

⁷⁸ Ama, kujadili, usijadiliane nalo! We—wewe unasema, “Vema, naamini . . .” Huna haki. Mungu anaposema jambo lo lote, ji—jinsi tu alivyosema, hilo ndilo jambo la kutenda. Unasema, “Vema, nafikiri . . .” Bali huna wazo linalokuja. Iweni na nia iyo hiyo ambayo iliyokuwemo ndani ya Kristo. Na Kristo ni Neno! Acheni Neno liwe ndani yenu. Maneno mengine yote yawe si kweli, Maneno ya Kristo yawe kweli! Wengine wanamwamini na sababu zake zote, kama alivyofanya Hawa, jadili, “Vema, mbona Mungu atende hili? Naam, *hili* si ni zuri tu kama lile?” Iwapo ni kinyume cha Neno, sivyo! Kwa hivyo, kitu cho chote, mwalimu ye yote, mfafanuzi ye yote wa Biblia, kitu cho chote kile ambacho kingekufundisha au kujaribu kukufanya uamini lo lote yodi moja mbali na yale Biblia hii isemayo, ni fundisho la uongo. Ni Shetani, tena, sawasawa kama ilivyokuwa kwa Hawa. Mungu anaendelea moja kwa moja, hata afanyeje, Shetani afanyeje, Mungu anaendelea moja kwa moja akithibitisha kwamba ni hivyo.

⁷⁹ Sasa tazama alivyomwambia Hawa, “Hakika hutakufa. Utakuwa mwerevu.” Hicho ndicho ulimwengu unachotafuta siku hizi, thibitisho la kisayansi, maarifa ya mwanadamu. Naye alisema, “Hakika hautakufa.”

⁸⁰ Bali Mungu alikuwa amesema, “utakufa,” na Mungu akalithibitisha kuwa hivyo. Nasi tunaweza kuona, Yeye alimaanisha alilosema. Nenda hapa makaburini, utajua . . . kama alimaanisha hilo au la. “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Na ukienda hapa na kumchunguza mtu ye yote utakaye, wa wakati wo wote, hamna mwanadamu aliyeishi miaka elfu. Mungu alithibitisha Neno lake kuwa kweli, yeye atafanya hivyo kila mara.

⁸¹ Bali, kumbuka, Yeye hutimiza ahadi Zake zote za baraka na za laana Zake pia. Kwa sababu wao walikula, wakafa siku hiyo; Naye hukuthibitishia hilo, ya kwamba wao kweli wakila hufa siku hiyo. Yeye pia hutimiza kila Neno alisemalo kuhusu baraka Zake. Kila ahadi, Mungu huitimiza! Lo, napenda hilo. Huna budi kuchagua unalotaka: Baraka Zake, kwa kuamini; au laana Zake, kwa kulipotosha. Ukilipotosha na kuamini sehemu iliyopotoshwa, basi umelaaniwa. Ukiliamini jinsi tu alivyoliandika, na kulishikilia, basi unabarikiwa. Na kila mara huwa kinyume cha sayansi, kila mara ni kinyume na—na njia ya kisayansi ya watu ya kuonyesha mambo. Kwa maana Yeye hutimiliza kila Neno, la baraka Zake na laana Zake pia.

⁸² Wanaume na wanawake walipotenda dhambi sana katika ule ulimwengu kabla ya ile gharika, yeye . . . dhidi ya Neno Lake la Kweli, Adamu na Hawa walitenda dhambi dhidi ya Neno Lake la kweli. Lakini vizazi vyote vilivyowafuata vilipoanza kutenda jambo lile lile, Yeye akatangaza mauti juu yao, hatimaye ikafikia kuangamizwa kwa vitu vyote kabisa juu ya nchi, ikafunikwa na maji, ikaangamizwa kabisa kwa maji.

⁸³ Sasa, Mungu yule yule aliyesababisha maangamizi ya kila kitu juu ya nchi, kila mche, kila kiumbe ila kile alichohifadhi na kukiinua juu ya uso wa dunia, kila alichohaidi ya kwamba angetenda, alitenda. Na Mungu yule yule aliyeahidi maji, na akalitimiza Neno Lake, Mungu yuyo huyo ameahidi moto, naye atalitimiza Neno Lake. Atalitimiza Neno Lake.

⁸⁴ Sasa, sasa Yeye alifanyaje? Wao walijuaje Neno Lake? Kwa sababu njia Yake daima ya kufanya hivyo, ya kuthibitisha nafsi yake kabla hajafanya uharibifu wo wote, ama hajafanya hukumu yo yote, kila mara Yeye huwatumia watu Neno, na kila mara huwaonya watu. Lo, napenda hilo! Basi tunaweza kuona mahali tulipo hasa.

⁸⁵ Kulikuweco na kila namna ya wahudumu na mashirika katika siku za Nuhu, na kulikuweco kila namna ya dini katika siku za Nuhu, kwa kuwa Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa

Adamu.” Bali akatokea hadharani, nabii, naye akaanza kufanya jambo fulani, akaanza kujenga safina. Basi Mungu akamtuma nabii Wake, Nuhu, kuthibitisha ya kwamba Yeye aliisha tuma Neno Lake, akawaambia ya kwamba maangamizi ataleta, ya kwamba Yeye hangalivumilia mambo ambayo—ambayo hao watu walikuwa wakitenda, kwamba ilimbidi kuwaangamiza wanadamu aliokuwa amewaumba.

⁸⁶ Naam, Neno lilimjia nabii, kila mara, Yeye habadiliki. Malaki 3, ilisema, “Mimi ni Mungu, nami sibatiliki.”

⁸⁷ Nuhu alitumwa kwa wakati wa sayansi, akiwa na Ujumbe usio wa kisayansi. Nuhu alitumwa kwa wakati wa kiakili, akiwa na Ujumbe usio wa kiakili. Alitumwa kwa wakati wa sayansi, huku akiwa na Ujumbe wa imani pamoja na ahadi kwa wakati wa kisayansi. Kwa hivyo je, mngaliamini ya kwamba wakati wa kisayansi ungeliamini Ujumbe usio wa kisayansi? Wakati mkuu wa kiakili, basi ungeliamini wangeliamini jambo lililoonekana la kipuzi kabisa kwa akili za kibinadamu? Bali Mungu kila mara hutenda namna hiyo. Nuhu alikuwa nabii wa Bwana aliyethibitishwa, na ni Ujumbe wa Mungu wa wakati. Ilimbidi kuamini hivyo, iliwabidi watu waamini Ujumbe wake baada ya yeye kuthibitishwa na Bwana, ya kwamba ilikuwa Neno la Mungu, naye Mungu angetimiza Neno Lake.

⁸⁸ Sasa ni jambo lile lile siku hizi. Tuko katika wakati wa mwisho. Sasa, iliwapasa watu hao kujua, mnaona. Sasa, angalieni, Nuhu alikuwa mfano wa Wayahudi watakaopitishwa katika ile Dhiki. Henoko alikuwa mfano wa—wa Ujumbe halisi, wa kuhamishwa kwa Kanisa, kwa kuwa Henoko alinyakuliwa ndiposa gharika ikaja. Na wote wawili. . . Yule nabii wa kwanza, Henoko, aliondoshwa kusudi Nuhu apate kuendelea na—na. . . Mungu apate kuendelea na Nuhu. Na saa Kanisa litachukuliwa kusudi Mungu apate kuwashughulikia tena Wayahudi, wale mabaki ya Wayahudi, wale mia na arobaini na nne elfu, kama tulivyoeleza katika Maandiko hapa.

⁸⁹ Lakini katika kukabiliana na wakati huu wa kisayansi, usioamini, Mungu alithibitisha Neno Lake la ahadi kuwa kweli, kwa kuwatumia wao gharika. Sasa, kumbukeni, katika siku za Nuhu, haikuwa imenyeshwa nchini. Mungu alifanya ukungu kupanda katika nchi, ukainyweshea, bali haikunyeshwa. Bali Nuhu alisema, “Itanyesha.” Sasa hivyo ilikuwa. . .

⁹⁰ Wao wangekitwaa chombo cha kupimia na kukirusha juu angani, wakasema, “Hamna unyevu kule juu. Hamna mvua kule. Tunaweza kuthibitisha hamna mvua mle.”

⁹¹ Bila kujali ilivyosema sayansi, Mungu alisema, “Itanyesha,” kwa hivyo hilo hilitenda. Basi, Mungu alifanyaje? Nionavyo mimi, wakati wengine wao waliitikisa dunia kidogo na kuiondoa mahali pake, kisha ikarushwa hivi, joto la nchi likawa baridi, likatoa tu ule—ule unyevu. Ndipo ulimwengu ukafunikwa,

kwanza, na anga kule juu, ule unyevu wa hewa, ukaunganika katika mfano wa wingu nalo likashuka, hivyo tu.

⁹² Sasa tunajua leo, kuna moto kule juu, kwa maana hizo gesi ziko duniani. Na Biblia ilisema, “Mbingu na nchi zitatoweka kwa mshindo mkuu, na dunia itayeyuka kwa joto kali sana.” Kwa hivyo tunajua ya kwamba iko kule juu, kwa hivyo ni kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.

⁹³ Na sasa kumbukeni, ule Ujumbe wa wakati wa Nuhu ulikuwa tu kwa imani, na haukuthibitishwa kisayansi. Bali, leo, Ujumbe unalingana na Neno la Mungu, na ukathibitishwa kisayansi. Eliya alikuja kwanza, akitenda miujiza, bila kuhubiri; akienda tu mahali mahali, akifanya miujiza. Wakati uliofuata, akaja katika mfano wa Yohana Mbatizaji, akaja asifanye miujiza, akihubiri tu. Na mara ya tatu ajapo, kuna miujiza na mahubiri pia. Mnaona? Mnaona jinsi ilivyo? Tazama Maandiko yanavyoshikamana. Tungetumia muda mwingi sana juu ya hilo, bali hatutafanya hivyo, tutayaacha, kwa sababu naamini mnapata hilo wazo.

⁹⁴ Yeye alifanya katika wakati huo jinsi tu alivyoifanya katika nyakati zote, na kama atakavyofanya, jinsi tu alivyoahidi kufanya. Mungu huahidi cho chote, kisha anashuka na kuthibitisha Neno Lake kuwa kweli. Wote waaminio, wote waaminio Ujumbe wa wakati huo, wakaja wakaokolewa. Ndivyo itakavyokuwa katika wakati wo wote. Wote ambao hawakuamini ujumbe pamoja na mjumbe, wakaangamia.

⁹⁵ Na wote ambao kweli wanaliamini Neno la Mungu leo, watatwaliwa. Wote wasioamini Neno la Mungu, wataangamia pamoja na ulimwengu, kwa kuwa wao ni wa ulimwengu, na cho chote kilichomo ulimwenguni, hakina budi kuangamia na ulimwengu. Na kila kitu kilichookolewa katika Mungu, hakina budi kuwa katika Mungu, na hakiwezi kuangamia, “Nitawapa Uzima wa Milele na kuwafufua katika siku ya mwisho.” Naam, ni faraja jinsi gani kwa kila mwamini kujua unapokuwa katika Kristo, ya kwamba bila shaka kama Mungu anavyolitimiza Neno Lake na kuangamiza ulimwengu, Yeye hutimiza Neno Lake na kuwainua watu Wake na kuwaokoa. Yeye hulithibitisha.

⁹⁶ Yeye huthibitisha Neno Lake la ahadi kweli kwa Ibrahimu katika kizazi chake. Tazama, ulikuwa usio wa kisayansi, katika wakati wa Ibrahimu, kwa mtu mwenye umri wa miaka mia, na mwanamke wa miaka tisini, kwao kumpata mwana, wakisha kupita ule umri. Bali Ibrahimu hangaliweza kulieleza. Angewendea daktari, akasema, “Daktari, inawezekana?”

⁹⁷ “Haiwezekani!” Anaenda hospitalini na kumtayarisha yule mama kumpata mwana, ama cho chote kile ukitaka kuilinganisha na wakati huu, wao wangelimwita mwenda wazimu, “Yeye amerukwa na akili.”

⁹⁸ Bali Mungu alisema! Na yeye...Biblia ilisema katika Warumi, sura ya 4, ya kwamba, "Ibrahimu, akiona ahadi ya Mungu, hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu. Kwa kuwa yeye alivumilia kama kumwona Yeye asiyeonekana, na akaridhika, akashikilia." Akaing'ang'ania kwa kuwa yeye alishawishika kuwa kile Mungu alichohidi, Mungu aliweza kukitenda! Nasi inatupasa kuwa watoto wake. Amina! Sasa najisikia wa kidini, kuchangamka, wazia tu hilo! Lo, Yeye alilithibitisha, baada ya miaka hiyo yote, akamgeuza Ibrahimu, na Sara kuwa kijana mwanamke, kisha akapata mtoto. Basi Ibrahimu na Sara waliishi... Miaka arobaini na mitano baadaye, Sara akafa, kisha Ibrahimu akaoa tena alipokuwa na umri wa miaka mia na arobaini na mitano, naye akawapata wana wengine saba bali na binti zake. Huku, Ibrahimu alikuwa tayari amepita umri wa kuwapata watoto, alikuwa mgumba, ha—hakuwa na mbegu, hamna uhai uliobaki ndani yake, karibu yapata miaka mingine mia kabla ya hayo. Amina! Kwa nini? Hakufikiria mwili wake mwenyewe, hakufikiria ufu wa tumbo la uzazi la Sara. Alifikiria tu yale aliyosema Mungu, na alijua Mungu angethibitisha yale aliyosema. Amina! Mungu huthibitisha yale Yeye asemayo atatenda. Kati ya yasio ya kisayansi na yaliyo ya kisayansi, na—na miongoni mwa cho chote kile, hata kiwe nini, Mungu huthibitisha ya kwamba Yeye yu sahihi, kila mara huthibitisha Neno Lake. Yeye yu kweli, wengine wote wamekosea.

⁹⁹ Pia alilithibitishia Lutu, wakati aliposema, "Usipoondoka katika mji huu, nitauteketeza." Kisha akamwambia Ibrahimu, kama angalipata "watu kumi," angeuokoa huo mji. Naye hangewapata watu kumi, kwa hivyo akathibitisha Neno Lake kuwa kweli.

¹⁰⁰ "Moto utatoka wapi? Hamna wo wote humu mialoni, huku kwenye mashimo haya ya matope." Bali Mungu alisema hivyo, na Ibrahimu alijua ingetendeka. Lutu alijua ilikuwa hivyo, naye akakimbilia mlimani.

¹⁰¹ Yeye aliahidi uzao wake ungekuwa mgeni katika nchi isiyo yake, na kutoeleweka na kuchukiwa na watu, nao wangekuwa wapitaji, uzao wa Ibrahimu, kwa miaka mia nne kati ya wageni, watu wa kigeni. Naye akalitimiza Neno Lake sawa kabisa kama alivyosema angefanya. Uzao wa Ibrahimu kweli ulikuwa mgeni katika nchi ya Misri kwa muda wa miaka mia nne. Yeye aliahidi, pia, kuwakomboa kwa mkono wenye nguvu. Mkono wenye nguvu, Yeye angewakomboa wale watu toka katika utumwa wa Misri. Naye akalitimiza Neno Lake. Tazama yale aliyolazimika kutenda kuwapeleka wanawe kule Misri. Ilionekana kama kwamba mkasa ulikuwa umewapata, ulikuwa unawapata, na kila kitu.

¹⁰² Ilionekana kama kwamba...ilikuwa vibaya sana kwa Yusufu kudhaniwa mfu, na maskini Isaka...au Yakobo,

babake. Au Isaka, baba yake...hasa, kwa Yakobo, huyo ndiye, Isaka aliyekuwa babuye. Yakobo, babaye, kuamini kuwa mwanawe mwenyewe alikuwa tayari ameuawa na wanyama. Jinsi ilivyokuwa vigumu kwa maskini Yusufu kujua ya kwamba maskini kijana huyo, akiwa mbali na watu wake, aliyesalitiwa na ndugu zake, akatupwa shimoni, akidhaniwa amekufa, damu ya kondoo ikapakwa kwenye kanzu yake, ambapo, wao walikuwa wamemchinja mwana-kondoo wakamle, wakaipaka damu na kumpelekea babaye, huku anajua haya yote. Bali Yusufu angekumbuka jambo moja, ya kwamba mkono wa Mungu ulikuwa juu yake. Alijua ya kwamba yeye alikuwa mwamini. Haidhuru ndugu zake walimkataaje, jinsi hawakushirikiana naye ama cho chote kile, Yusufu alijua Mungu angetimiza Neno Lake. Alipoona lile ono la hao wote wakipiga magoti mbele zake, yeye alijua hayo hayana budi kutimia kwa maana yalikuwa BWANA ASEMA HIVI. Amina. Sijali jinsi yalionekana yasivyo na busara, Yusufu alijua ilikuwa kweli. Haidhuru kazi ilikuwa ngumu vipi, na yale yeye aliyopaswa kupitia, yeye alijua siku moja kila mmoja wao atampigia magoti miguuni mwake. Yeye angefanyaje hayo huku wao walimchukia? Bali yeye alijua Mungu angethibitisha Neno Lake kweli, kila wakati.

¹⁰³ Ndivyo Yeye atakavyofanya leo! Mungu atathibitisha Neno Lake kweli, haidhuru sayansi itasemaje, “Haiwezekani.” Hata tuelimike vipi, tuwe na akili vipi, jinsi makanisa yamepotelea katika hali ya kidesturi na kadhalika, Mungu angali athibitisha Neno Lake “kweli.” Tulieni katika hilo Neno.

¹⁰⁴ Naam, Yusufu alipitia katika shida nyingi, lakini, kushuka kwenda Misri, lakini Mungu akampandisha kutoka kule jinsi hasa alivyokuwa amesema; mfano bora sana wa siku hizi, kama tungalikuwa na wakati wa kuyaingilia. Naamini tumefanya hivyo, hapo awali, hapa Maskanini, tumeyaeleza. Bali Mungu alitimiza Neno Lake, kwa maana, iliwabidi kukaa kule. Ilikuwa vigumu kwa wale wana Waebrania kule chini katika utumwa wa Kimisri, ambao walikuwa wamebarikiwa na kupewa matunda ya nchi, mahali bora sana, Gosheni, kutambua ya kwamba iliwapasa kuwa watumwa; na wale mama kulazimishwa kuweka mikononi mwa askari wa Kimisri, wazao wa tumbo zao, hao watoto wao wachanga na wapendwa, na kumwona yeye akisimama pale, akichukua kisu kikubwa na kupasua na kumtupa ardhini kumtupa kwa mamba. Naam, lilikuwa jambo gumu kwao, kupitia hayo.

¹⁰⁵ Bali siku moja yule mzao aliyechaguliwa tangu awali akazaliwa, mwana halisi. Kulikuweko na kitu fulani kumhusu yeye kilichoonekana cha kigeni. Kule upande wa nyuma wa jangwa, siku moja, Roho Mtakatifu alishuka katika mfano wa Nguzo ya Moto akakaa kijitini, akasema, “Nimesikia kilio cha watu Wangu, nami nakumbuka ahadi Yangu. Na wakati wa ukombozi umefika, nami nitakutuma kule kutenda hayo.”

Akiwa na fimbo mkononi mwake, mkewe juu ya nyumbu, mtoto mchanga pajani mwake, yeye alifanya hivyo kwa uweza wa Mwenyezi Mungu. Jambo la kuchekesha sana, fi—fimbo iliyokunjana ingelifaa nini kwa mikuki elfu kumi? Lakini, waona, Mungu yuko ndani yake. Inategemea Neno Lake lilipo. Musa alikuwa na Neno Lake, Farao alikuwa na mikuki. Musa alikuwa na Neno.

¹⁰⁶ Hilo tu ndilo alilohitaji, ilikuwa Neno. Hilo tu ndilo unalohitaji leo. Si kitambulisho kutoka kwa kanisa fulani. Hauhitaji kuungwa mkono na dhehebu. Unahitaji Neno, kunyakuliwa Kwalo. Huhitaji kitambulisho fulani. Huhitaji historia ndefu ya shule fulani, kuponywa asubuhi ya leo. Unapaswa kulikubali Neno, hilo latosha!

¹⁰⁷ Hauhitaji neno la daktari. Daktari akisema amefanya yote awezayo kufanya, hayo tu ndiyo awezayo kufanya. Akisema una kansa, kivimbe, unakuwa kipofu, u kiziwi, bubu, cho chote kile, hiyo haidhuru. Kama ungalichukua hilo Neno ulipeleke kwenye hiyo ahadi ya kijiti kilichowaka moto mle, amina, jambo fulani litatendeka! Mungu atathibitisha Neno Lake kuwa kweli, kila wakati linapokelewa katika msimamo halisi. Hicho ndicho unachohitaji, Neno Lake. Yeye hulithibitisha, hilitunza. Waweza kuwa na hakika ya kwamba ni kweli.

¹⁰⁸ Yeye hulithibitisha Neno Lake katika kila kizazi, kwa njia ya ajabu sana, bali Yeye daima hutenda hivyo kwa njia ile ile. Mnaona? Yeye alifanyaje katika siku za Nuhu, anapokuwa tayari kuwakomboa waliosalia? Aliwatumia Nuhu, yule nabii. Akamtuma Nuhu, ishara.

¹⁰⁹ Na sasa tazama, ajapo kuwakomboa wana wa Israeli, anafanyaje? Njia yake ile ile, anamtuma nabii Wake. Nabii Wake ana Neno. Zile ishara na maajabu ya Neno lililoahidiwa yanaliunga mkono, ya kwamba ni Kweli kabisa. Israeli walipiga hatua wakaingia ile nchi ya ahadi, kwa sababu waliliamini.

¹¹⁰ Na katika ile safari ya jangwani, ikawa ya kwamba wao hawakumwamini huyu nabii, baada ya kuona Neno likithibitishwa sana, yule Bibi—arusi alipiga hatua baya (mwajua ninalozungumzia, katika lile ono, mnaona, “wakipiga hatua baya”). Kulikuweko mmoja aliyesimama, jina lake Yoshua na Kaleb, akaamini lile Neno la ahadi kuwa ni kweli, bila kujali hali ya mambo ilivyokuwa.

¹¹¹ Tazama walipofika Kadeshi-barnea. Kule Kadeshi-barnea, Musa alimtuma mmoja toka kwa kila kabila, waende wakaipieleze ile nchi, waone wangeingilia njia gani. Naye akamtuma jemadari wake, Yoshua, aliyekuwa nabii, kwa hivyo akamtuma nabii, mdogo chini ya Musa. Naye Yoshua akamsikiza Musa. Nao wakamtuma, kwa hivyo yeye akasema, “Ondokeni mwende mkaipieleze ile nchi.”

112 Kisha yule jemadari akatoka akajitwalia mtu mmoja toka kila kabila, na wakaanza safari. Akamchukua Kalebu, rafiki misri wake, kwa sababu alijua Kalebu aliamini. Wao wakaingia katika nchi ya ahadi, wakarudi na kichala cha mizabibu kilichohitaji watu wawili kukibeba. Mnaona? Yeye akasema sasa, “Kusudi Israeli wapate thibitisho kabla hata hawajaingia kwenye nchi ya ahadi. Mnaona, watapata thibitisho ya kwamba Mungu alisema hiyo ni nchi nzuri, na imejaa maziwa na asali. Ni nchi yenye fahari. Ni nchi nzuri. Sasa. . . Lo, maskini vitunguu saumu vyote, na vitunguu vidogo, na vyote mlivyo navyo hapa Misri. Sasa tunawapeleka katika nchi yenye maziwa na asali. Huenda ikawa hamjapata kuonja vyote viwili, kule Misri miaka hii yote. Wao waliwapa tu posho ya watumwa. Bali mnaenda kwenye nchi hii.” Kwa hivyo wakati tu walipofika yapata safari ya siku moja, ambapo Kadeshi-barnea, kilipokuwa kile kiti kikuu cha hukumu ya ulimwengu, wao wakasimama chini ya hii—hii minazi mikubwa kule nje, zile chemchemi, wakapiga kambi. Akasema, “Basi, kuwafanya watu hao wajue. . .” Tazama ilivyo kamilifu, timilifu, na jinsi ulivyo ushahidi halisi, jinsi Mungu afanyavyo hilo kama tu afanyavyo siku hizi. Yeye alisema, “Naam, Mungu alisema, ‘Nchi hiyo ni nzuri sana.’ Sasa kabla kuvuka, nawataka muione nchi hiyo ni kuu. Kwa hivyo nendeni mkaniletee ushahidi fulani wa hiyo nchi nikawaonyeshe watu.”

113 Basi wakapanda wakaenda kule. Na, sasa, kila mara unaporudi kuleta ushahidi, ndiyo huyo adui amejificha njiani. Wakati baadhi ya watu hao walipotazama kule na kuwaona hayo majitu makubwa ya Kanani, lo, jamani, wao walisema, “Hatuwezi kufanya hivyo.” Bali walirudi na ushuhuda ya kwamba hiyo nchi ilikuweko. Hawakuwa wameongozwa vibaya. Mungu alikuwa akiwathibitishia Neno Lake, hata kabla wao hawajaingia katika ile nchi.

114 Hamwoni, siku hizi, ya kwamba kama mkiendesha magari maili elfu moja kulisikia Neno, na kuliona likithibitishwa na kuhakikishwa, ni ushahidi ya kwamba ni nchi nzuri sana. Mnaweza kuona kivuli cha mtu kimelala, yuafa kwa kansa, “Na apone.” Na tunaona Maneno ya Mungu aliyosema yangetendeka siku hizi, yakithibitishwa, ni ushahidi ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake. Kuna Nchi kuu mno. Ikiwa maisha yangu yako karibu kwisha, na Mungu ashuke na kuyarejesha tena, hilo laonyesha ya kwamba kuna ushahidi wa Uzima wa Milele. Ambapo, wakati mmoja wewe haungalithubutu kuingia katika mlango wa hilo kanisa, sasa unapanga mstari kuingia mle. Ni ushahidi. Mungu hutimiza Neno Lake na kulithibitisha kwako, kwamba ni kweli.

115 Naendesha gari maili elfu moja, naja humu asubuhi na nikatazama kule kuona watu hao wakiwalisha watoto wao kwa chupa ya Coca-cola, nafaka kidogo, yapata saa kumi

na moja za asubuhi, wameketi kule. Niliwazia, “Ee, Mungu ningekuwa mnafiki aliye duni sana duniani, kuwaacha watu wasafiri umbali huo wote, kisha niwaambie neno ambalo si kweli. Kwa maana ninawasikitikia, moyo wangu unawapenda. Wana njaa na kiu cha Mungu. Nisaindie, Bwana, kuwaambia yaliyo Kweli, la sivyo, niondoshe katika huu ulimwengu. Hebu niwaambie hao watu yaliyo Kweli, kwa hivyo nisaidie, Mungu.” Nikasema, “Nishike mkono, ukaniruhusu kujua yaliyo Kweli, kisha ukaunge hilo mkono kwa kuthibitisha niliyosema kuwa ni Kweli, wapate kujua ya kwamba ni Kweli. Usiwaachilie maskini watu hao wapotezwe. La.” Jinsi moyo wangu upendavyo jambo kama hilo, kuona watu waaminifu.

¹¹⁶ Nakisia Yoshua aliwazia jambo lilo hilo, siku hiyo yeye alipowakusanya pamoja, alipowaona wakifua nguo zao na kujitayarisha kwa ajili ya siku ya tatu. Naam, Yeye alilithibitisha. Sasa Yoshua alisema nini? Wao waliposema, “Lo, hatuwezi kulitenda. Hauwezi kufanya hivyo. Itatubidi kutoka kwenye dhehebu letu. Tume—tume—tumekwisha. Unaona, hatuwezi kufanya hivyo sasa. Hatuwezi kufanya hivi, kwa maana halina maana.” Kisha Yoshua alipowaongoza mle, ilikuwa mwezi wa Aprili, wakati wa mafuriko, na Yordani ulikuwa karibu mpana kama Mto Ohio. Ilionekana kama kwamba Mungu alifanya kosa baya sana.

¹¹⁷ Wajua, wakati mwingine wewe huwa mgonjwa, nawe husema, “Vema, mimi ni Mkristo. Mungu, Yeye—Yeye alifanya kosa, Yeye aliacha niwe mgonjwa, nami ni Mkristo.” Je, hamkubuki kuwa Biblia ilisema kuwa mambo yote hutendeka pamoja na kuleta mema kwa wale wampendao Mungu?

¹¹⁸ Pale ambapo Yoshua aliwaongoza, sasa, Yordani hupunguka maji sana. Unaweza kuvukia po pote pale, isipokuwa ufikie kilindi cha maji ambapo pana kina kirefu sana; unaweza, pamoja na vivuko vyote vidogo na kadhalika hapo kwenye—kwenye zile pwani ulikokuwa Yeriko. Kwani, ni kwa sababu, waweza kuvuka kwa miguu, hayana kina kufikia kifundo cha miguu, kuvuka kwa gari, kuendesha, kuvuka kwa mnyama, kuvuka kwa miguu, au cho chote kile. Lakini Yeye aliwaongoza kule mnamo mwezi wa Aprili, wakati ile nchi iliyofurika ilifurika pale kwa upana wa maili moja. Yale maji yalikuwa na kina cha futi thelathini ama arobaini mle. Naye alisema, “Mnamo siku ya tatu, tutavuka. Mungu alisema hivyo! Wakusanye watu ukawatakase, kwa kuwa, siku ya tatu, mtavuka Yordani.” Waona jinsi Mungu huruhusu jambo hilo kutendeka? Ili tu kufanya, kuwafanya watu. . . kusudi apate kuutoa umati Wake. Wangefanyaje? Walijitakasa wakajitayarisha, bila kujali yale maji yalikuwa yenye kina kirefu vipi, ama jinsi yalivyojaa matope, na jinsi mkondo wa maji ulivyoenda kasi. Mnaona, wao walijua ya kwamba Mungu angethibitisha Neno Lake.

¹¹⁹ Haidhuru nini, jinsi unavyokaribia Yordani, haidhuru uko katika hali gani, kama tu ungeshikilia ahadi hiyo ya Mungu moyoni mwako, Mungu ataithibitisha, ya kwamba ni kweli. Kati ya kutokuamini kwote, Yeye bado atalithibitisha kuwa kweli. Naam, Yeye hufanya hivyo. Na hali za mambo hazimzuii, Yeye bado atafanya vivyo hivyo kama alivyofanya wakati huo.

¹²⁰ Tazama, Yeye huthibitisha Neno Lake kwa waamini Wake. Yeye aweza tu kuthibitisha Neno Lake. . . si kwa wasioamini, Yeye aweza tu kuthibitisha Neno Lake kupitia kwa waamini. Haidhuru hao wengine walidai kuwa hivyo vipi, “Lo, naamini, ndugu!” Tazama, kama unaamini, Mungu ataithibitisha kuwa kweli, kwa maana sisi hutazama na kuona wale wengine. Tunaweza kusemaje, basi? Mnaona, Yeye huthibitisha Neno Lake kupitia kwa waamini wa kweli, si kwa wale wanaosema wanaamini, bali wale wanaomini hakika. Yeye huthibitisha Neno Lake kwa watoto Wake wanaoamini.

¹²¹ Sasa, yeye alikuwa na waamini. Yale mazao ya zamani yalikuwa yamekufa, wale wasioamini waliosema, “Hatungeitwaa hiyo,” aliachilia kila mmoja wao aangamie (kwa nini?), kila mmoja wao ila waamini. Nani aliyesalia? Musa alikuwa amekwisha kutwaliwa akapelekwa utukufuni. Nao wale wasioamini tayari waliisha kufa jangwani, na hawa walikuwa watoto wao. Ni wawili tu waliovuka, nao walikuwa wale waamini, Yoshua na Kaleb. Hao walikuwa waamini, hao ndio waliovuka. Ndiyo njia pekee Mungu anayoweza kufanya hivyo, ni kwa watoto Wake waaminio. Mnaamini hivyo? Vema. Waamini Wake ndio waliofanya hivyo. Aliwatumia kuvukia. Mnaona?

¹²² Sasa nataka mtambue, Yeye hufanya hivyo katika kila wakati. Yeye hutumia njia iyo hiyo kila wakati, hana budi kuwachukua waamini. Kisha, kusudi waamini wapate kutimiza Neno hilo, hana budi kuwachagua tangu asili kwa wakati huo. Mnaliona? Hana budi kuchagua tangu asili jambo hilo kuweko kukabiliana na shindano la wakati huo. Je, mlilipata? Je, mlifahamu hilo? Je! mmeliona? Mmelielewa? Hilo ndilo linalotendeka siku hizi, Yeye alililichagulia hili tangu awali, kwa kujua Kwake tangu awali. Yeye alipochagua tangu awali, katika Malaki 4, halina budi kutendeka. Yeye anapokuja na kuchagua tangu awali lo lote litendeke katika Neno Lake, hana budi kuthibitisha Neno Lake kuwa hivyo. Anapochagua tangu awali jambo litendeke na kusema litatendeka, Yeye anajua ya kwamba hivyo mbegu itakuwepo pale wakati huo hasa. Alimchagua Bibi-arusi tangu awali, lazima atakuweko! Kutakuweko na kunyakuliwa, lazima Bibi-arusi aweko! Yeye huchagua tangu awali kwa kujua Kwake hapo awali. Mnaona, hamna kitakachoikomesha.

¹²³ Mungu alipowaambia, “Sasa, nawapa ninyi ahadi ya nchi ya ahadi. Nalimwambia baba yenu, Ibrahimu, kwamba watoto wake wangekuwa wageni humu kwa miaka mia nne.”

124 Basi Musa alisema, “Mimi ni nabii wa Bwana. Sasa tazama uone yale ninayotabiri. Yakitimia, basi mtajua nimetumwa na Bwana, kwa kuwa mnajua ya kwamba Mungu tayari amewaambia hilo. Sasa, sasa kama nikitabiri *hili* kisha litendeke, na *lile* halafu litendeke, na *hili* na litendeke, kila wakati vivyo hivyo tu, basi mtajua nimetumwa na Bwana kuwaambia. Sasa, kuna nchi ya ahadi, ambayo Mungu aliahidi. Mnaona? Naye Mungu aliahidi nchi hii. Sasa, ni nchi nzuri, yenye wingi wa maziwa na asali. Nifuateni.”

125 Nao walipokwenda jangwani ambako alipaswa kusafiri, kuwapeleka jangwani, ambako, Mungu alimwambia awarudishe kwenye Mlima wa Sinai, ndipo Mungu akashuka mbele ya Israeli wote, kwa Nguzo ya Moto, na kuthibitisha mambo ambayo Musa alikuwa amesema, yalikuweko, akithibitisha ya kwamba ilikuwa kweli, akiimarisha Musa pale, “Musa alisema ya kwamba Nilikuwa juu ya Mlima huu, Nilimtokea katika mfano wa kijiti kilichowaka moto. Na sasa nimeufanya mlima wote uwake moto.”

126 Wao wakasema, “Hilo! Usiache Mungu anene, hebu Musa anene. Tutaangamia.”

127 Yeye alisema, “Si—si—sitafanya hili tena. Nitawainulia nabii, yeye ata—yeye atazungumza nao katika Jina Langu.” Kwa hivyo, hivyo ndivyo atendavyo, jinsi hasa anavyoendeleza Neno Lake.

128 Tazama basi hao ambao hawakuamini, baada ya kuikaribia kabisa nchi ile kwamba hawakuamini. Sasa, ninyi mnaoandika kwa ufupi, andikeni Waebrania 6, papa hapa ambapo ilisema, “Wao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washiriki wa Roho Mtakatifu, ya kwamba, wakianguka, kuwafanya tena upya hata wakatubu, kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfadhehi kwa dhahiri; haiwezekani kwa hao kuokolewa.” Mnaona, vile ambavyo haiwezekani kwao kuvuka waingie katika hiyo nchi ya ahadi.

129 Watu huja hata wakafikia Ubatizo wa Roho Mtakatifu, wao watakuja moja kwa moja hata kwa Neno, watapitia katika madhehebu yote, na makanisa yote, na katekisimu zote, na kila kitu, bali ifikiapo hilo Neno, huo mstari wa kuvukia, wao husema, “Lo, sijui kuhusu Hilo, kanisa langu halifundishi Hilo hivyo.” Sijali kanisa Lako linafundisha nini, Biblia inasema ndivyo ilivyo. Ndipo unasema, “Najuaje ni kweli?” Yeye huithibitisha, na kuihakikisha!

130 Sasa, Biblia siku hiyo, ilisema, “Kuna nchi nzuri kule ng’ambo, na ina wingi wa maziwa na asali, na zabibu nzuri na kukungumanga” na, lo, ni mahali pazuri.”

131 Vema, wao walisema, “Naam, wengine wenu ingieni kule kisiri mkapeleleze, kisha mrudi, ili tukawafariji watu hawa.

Tutavuka mara moja sasa, iwapo ninyi nyote mtaamini tu.” Vema, wakashika njia wakaenda.

¹³² Ndio hawa wanarudi, lo, wawili wao, wakipiga shangwe, “Vema, Bwana asifiwe! Tumeiona! Tumeiona! Jamani, ni ya ajabu, hamna iliyo kama hiyo!” Hao wengine, hao kumi wakisimama pale, wakisema, “Lo, la, la, la, la, hatuwezi kufanya hivyo.” Wangapi walivuka? Hao wawili! Hiyo ni kweli. Hao wawili, kwa sababu walijua Mungu angethibitisha Neno Lake kuwa kweli. Tazama, hamna kufurika kwa Yordani, la, bwana, hamna kingo za Yordani zilizofurika, wala majitu ya Kanani wanalihakomesha. Mungu alithibitisha Neno Lake huwa kweli, Yeye aliwapeleka moja kwa moja hadi mle nchini.

¹³³ Yeye atafanya jambo lile lile tena, naam, bwana, katika ahadi ya siku hizi. Yeye huthibitisha Neno Lake. Si hoja, Yeye huthibitisha Neno Lake.

¹³⁴ Yeye alifunga vinywa vya simba wala—watu wenye njaa siku moja, kuthibitishia Neno Lake lilikuwa kweli, ya kwamba Yeye angeweza kuokoa, nabii Danieli. Nao waliwalisha hao simba nyama za binadamu. Nao waliwaacha hao simba wapate njaa, kusudi mtu akianguka mle ndani, au mtoto au cho chote walichokitupa mle ndani, ilikuwa hukumu ya kifo, ya kwamba hao simba wanaliharua vipande-vipande, hili kundi la simba wenye njaa. Nao wakamchukua huyu nabii aliyekuwa na Neno la Bwana kwa Waisraeli, ambayo ilitabiriwa kwamba ingetendeka. Ndiye huyo hapo pamoja nao. Bali Mungu hakuwa amemaliza kazi, Yeye alitaka kuthibitisha Neno Lake, Yeye angeweza kuokoa. Nao wakawaacha hao simba waone njaa, kisha wakamtupa yule nabii mle ndani, nao wakamjia mbio hivyo. Hiyo Nguzo ya Moto ikisimama pale (na mnyama ye yote anatishwa na moto), hiyo Nguzo ya Moto ikisimama pale, hao simba wakalala chini. Yeye alitimiza Neno Lake. Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu hutimiza Neno Lake, hulithibitisha, hulithibitisha kuwa kweli.

¹³⁵ Basi, Yeye aliondosha joto toka kwa ile miali ya tanuru iliyowaka moto, kuthibitisha Neno Lake lilikuwa kweli, ya kwamba Yeye angewaokoa na moto. Papo hapo kati ya hiyo miali, ambamo hao watoto walitupwa mle, na kukaa mle ndani kwa muda mrefu, huku wale watu waliowatupa humo, lile joto jingi la ile—la ile tanuru liliwauwa hao wanajeshi wakuu waliokuwa wakiwaongoza kule. Naye Mungu akaachilia huo moto uendelee kuwaka, bali akaondosha lile joto mle. Yeye huthibitisha! Kama ukimshindania, Yeye atakushindania. Akushindanie? Vema, hakika! Saa moja baadaye wao wakaufangua mlango, wakasema, “Aisee, hata hivyo, mliwatupa wangapi mle?” Kasema, “Twaona watatu tuliowatupa mle.” Akasema, “Kuna wanne mle, na mmoja wao ni mfano wa Mwana wa Mungu.” Unaona, Yeye huonyesha! Sababu gani? Yeye ni Neno.

¹³⁶ Nao walisema, “Mungu anaweza kutuokoa na tanuru hiyo, bali, kama sivyo, hatutaisujudu sanamu yo yote, kwa maana tunasimama kwa Neno.” Sanamu yo yote, namna ya dini, ikimbie. Mungu atakushindania. Yeye ataondosha lile joto toka kwenye mateso. Yeye atondoa uhai ka—katika kansa. Ataondosha . . . Atafanya cho chote, Yeye ni Mungu! Mshindanie, atakushindania. Yeye huthibitisha Neno Lake kweli, kila wakati. Aliondosha ukali wa moto katika miali mikali ile ya moto, akafunga vinywa vya simba, na kadhalika.

¹³⁷ Hapa pana jambo jingine alilotenda Mungu, kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Mwanadamu alifikia mahali ambapo, baadaye kule jangwani, hata walikuwa wakijipatia wenyewe elimu, wakijifanya watu wakuu. Wao walikuwa na madhehebu kadhaa yaliyoitwa Mafarisayo, Masadukayo, Waherodia, na kadhalika. Nao walikuwa watu mashuhuri. Walijifanyia makuhani wao kwa wao. Nao walitenda mambo makuu hivyo wakijitwalia makuhani wakuu na watu wakubwa, na waheshimiwa na kadhalika.

¹³⁸ Bali Mungu katika hayo yote, Yeye alimwinua nabii, mwana wa kuhani. Hakuwahi . . . alienda jangwani akiwa na umri wa miaka tisa. Hangaliweza kusoma jina lake, hata kama lingalikuwa katika herufi ukubwa wa behewa. Mbona, mbona yeye alitenda hayo? Yeye alikuwa nabii. Kama yeye angalizoezwa katika elimu ya baba yake, huenda ikawa angalikuwa Mfarisayo ama Msadukayo, ama moja ya makundi yao. Bali yeye alikuwa na kazi muhimu, hiyo ilikuwa kumtangaza yule Masihi. Sababu gani? Mungu alitimiza Neno Lake, kisha akalithibitisha. “Sauti ya mtu aliaye toka seminari, ‘Tazama, nina digrii ya juu sana’? Hayo—hayo huenda yakawa katika Twakimu ya Maulidi ya Bibi Kizee, bali si katika Neno la Mungu. Yeye alisema, “Sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito Yake!’” Je, yeye alikuwa akitengeneza njia ya Neno wakati huo, Neno lipate kuthibitishwa? Haleluya!

¹³⁹ Je, hamwoni, katika mifano? Na tukomee hapa kwa dakika moja. Katika siku za mwisho, sharti kuwepo mahali palipotayarishwa kwa Neno kudhihirishwa, nasi sasa tunaishi kwa ushuhuda wa ile Nchi mpya, amina, Mwana wa Adamu.

¹⁴⁰ Agizo la Yohana, bila elimu, bila cho chote kile, yeye alikaa jangwani. Mahubiri yake yalikuwa katika mifano. “Shoka limevekwa kwenye shina la mti,” hayo ndiyo aliyooona. Alikata kwa shoka, akatengeneza banda lake, akakoka moto kuchoma kuni zake. “Lo, enyi uzao wa nyoka,” hao ndio aliowaona. Kitu kiovu sana nyikani, kweke, kichakani, kilikuwa nyoka. Kasema, “Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kukimbia ghadhabu itakayokuja? Msiwaze mkisema, ‘Tuna *hiki*, nasi ni wa *hiki*, nasi tu wa *kile*,’ Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu Watoto. Shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti, na kila mti usiozaa matunda mazuri. . .”

Yeye anafanyaje jangwani wakati hauwezi. . . kumletea nzige na kadhalika, yeye huukata na kuuchoma. Mnaona? “Yeye ataikusanya ngano ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.” Mtu kama huyo, asiye hata na joho lake la kikasisi, wala naivera yake ya kuhani. Mnaona? Yeye anakuja huku amejifungia kipande cha ngozi ya kondoo, mwenye kipande cha ngozi iliyoikatwa kutoka mgongo wa ngamia, amejifungia, akatoka akaja pale huku amejaa masharubu na msitu wa nywele kama hivyo, kasema, “Shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti.” Yeye alikuja, kishujaa. Kwa nini? Ilikuwa ni Neno la Mungu likithibitishwa, “Mungu aweza katika mawe haya!” Mungu aliliahidi, “Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele Zangu.” Si la kidini au si thibitisho la kisayansi ama la kidini sana, bali Neno la Mungu ni thibitisho. Mungu alikuwa akitimiza Neno Lake, mnaona. Si mwanachuoni kamwe, bali nabii, aliyetumwa katika Jina la Bwana. Yeye alifanya hilo, kwa nini? Kuthibitisha Neno Lake.

¹⁴¹ Sasa, hao makuhani walisema, “Sasa, tunajua yuaja mtu mmoja katika siku za mwisho, kwa hivyo tutamwelimisha kila mvulana tuliye naye, tujitayarishe kwa ajili yake. Kila mmoja wenu enyi wavulana hana budi, kupata elimu ya chuoni. Hamna budi kuja humu. Hapana shaka atakuwa katika ule ukoo, atazaliwa katika ukoo wa Walawi, kwa kuwa humo ndimo unamotoka ukuhani.” Bali Yeye hakuwa kuhani, alikuwa nabii! Na hilo ni chaguo la Mungu. Si lazima atoke katika dhehebu fulani au ukoo fulani. Ni uchaguzi wa Mungu, kwa kuchagua tangu awali, kujua hapo awali. Yeye huja kwa uchaguzi wa Mungu. Kwa hivyo hawangemwamini, kwa maana Yeye hakuja kwa njia waliyomtengenezea, walifikiria alikuwa yuaja. Hayo yangeweza kutendeka tena, mnajua, kwa kwaida hutendeka. Lakini tunaona ya kwamba yeye alikuja jinsi Mungu alivyokusudia, kuthibitisha Neno Lake.

¹⁴² Tazama, Yeye alimfanya bikira achukue mimba, kuthibitisha Neno Lake. Isaya 9:6, nasi twaona ya kwamba, “Maana kwa ajili yetu mtoto mwanamume amezaliwa, tumepewa mtoto.” Sasa, twaona ya kwamba aliisha sema kwamba bikira angechukua mimba. Naye Mungu akamfanya bikira kuchukua mimba. Nini? Kuthibitisha Neno Lake. Sasa, sikizeni kwa dakika chache, tutafunga. Yeye alimfanya bikira kuchukua mimba, kuthibitisha Neno Lake. Hilo lilikuwa bila shaka. . . Iliduwaza wanasayansi wote. [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] . . . kwenda.

¹⁴³ Mnafahamu hiyo, sivyo? Mnaona, dunia yote imelaaniwa, dunia nzima imelaaniwa, kwa sababu ya dhambi ya Adamu. Bali wakati hii mbegu ndogo. . . Naam, mwanamke hana mbegu. Yeye ana shamba ambamo hukaa ile mbegu, si mbegu, sababu hamna yai, yai halina budi. . . ile mbegu haina budi kuwa na uhai ndani yake. Kama haina, ni kitu cha kawaida tu, hamna uhai mle. Kwa hiyo ile mbegu imo ndani ya mwanamume. Hiyo ndiyo sababu

ule uzao wa nyoka ulibidi uwe katika mwanamke, mnaona, kwa sababu haukuwa mzao wa Mungu. Tunajua hilo. Endeeleni, ngojeni mpaka mtakapokipata kitabu hiki mkakisome, ndiposa mta—mtaona, ama kuwaonyesha tu kwa Maandiko, kulifunua jambo hilo lote tu kama ubatizo wa maji katika Jina Lake, mwone jinsi ulivyo. Mungu hawezi kukosea kamwe, Yeye kila mara yu sahihi. Hata kama huwezi kulielewa, liamini tu. Ni Kweli kabisa.

¹⁴⁴ Na sasa tunaona ya kwamba Yeye—Yeye alisema hili, alifanya hili litendeke. Sasa, wakati mbegu hii ndogo, bila mwanamume, ilipoingia katika yai dogo alilokuwa ameliumba, basi mbegu hiyo ndogo, hiyo chembechembe hai ndogo huingia katika lile yai, na huo mkia ndogo hujongea mbele hapa na kuanza kukua kuwa chembechembe moja baada ya nyingine, ikiishi kwa uhai wa mama, mwili wake, na mle ndani yeye anailisha kwa damu yake. Nasi tunaona, basi, yeye huilisha. Si damu yake, ni damu ya mama. La, haina hata chembe moja hai ya damu ya mama yake. Lakini inalishwa na mama kwa vitu vyenye vitamini, bali si damu yake. Yote imeshikamanishwa kwa kundi la damu yake, kuikinga isipate vishindo na vitu kama hivyo, na maji, bali haina hata chembe moja ya damu ya mamaye. Maana huenda akawa yuafa kwa ugonjwa wa TB, wala akizaa mtoto; yeye hawezi kuurithi, kwa sababu viini vya TB, huja kupitia kwa damu. Lakini, mnaona, yeye anaweza—anaweza. . . Kifua kikuu hakirithiwi; unyonge hurithiwa, bali si TB, kwa maana hakina budi kupata pumzi ya mama na kupata kiini, mwaona, kabla hajaipata. Mtoto ni huru kabisa anapozaliwa, kwa sababu si sehemu ya damu ya mama.

¹⁴⁵ Sasa, tunaona ya kwamba Mungu aliingia katika hii chembechembe ndogo, mnaona, naye akaanza kufanyiza chembechembe, akiishi kwa vitamini za mama Yake na kadhalika, kama yeye naye. Ndipo alipokua kutosha kula, akaanza kula. Na hicho ni nini? Ni—ni mavumbi ya ardhi, ambapo ulimotoka na uhai wa mmea na uhai wa mnyama na uhai na kadhalika, naye alipoanza kula samaki na mkate na vinginevyo, zile chembechembe zikaanza kukua. Ndiposa alipokuwa mkubwa kabisa katika umri wa miaka thelathini, alibatizwa kwa kumtii Yohana hapa, au Mungu, katika maji, kisha akaondoka. Halafu nini ilitendeka? Yule Hua, aliyekuwa Mungu, akishuka kutoka Mbinguni, na sauti iliyosema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake.” Yeye alikuja kufanya nini? Kukomboha sehemu hiyo ya dunia. Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Kwa sababu, Mungu si kiumbe, Yeye huwa kiumbe tu katika Kristo, kwa sababu Mungu ni wa Milele na ni Roho, na Roho haumbwi. Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu, naye Mungu akaukomboa mwili huo. Unaona, Yeye aliposhuka, “Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa Naye.”

¹⁴⁶ Kwa hivyo Yeye, Mungu, alishuka chini baada ya kupitia haya, na sasa kila mwana, ambaye hula na amezaliwa kwa kujuana kimwili kwa kawaida, jinsi alivyokuja; ndipo inapofikia mahali ambapo huna budi kupitia katika ubatizo wa maji, halafu ubatizo wa Roho Mtakatifu, basi Roho Mtakatifu hushuka kwa ubatizo wa moto na kudai kiumbe hiki, jinsi alivyomfanya Yeye. Roho Mtakatifu na Mungu ni Roho yule yule, mnaona, hushuka na kudai mwili huu kwa ajili ya afufuo. Naye alifufuliwa kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, “Wale wote alionipa Baba watanija, hamna hata mmoja atakayepotea.” Nitamfufua katika siku ya mwisho. Hamna hata unywele mmoja wa kichwa chao utaangamia.” *Huo* ndio mwanzo wa kuumba kwa Mungu. *Huku* ni kuendelezwa kwa kuumba kwa Mungu. *Kisha* dunia nzima haina budi kupata ubatizo. Ndiposa Roho Mtakatifu atashuka katika mji fulani akakae juu ya nchi, kisha maskani ya Mungu yatakuwa pamoja na wanadamu, na kuishi pamoja nao, Mungu akiisha hapa duniani. Huu ndio mpango wote wa ukombozi, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama ilivyokuwa wakati huo.

¹⁴⁷ Sasa tazama, Yeye akimfanya huyu bikira kuchukua mimba, na ni kwa njia hii alimzaa Mwana bila kumjua mwanamume. Hili limeikwaza sayansi katika nyakati zote. Lingali linafanya hivyo. Wao huenda walimcheka Isaya aliponena na kusema huyu bikira angechukua mimba, “Naam, hilo lingewezekanaje?”

¹⁴⁸ Nawazia, Isaya, hiyo fadhaa, alipomsikia Mungu akisema, “Nitawapa ishara kuu, nitawapa ishara ya milele, bikira atachukua mimba.” Naam, yeye aliheshimiwa miongoni mwa watu, watu wake, nabii, aliyethibitishwa na Mungu. Sasa, yeye alipojitokeza mbele ya madaktari na kadhalika, na tamshi hili, “Bikira atachukua mimba.” Waona, haijapata kutendeka, tangu wakati ulipoanza, inarudi kule nyuma kabisa ambapo Mungu alimuumba mtu Wake wa kwanza. Bali hapa, sasa, kwamba, mwanamke aliye humu duniani atachukua mimba. Wazia hilo kwa busara, vipi kama huyo nabii alishikwa na fadhaa? Bali alijua ya kwamba Mungu atatimiza Neno Lake, angelithibitisha. Nakisia, kila jamaa ya Kiebrania ilimtarisha binti yao mdogo kwa kumpata huyu mtoto mchanga, mnaona, wakamnulia viatu na buti ama cho chote kile wanachovalia, na vitundu, na kujitayarisha kwa ajili ya—ya kuja kwa mtoto. Vizazi kadhaa vikapita, bali Mungu akathibitisha Neno Lake! Bikira kweli akachukua mimba, akamzaa mtoto mchanga, akathibitisha ya kwamba Neno la nabii Wake lilikuwa Kweli. Yeye daima huwapigania.

¹⁴⁹ Huyu Mwana wa bikira alikuwa Neno lililodhihirishwa. Sasa, Yohana Mt. 1, ukitaka kusoma hayo Yohana Mt. 1, huyu nabii, pia. Bali huyu Mwana wa bikira alikuwa Neno lililodhihirishwa, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Sasa, dunia yote ni uumbaji wa Mungu, bali imepotea. Mnaona? Kisha

anaikomboa dunia hii. Nawe ni sehemu ya dunia hii, naye anakukomboa vile vile anavyoikomboa dunia nzima. Unaona? Sasa, huyu Mwana wa bikira alikuwa Neno lililodhihirishwa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu, Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.”

¹⁵⁰ Shetani alijaribu kila hila kumfanya alipuuze hili. Shetani alijaribu kila alichoweza ku kumfanya alipuuze, akajaribu kumfanya autwae ule Ufalme bila mateso, akajaribu kumfanya autwae bila ukombozi (na huku ulikuwa ndio mpango wa Mungu katika Bustani ya Edeni alipomuua mwana-kondoo, ya kwamba angaliweza kuutwaa kwa damu pekee), hata akamwahidia falme zote za ulimwengu kama angalizitwaa. Wazia tu hiyo ni ahadi jinsi gani!

¹⁵¹ Hamtambui, marafiki zangu wapendwa na wa thamani katika dakika hii, kwamba Shetani amekupa ahadi ya... yeye atakufanya mmoja wa wahudumu bora sana katika hilo shirika. Atakupa kiti cha mbele katika kila kanisa na kukufanya shemasi. Atafanya cho chote kile, mradi tu utaenda mbali na hili Neno.

¹⁵² Sasa tazama, anafanya kila... ampe Yeye ulimwengu mzima na falme zote, Yeye angezitwaa. Yeye alikuwa akijaribu kumfanya avunje hilo Neno, kwa kuwa alijua alikuwa naye papo hapo kama angaliweza. Alimfanya Musa kulivunja, alimfanya hawa kulivunja, bali alimwendea mtu asiyemweza wakati huu. Kwa nini? Yeye alikuwa Neno, na hakujua hivyo. Yeye alikuwa hilo Neno, Yeye Binafsi.

¹⁵³ Naweza kumwona. Tunataka kuona mfano wake kama picha ya mtoto. Naweza kuona hayo mabawa meusi ya kale yakivuma dhidi ya Hawa, na kusema, “Naam, hebu nikwambie, ni nzuri. Ungelijaribu.”

“Lakini Mungu alisema tukifanya hivyo, tutakufa.”

¹⁵⁴ “Lo, vema, bila shaka hutakufa. Unaona? Lo, upuzi huo. Hilo ni wazo la kijinga. Usiliamini.” Bali Mungu alisema hivyo! Mungu alilithibitisha kuwa kweli. Naye anaithibitisha sasa, watu wanakufa dakika hii. Yuangali anaithibitisha kuwa ni kweli.

¹⁵⁵ Tazama, naye alipomtokea Musa, akasema, “Musa, unajua wewe ni mwepesi wa hasira, una hasira sana. Tazama yale hilo kundi la wahaini lilivyotenda, waona? Mbona usishuke uende hapa chini ukawakemee vilivyo.” Naye akafanya hivyo.

¹⁵⁶ Bali alipogonga hizi nyuzi za umeme za kipimo cha nguvu kipatacho elfu kumi, zilichoma nyoya zake alipokabiliana Naye. Akasema, “Lo, sikiza,” kasema, “nitakupa falme zote.”

“Imeandikwa!” Mnaona? “Imeandikwa!”

157 Akasema sasa, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu.” Mnaona, yeye kila mara alilitilia shaka. Bado yungali anawafundisha wengine kulitilia shaka. Alimfundisha Hawa kulishuku, akamfundisha Musa, kawafundisha hao wote kujaribu kulishuku.

158 Yeye anakufundisha kujaribu kulitilia shaka. Nanyi mnaoketi papa hapa sasa, mkitaka niyataje majina yenu, imekuwa, Shetani amejaribu kwa muda mrefu kuwafanya mnishuku. Msifanye hivyo. Dada, ukifanya hivyo, vema, wewe . . . ama, si mimi, bali kutilia shaka tu. Amini tu hili Neno. Si lazima uniamini mimi, bali uliamini Hili. Mnaona? Nikisema Neno hili, si langu, ni Lake. Mnaona? Neno langu ni tofauti, bali Hili ni Neno Lake. Mnaona? Tazama sasa, tazama, sitaki kuingilia hayo hivi sasa.

159 La, aliahidi Maneno Yake yote, ni ya kweli kabisa. Yeye aliyathibitisha. Aliyathibitisha, kwa maana alithibitisha kuwa Yeye alikuwa Neno lililo kweli. “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

160 Naam, je, yeye huishije? “Kwa, vema, ukitaka kuchukua baadhi ya Neno la Mungu, ataishi?” Sasa, hivyo sivyo alivyosema. Uliwahi kutambua “k-i-l. . . kila Neno”? Yeye anaishije? “Lo, yeye huila humo?” La, yeye anakufa upesi, huo ni mwili. “Vema, yeye, lo, yeye ni mfuasi wa kanisa, yeye anaamini kila kitu ila *Hilo*?” Yuangali amekufa. Mnafahamu? “Yeye aweza kuishi tu kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha kuhani mkuu, askofu, kardinali, mchungaji?” Mungu! Kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu. Tunajuaje ni Neno la Mungu? Yeye husema hivyo, kisha akalithibitisha. Yeye hulithibitisha Neno Lake. Tazama basi, kama hivyo ni kweli, maungano yako hayatakuifanya upate kuishi. Ufuasi wako wa kanisa hautakufanya uishi. Tazama, kwa Neno Lake pekee, si tu neno moja lililowekwa mahali pasipo pake. Hamna Neno ambalo . . . neno moja liliangamiza jamii ya kibinadamu. Katika Biblia, katika Ufunuo 22, neno moja lingali litaangamiza kitu hicho chote, jina lake litaondolewa kutoka Kitabu cha Uzima. “Mtu ye yote atakayeongeza neno moja, au aondoe Neno moja.” Si neno moja! Si . . . la, namaanisha, si—si maneno mawili, neno moja tu! Si fungu moja la maneno; neno moja! Neno moja! Lo, enyi watu mnafahamu?

161 Sasa, siongei hasa na wasikizi hawa. Haya yananaswa, mnaona, na yanaenda ulimwenguni kote. Je, mnafahamu, watu wa ulimwengu, ya kwamba Neno moja, Neno moja, si fungu moja la maneno, si aya moja, Neno moja, hilo tu ndilo Hawa alikosa kuamini. Ikasababisha . . . Mungu akalithibitisha. “Lakini basi, mkitii kila Neno, mtaishi.” Wao walishuku Neno moja, likasababisha mauti kwa jamii ya binadamu. Lakini mtu hataishi kwa mkate tu, kwa ajili ya nguvu zake za kimwili, bali kwa kila Neno, kila Neno jinsi lilivyoandikwa. Biblia inasema,

“Si ya kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani.” Hamna mtu aliye nayo po pote, ye yote kamwe, kujaribu cho chote kufasiri Neno la Mungu. Mungu hujifasiria Mwenyewe.

¹⁶² Alipoahidi, alisema, “Iwe nuru,” ikawa nuru. Akasema, “Bikira atachukua mimba,” akafanya hivyo. Mnaona, lo lote asemalo Mungu, Mungu hulithibitisha.

¹⁶³ Haidhuru utajaribu vipi kuwazia kuwa ufufuo wa mwili haungewezekana, na watu hao wako kule nyuma, wakiwa mavumbi ya ardhi, na tayari wamepita mavumbi sasa, wamekuwa madawa na gesi ambayo miili yao ilifanyiwa. Nafsi zao zingali hai. Mungu alisema, “Nitaifufua.” Ayubu alisema, “Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi na mabuu ya ngozini, lakini katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Mnaona, haidhuru, kila Neno halina budi kutiwa, na mtu ataishi kwa Neno hilo. Yeye alimfufua mtu kutoka kwa wafu, baada ya kufa kwa siku nne, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ufufuo na Uzima. Mtu akiisha kufa kwa siku nne na huku ananuka, pua lake lilikuwa limebonyea katika siku nne. Hiyo ni kweli. Kitu cha kwanza kubonyea, kwa mwanadamu, ni pua linabonyea katika mwili wa maiti, linakuwa jepesi na kubonyea ndani. Kisha ngozi, wale mabuu, wewe. . . Hata wakikuwika katika sanduku la kuzikia maiti lililozibwa kabisa, cho chote kile, hata hivyo mabuu ya ngozini si lazima yatoke ardhini, yamo ndani yako. Ulitambua ya kwamba Ayubu alisema, “Hata kama mabuu ya mwili wa—wangu yakiniharibu.” Si mabuu ya ardhini, hakungekuwika na yo yote. Hao mabuu yamo ndani yako, yakiwa tayari kukuangamiza, mauti yakitenda kazi katika mwili wako uharibikao. Ulipompata Kristo, basi Uzima unatenda kazi katika mwili wako uharibikao, kukufufua tena. Unaona? Yeye alimfufua mtu mmoja katika wafu, baada ya kufa kwa siku nne, “ananuka,” kuthibitisha Yeye aliposema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima.” Sasa, nani angalisema hivyo ila Mungu, mnaona, “Mimi ndimi ufufuo, na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi,” Je, mnaamimi hayo? Naye alimfufua huyo mtu, kuthibitisha ya kwamba Neno Lake lilikuwa sahihi. Vema!

¹⁶⁴ Tazama, yeye alikuwa Neno. Waebrania 4:12, ukitaka kuandika hili. Waebrania 4:12, ilisema, “Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, linapambanua mawazo na makusudi ya moyo.” Sivo? “Kupambanua.” Kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Neno, Yeye alifanyaje? Petro alimjia, jina lake lilikuwa Simoni. Naye akaja kwa Yesu, na akasema. . . akaketi chini kule, na Yesu, mara alipoingia, akasema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Hana elimu, hana digrii yo yote, hakuwa na cho chote ila alikuwa tu mvuvi wa kawaida, hana elimu, Biblia ilisema ya kwamba alikuwa “asiye na elimu, wala maarifa,” bali akawa askofu wa kanisa la—la Yerusalemu. Kwa nini? Kwa nini? Yesu alimwambia Yeye alikuwa nani, jina lake lilikuwa nani, na jina la baba yake. Naye alijua ya

kwamba hilo lilikuwa Neno, kwa maana Biblia ilisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii aliye kama Mimi,” na hapana budi huyo alikuwa nabii, na hapakuwepo na manabii walioahidiwa baada ya Malaki hadi Masihi, miaka mia nne bila nabii. Na hapa alikuwepo mtu amesimama pale, akihakikisha, ama akilithibitisha Neno Lake, kwa huyu mtu aliyechaguliwa Uzima tangu awali, kasema, “Jina lako ni Simoni, tangu sasa . . . U mwana wa Yona, tangu sasa utaitwa ‘Petro.’ Wazia hilo! Je, Yeye alilithibitisha kwa nani? Mbona hakulithibitisha Neno hilo kwa . . . Mbona hakulithibitisha hilo Neno kwa Kaiyafa? Yeye alikuwa Mungu, alijua ya kwamba Kaiyafa hangaliliamini. Bali mtu huyu alichaguliwa Uzima, alijua hivyo papo hapo.

¹⁶⁵ Siku moja akisimama kati yao, ambapo mtu mwingine siku chache baadaye alienda akampata rafiki yake karibu na mlima, yapata maili kumi na tano kutoka mahali ambapo wao walikuwa wanahubiri, akamrudisha siku iliyofuata. Alikuwa amesimama pale miongoni mwao, kisha akaja mahali alipokuwa Yesu. Yesu akatizama pande zote, Yeye alikuwa Mungu, mwaona, alikuwa na upambanuzi. Hilo lilidhibitisha hilo, mnaona, akilifanya Neno Lake kweli, akalithibitisha Neno Lake.

Naam, wengine wao husema, “Mwajua, huyo mtu ni Neno.”

¹⁶⁶ Upuzi,” hao makuhani wakasema, “mtu huyo siye. La. Hilo si Neno.”

¹⁶⁷ Kasema, “Mnajua Maandiko yasemavyo, ‘Bwana Mungu wetu atatuondokeshea nabii kama alivyo Musa.’ Na huyo ndiye. Msikizeni.”

¹⁶⁸ Vema, akasema, “Wewe ni, mtazame, Mwisraeli, ndani yake hamna hila.”

Mtu huyu akasema, “Rabi, ulinijua lini?”

¹⁶⁹ Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.” Yeye alijua yule angeliamini.

¹⁷⁰ Akasema, “Rabi, Wewe u Mwana wa Mungu. Wewe ni Neno.” Yesu alithibitisha alikuwa Neno, kwa Neno.

¹⁷¹ Tazama maskini mwanamke kisimani. Alikuwa akimtizimia Masihi. Hakuhusikana na makundi yao makubwa na madhehebu, na kadhalika, waliyokuwa nayo siku hizo. Yeye alikuwa akilitazamia Neno. Kwa hivyo Mtu mmoja, wakati mmoja, akiketi kule, Mtu wa kawaida, akiketi kandoni mwanja, alisema—alisema, “Mama, niletee maji.”

¹⁷² Akasema, “Sasa, ngoja kidogo, Yeye labda anajaribu kunichezea,” huenda aliwazia moyoni mwake, maana yeye alikuwa ametiwa alama ya mwanamke mwenye sifa mbaya. Kasema “Mbona, naam, mbona unaniuliza swali kama hilo? Tuna ubaguzi humu. Wewe ni ni ni . . . Wewe ni Myahudi, sisi ni Wasamaria, si . . . si desturi, si halali Kwako kuniuliza hivyo.” Mnaona?

173 Akasema, “Mama, kama ungalijua ni nani unayeongea naye, ungaliniomba Mimi maji.”

174 Akasema, “Wewe, nikuombe maji? Hata sioni ndoo wala kamba. Ungenipaje maji yo yote toka humu kisimani?”

Yeye akasema, “Hicho sicho kisima nilichokuwa nikinena habari zake.” Mnaona?

175 Na baada ya muda mfupi, akasema, “Huyu ni mgeni.” Kwa hivyo akaanza kuuvuta ule mtungi wa maji, akiuvuta.

176 Kasema, “Vema, maji ninayotoa yangekuwa chemchemi za maji, bubujiko, yakibubujikia Uzima wa Milele, na katika nafsi yako.”

177 “Vema,” Akasema, “sasa, ngoja kidogo, na nafahamu, Wewe ni Myahudi.” Kasema, “Sasa, ninyi Wayahudi,” kasema, “Unataka kuniambia ya kwamba Wewe ni mkuu kuliko baba yetu, Yakobo, aliyekichimba kisima hiki?” Yeye alikuwa Mungu wa Yakobo. Mnaona? Kasema, “Unataka kusema Wewe ni mkuu kuliko—kuliko Yakobo, aliyekichimba kisima hiki?” Mtu wa kawaida, mnaona, alionekana hivyo. Hicho tu ndicho mlichooona, mtu wa kawaida. Kasema, “Unasema wewe ni mkuu kuliko baba yetu, Yakobo, aliyekichimba hiki kisima, naye mwenyewe akanywa maji yake, na ng’ombe zake pia? Vema, tunabarikiwa kwa kunywa kisima hiki ambacho huyo nabii alichimba.”

Akasema, “A-haa,” akasema.

“Nasi tuabudu katika mlima huu. Nanyi mnasema ‘huko Yerusalemu.’”

178 Akasema, “Wakovu ni wa Wayahudi, mama, tunajua tunayonena.” Akasema, “Mnaambudu msichojua.” Myahudi anapaswa kujua Neno, mnaona, jinsi lilivyopaswa kuwa. Lakini, unaona, alikuwa akiangalia sasa. Kwa nini. Anaenda ku... atafanyaje? Kuthibitisha Neno Lake. Unaona? Tazama, mwanamke alisema... Yeye akasema, “Basi, nenda kamwite mumeo mje hapa.”

Naye akasema, “Sina mume ye yote.”

179 “Naam,” akasema, “umesema kweli, waona, kwa maana umekuwa na watano na uliye naye sio mume wako.” Waona? Tazama! Jambo fulani likatendeka, waona, kitu fulani kikapata Uzima. Sasa, kama haungalikuwa mle ndani tangu mwanzo, kama yeye hakuwa na—na uwakilisho tangu awali, haungalishikilia.

180 Pale walisimama makuhani, wakasema, “Mtu huyu ni Beelizebuli.” Mnaona, hawana uwakilishi.

181 *Uzima wa Milele*, “ulikuweko kila mara.” Unaona, una Uzima wa Milele, kuna aina moja tu yake, hiyo ni Mungu. Wewe ni Wazo Lake Yeye alikuwazia na akakujua kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu, katika nia Yake. Unaona?

182 Akatazama huku na huko. Tazama jinsi—jinsi alivyokuwa katika dhambi. Lakini, waona, Yeye hange—hangempata huyo kuhani, kwa maana huyo kuhani alikuwa mwanachuoni aliyeelimika, mthiolojia katika Neno, bali, bila uwakilishi Mbinguni, unaona, hakuwa kamwe katika mawazo ya Mungu. Bali mwanamke huyu alikuwa. Yeye alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.” Hayo ndiyo tu aliyotaka yeye aone. Mnaona? Kasema, “Tunaamini ya kwamba ndivyo ulivyo, naamini ya kwamba Wawe ni nabii. Sasa, tunajua. Hutufahamu kuhusu nabii sasa, kwa sababu tumechelewa sana, tunajua ya kwamba kuna Masihi anayekuja. Na huyu Masihi ajapo, Yeye atakuwa Neno. Unaona, Yeye atajua siri za moyo, Yeye atafanya jambo lile lile ambalo—ambalo ulitenda kule.” Kasema, “Huna budi kuwa mmoja wa manabii wake, kumtangulia ama cho chote kile.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

183 Angefanya nini? Alikuwa akithibitisha Neno Lake, akithibitisha mahali pake, akithibitisha kile alichokuwa. Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake. Na Mungu ni Neno. Vema. Alituliza upepo na mawimbi, kuuthibitisha unabii wa Isaya, “Ataitwa Jina Lake ‘Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele.’” Mnaona? Yeye pia aliizidisha mikate na samaki, huyu Mwana aliyezaliwa kibikira. Ilikuwa nini? Kulithibitisha Neno. Maandiko yote hayana budi kutimizwa. Yeye alilithibitisha Neno, kwa kusema alikuwa Yehova aliyedhihirishwa. Alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Mungu katika uumbaji, Mungu pamoja na sehemu ndogo ya uumbaji hapa ambapo Mungu alikuwa akiishi kwa nafsi Yake, Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu, “Kutoka Kwake wanazaliwa wana wengi.” Tazama, Yeye pia alizidisha samaki. Yeye ni Neno na thibitisho la Neno.

184 Sasa sikizeni kwa makini, tunapoelekea kumalizia. Siku hiyo, ambayo nilisoma habari zake kakika dakika chache zilizopita, basi, Yeye alipofika katika nyumba ya Yairo. Akaingia, alipofika kule. Sasa, kumbukeni, Yairo alikuwa ku—kuhani, mwamini mwenye kukwamia mpakani. Yeye alitaka kumwamini Yesu, lakini alichukia kuachilia kanisa lake, kwa sababu wao walikuwa wamesema, “Mtu ye yote anayemwamini atafukuzwa kanisani.” Sasa, sikizeni kwa makini sasa, tunapomalizia, nisikizeni kwa makini sana. Tazameni hili. Naamini ya kwamba Yesu alijua hayo alipovuka bahari, kwa kuwa Yeye alijua mambo yote. Naye alipovuka bahari, akasimama pale, kisha akashuka akija maskini kuhani huyu. Msichana wake akawa mgonjwa sana, madaktari waliisha mkatia tamaa, “yeye ni mgonjwa mahututi.” Naam, wakati wa matendo ukafika.

185 Labda hilo ni kwenu asubuhi ya leo, wakati umefika kwenu mtende. Mnaona? Labda u mgonjwa sana. Labda umeshawishika

ya kwamba umekosea. Huenda ikawa. Mungu huhimiza jambo, wakati wa matendo huja.

¹⁸⁶ Sasa kwa makini. Basi akaja, hakujali waliyosema hao wengine, kule hadharani, akaja akaanguka miguuni pa Yesu. Ni hatua ya jinsi gani kwa—kwa mwanachuoni mwenye elimu, kumjia Mtu ambaye hatuna habari ya kwamba alienda shuleni kamwe. Jinsi mtu mmoja alivyokuja, alidhaniwa kuwa katika theolojia yote, akamjia Mtu aliyedhaniwa kuwa “mpotovu, mshenzi, mwenda wazimu, amerukwa akili, hata hana akili timamu.” Kunradhi hili tamshi, bali “Yeye ni mwenye kisirani wa kwaida mambao,” kila mtu alimfikiria hivyo. Kama vile tungalisema leo, katika msemu wa barabarani, “Nati!” Kama nilivyohubiri hivi majuzi juu ya nati na skurubu, mwajua. Mnaona, hivyo ndivyo alivyokuwa kwa umma, mtu tu wa kawaida. . . kasema, “Naam, umerukwa na akili! Una kichaa! Wewe ni mwenda wazimu!” Basi, hapa alikuwepo mtu aliyekuwa na elimu yote, akimjia Mtu aliyedhaniwa ana wazimu. Alilazimishwa kumjia.

¹⁸⁷ Mtazame sasa. Itaumiza kidogo, bali itakufaidi. Unaona, wakati mwingine mshtuo hukuamsha.

¹⁸⁸ Tazama, Yeye alikuja na akaingia ndani kando ya huyu msichana mdogo, maiti, aliyekufa labda masaa kadha hapo kabla, nao walikuwa tayari wamemlaza chini, na kumnyunyizia mafuta ya kuzuia maiti yasioze na wakayanyunyizia machela. Hivyo ndivyo walivyofanya siku hizo, wakawachukua wakawaingiza shimoni, katika ubao. Alilazwa katika machela, amezungushiwa maua.

¹⁸⁹ Kisha, lo, maskini huyo mchungaji mwema, Yairo mdogodogo, kila mtu alimpenda. Kwa sababu, unaona, naweza kuthibitisha hilo, kwa sababu moyoni mwake, alimwamini Yesu. Lakini ilikuwa vigumu kwake kukata kauli au, maana hangeletewa cheki kila Jumamosi ama kila Jumatatu asubuhi. Mwaona? Ilikuwa vigumu kwake ku—kujiamulia. Na jambo lingine, hao watu, ile sifa kubwa na nzuri aliyokuwa nayo kati ya watu, wao wangesema, “Mnajua, Yairo amekuwa mshupavu wa dini. Mnaona, alikwenda kule pamoja na huyo nabii wa uongo. Hivyo ndivyo alivyofanya hasa, ambapo hayo yote yanayodhaniwa kuwa ishara na kadhalika, huyo Nabii wa Galilaya, mwajua, Yesu wa Nazareti.”

¹⁹⁰ Hatuliamini sasa, laonekana kama kukufuru, lakini hivyo ndivyo ilivyokuwa wakati huo. Mnaona? “Na, siku moja, kama ilivyo sasa, itakuwa hivyo basi.” Mnaona, jambo lile lile!

¹⁹¹ Sasa tazama, yeye alikwenda kule. Na ilikuwa vigumu kwake kufanya hivyo, bali ulifikia wakati ilipomlazimu kufanya hivyo. Ilimbidi kufanya hivyo. Naye akaja hapa akampata Yesu, moja kwa moja mbele ya hao wote, akaanguka miguuni Pake,

akasema, “Bwana! Bwana!” Unajua hiyo ni nini? Utawala, umilkaji. Hiyo ni kweli.

¹⁹² Unaona, watu wengi sana wanataka Yesu awe Mwokozi wao, bali si Bwana wao. Angalia, *Bwana* ni “mtawala.” Naam. Unasema, “Yesu, niokoe na uache nikasimame papa hapa, na hili ni sawa, nami nitafanya shughuli zangu. Basi usiingilie mambo yangu. Bali waweza kuwa Mwokozi wangu, bali si Bwana wangu.” Yeye anataka kuwa Bwana, waona, kisha Yeye ni Mwokozi wako.

¹⁹³ Lakini sasa, yeye alisema, “Bwana, Mwokozi!” Unaona, mimi. . . msichana wangu mdogo, mtoto wangu wa pekee, yeye yuna umri wa miaka kumi na miwili, madaktari wamekwisha kumkatia tamaa.” Hapana shaka huenda kuhani alisema hivi, “Mwajua, wote wamezungumza kuhusu wewe kuwa mshupavu wa dini, lakini, wajua, Bwana, na—na—nakuamini. Naamini. Najua una upambanuzi. Na neno tu ninalotaka useme, ni, mwekelee tu mikono yako. Kisha uniambie la kufanya, nitalifanya.” Lo, unafikia mahali fulani!

Kasema, “Nitaenda. Nitaenda.” Na akashika njia akaenda.

¹⁹⁴ Akiisha kuondoka kwa masaa hadha, hapa yuaja mtu fulani mbio kama desturi zao zilivyokuwa wakati huo, jivu kichwani mwake, kasema, “Usimsumbue Mtu huyo, binti yako alikufa. Amekwisha kufa, tayari wamemtengeneza na kumlaza nje.”

¹⁹⁵ Lo, moyo wake mdogo! Yesu akageuka akamwangelia, akasema, “Lo! Lo! Lo!”

¹⁹⁶ Akasema, “Sikukuambia?” Sasa, alifanya nini hapo, alimwahidi Yairo. Sasa hana budi kuthibitisha hilo. Amina. “Nilikwambia. Amini tu nawe utauona utukufu wa Mungu.” Sasa, Yeye alijua alichokuwa akifanya. Alisema hatendi neno hata Baba amwonyeshe kwanza, Yohana Mt.—Yohana Mt. 5:19, “Natenda tu lile Baba analonionyesha Mimi,” kwa hivyo akamwonyesha yale yatakayotendeka.

¹⁹⁷ Kwa hivyo alipoingia nyumbani, akasimama pale kando ya umbo hilo dogo, lenye baridi na lililokauka, lilolazwa pale, liliugua kwa majuma kadha. Na maskini mwili wake uliokuwa kijivujivu, hamna chakula kilichokuwa kimeingia mwilini mwake, na homa na kadhalika, naye alikuwa—alikuwa tayari amekufa. Walikuwa wamenyunyizia manukato ya kuyazuia maiti yasioze na kadhalika. Naye akilala pale, wajua, juu ya machela na kadhalika, wakijitayarisha kumfunika na kumlaza kaburini, nao wakafanya sherehe zao za kumzungushia maua. Yesu akaja. Na kila mtu, “Lo, Jairo, msichana wako mdogo amekufa! Lo, baba Yairo, lo! Tunakusikitikia, na kila kitu.”

¹⁹⁸ Akasema, “Lo, tulieni, mnapiga kelele sana.” Akasema, “Mbona mnafanya ghasia hii yote humu?” Mnaona? “Ghasia hizi, mna. . . mna—mnafanya makelele na kulia. Huyu msichana hajafa. Amelala. Shhh.”

199 Ndipo wakafanyaje? Walipomsikia akisema ya kwamba hajafa, wakasema “wakamcheka sana.” Kwa maneno mengine, walimzomea. “Ewe! vipi Wewe! Vipii, wewe nabii wa uongo! Vipii wewe mdanganya watu! Huyu msichana amekufa. Daktari alisema amekufa. Tumeihifadhi maiti isioze, tumemlaza kule nje. Amelala pale, amekufa.” Wao wakisema, “Ha, ha, ha! Sasa, Yairo, umekuwa ukinena habari Zake, na sasa je?”

200 Mwajua aliyotenda? Alisema, “Nyote tokeni humu.” Kati ya kutokuamini kama huko, haiwezekani. Basi, mbona Yeye akasema hivyo? Alisema, “Yairo, ikiwa utaamini tu, utaona utukufu wa Mungu.” Basi hilo ni Neno Lake. Hana budi kuthibitisha hilo. Vema.

201 Kisha alipoingia katika nyumba amabamo watu wote walikuwa wakilia, Yeye alisema, “Analala.” Hiyo ilikuwa kinyume cha sayansi. Hilo lilikuwa kinyume cha busara. Alikuwa amekufa, amepakwa na madawa asioze.

202 Mara tu walipokufa, walitiwa madawa papo hapo, mara tu uhai ulipowatoka, waliwamwagia manukato na kadhalika kisha wakawavika sanda na kuwatoa nje. Mnaona, kuwazika, wao huwazika kama tu, vema, wakati mwingine hata hawakuwaarifu watu. Mnajua, Anania na Safira; waliisha mzika Anania, wakati Safira. . . Anania, Safira alipoingia, mwaona; waliisha mtoa nje wakamzika, mnaona. Wao tu, mara walipokufa, wangewamwagilia kitu hicho juu yao na kuwapeleka kule na kuwazika. Mnaona?

203 Kwa hivyo yeye alikuwa tayari kwenda kaburini, bali wao walitaka kumngojea baba apate kumwona kabla kawajamzika. Naye alipokuja, naye akiwa katika hali hiyo, basi akasema, “Yeye amelala usingizi mdogo tu.”

Vema, walisema, “Sasa Mtu huyo ni mwenda wazimu kweli kweli!”

204 Kwa hivyo sasa Yeye alifanyaje? Tayari alikwisha kusema kwamba alikuwa analala, ilimpasa kuthibitisha Neno Lake. Yeye hangalifanya hivyo mbele ya kundi hilo, kwa hivyo akasema, “Watoe nje wote.” Nami naweza kumwona akimgeukia Yairo na kusema, “Ungali unaamini?”

“Naam, Bwana.”

205 Wewe na mkeo njooni hapa. Petro, Yakobo na Yohana, nifuateni.” Wakaenda kule na akaita neno hili, *talitha kumi*, ambalo maana yake ni, “Msichana mdogo, inuka.” Naye akalithibitisha Neno Lake, alikuwa tu amelala. Sivyo? Alithibitisha hapa, Neno Lake lilikuwa kweli. A-ah, bila kujali kutokuamini kwao, Yeye bado alithibitisha Neno Lake kuwa kweli, kwa kumwamsha, kwa sababu alisema yeye alikuwa amelala. Alikuwa amelala.

206 Yeye atafanya vivyo hivyo siku moja, kwa kila mwamini wa kweli, kwa maana Neno Lake liliahidi kufanya hivyo. “Hao walio katika Kristo, Mungu atakuja pamoja nao.” Mnaona, “Hao walio katika Kristo.”

207 Huyu msichana mdogo wa Kiyahudi alifanyaje? Nilianza tu kuruka Andiko hili hapa, bali ni—nita—nitaliweka. Najua huenda ikawa kumechelewa kidogo, nasi tutafikia mstari wa maombi katika dakika chake. Huenda nisiwaone kwa juma lingine labda, bali hebu tungoje hapa kwa dakika moja. “Mtu hataishi kwa mkate tu.” Mnoana? Tazama, hebu niliingize hili ndani sasa, kuwaonyesheni. Mbona Yesu akamwamsha huyu mwanamwali Mwebrania? Kwa sababu alijua hakuwa maiti? Kuchaguliwa tangu awali. Jinsi tu alivyomtendea Lazaro. Mnaona? Labda kuna wasichana wengi waliokufa siku iyo hiyo, Yeye hakuwaambia kamwe neno. Alijua ya kwamba huyu alikuwa na Uzima wa Milele. Mnaona, Yeye hakuwaamsha hao wengine.

208 Tazama, alipotoka Yeriko, wao walisema, “Hapa, mtu huyu hapa!” Hapana shaka walisema, “Ati unawafufua wafu? Unaniambia unaweza kuwafufua wafu, tuna makaburi juu hapa, njoo uwaamshe.” Mnaona, Yeye hata hakuwajali kamwe. Waona, hakuwajali, kwa sababu alijua alikuwa Neno.

209 Tazama, alikuwa amelala tu. Alijua baba angekuja. Sasa, huyu msichana, mnaona, Yeye alijua ya kwamba, huyo mwanamwali mdogo wa Kiyahudi alikuwa tu amelala. Mnaona, mwe—mwenye haki hafi. Yesu alikuja kuwakomboa wenye haki. Na, *kukomboa*, maana yake ni “kurudishwa ulikokuwa kwanza.” Waona? Yeye hangaliwakomboa wasioamini, haidhuru walielimishwa vipi na walikuwa na digrii ngapi za udaktari. Hangaliweza kuwakomboa, kwa sababu hawangekomboleka, iliwapasa waende kwenye mwisho wao. Lakini, katika kujua Kwake tangu zamani, alijua kwamba Lazoro angetoka kaburini. Alijua pia huyu msichana alikuwa na Uzima wa Milele. Kwa hivyo hakuwa amekufa, alikuwa tu amelala. Na kazi yetu itakapokwisha duniani, kama hatutaishi hadi kuja Kwake, hatuwezi tukafa, tumelala tu. Yeye alithibitisha hilo hapa. Atalithibitisha tena. “Hata mabuu ya mwilini yakiuharibu mwili huu, hata hivyo nitafufuka katika mfano Wake.”

210 Yeye huthibitisha Neno Lake lote, Neno Lake lote. Wazia hilo tu, Neno *Lake* lote! Nawe ulikuwa Neno Lake. Yeye alikuwa Neno, nawe ulikuwa sehemu ya Neno Lake. Na, hiyo ndiyo sababu umetumwa hapa kuhakikisha mahali pako maishani. Si—si—sidhani mmelipata hilo. Mnaona, Yeye ni Neno. Sasa mmefahamu?

211 Alikuwa miguuni, katika Luther; pajani, katika Wesley; mabegani, katika Pentekoste. Mnaona ninalomaanisha? Yeye ni Kichwa. Una sehemu inayounganisha huo pamoja, wakati

huu tunaoshi sasa; si sehemu ya miguuni, si sehemu ya pajani, si sehemu ya mabegani, bali sehemu ya shingoni. Sivyo? Inaunganisha na kichwa. Hiyo ni sehemu ya mwili. Hao waliokufa katika Yesu Mungu atakuja pamoja nao. Parapanda ya Mungu Italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Sivyo? Unaona, unakuwa sehemu ya hilo Neno, unakuwa sehemu Yake. Nawe unachukua Jina Lake kuitambua, waona, unawekwa mle ndani ukiwa umebatizwa katika Jina Lake, Mwilini Mwake, “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili mmoja,” humu, mahali pale pale hasa. Yeye habadilishi njia Yake. Kama . . . Wangapi wanaamini lile kanisa la mwanzoni limo ndani Yake? Hebu tuone, wangapi wanaamini hayo? Wao walibatizwaje? Vema. Angalieni, Yeye ni Mungu asiyebadilika. Tulithibitisha hayo. Tungekaa hapa hata usiku wa manene usiku wa leo, tukithibitisha hayo, na tuzidi kuendelea na kuendelea. Mnaona, asiyebadilika! Mnaona? Wewe umo katika Yeye na u sehemu Yake, kwa maana ulikuwa sehemu ya kuwazia Kwake. Kabla kuwekwa misingi ya dunia, Yeye alikuwa!

²¹² Biblia ilisema ya kwamba yule Mnyama juu ya nchi . . . Huyu ni Mpinga Kristo wa kidhehebu akija duniani, akifanyika yule Mnyama wa Rumi, ambayo ilikuwa dhehebu la kwanza. Nalo hili Baraza la Makenisa Ulimwenguni linaunda ile sanamu ya Mnyama, sawasawa kabisa tulivyoyaandika kitabuni mle hivi majuzi. Tazama, linaunda hiyo, mnaona, huyu Mpinga Kristo. Nayo Biblia ilisema, “Wote ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo,” (lini, katika ufufuo?) “aliyechinjwa kabla ya misingi ya dunia” (Jina lako liliandikwa pale), huyu Mpinga Kristo atakudanganya.” Mathayo 24:24, inasema ya kwamba—ya kwamba “Yule Mpinga Kristo atafanana sana na kitu chenyewe katika siku za mwisho, ingewapoteza walio wateule, ama waliochaguliwa tangu awali . . .” Ni jambo lile lile, Mungu alikuteua ama kukuchagua tangu awali kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. “Wataipokea wote ambao majina yao hayakuchaguliwa tangu awali kwenye Kitabu cha Uzima.”

²¹³ Danieli alinena habari hiyo, jinsi wenye busara watakavyokuwa katika siku hiyo, na jinsi wasio na hekima, na kadhalika. Vema, mengi sana, lakini naendelea kwenda mbali sa—sana, saa inapita upesi sana kwangu. Tazama, angalia sasa, Yeye aliona baada . . . Sasa tazama yaliyotendeka hapa. “Wote aliowajua tangu zamani, hao akawaita. Na wale aliowaita, hao akawahesabia haki. Na wale wote aliowahesabia haki, hao akawatukuza.” Safari yako imekwisha, unaishia sehemu iliyo yako. Neema ni yale aliyokutendea Mungu. Matendo ni yale ufanyayo katika kushukuru.

²¹⁴ Akathibitisha kwa jambo lile lile Lake, ya kwamba Yeye alijua mambo yote, huyu Mtoto Mwanamume aliyezaliwa na

bikira. Alijua ambapo samaki walikuwa majini, ambapo Petro na wengineo walikuwa wametupa wavu wao mkubwa kila mahali na wasipate kitu. Hilo lilithibitisha Neno Lake. Sivyo? Yeye alijua mambo yote.

²¹⁵ Na alipokuwa tayari kulipa kodi Zake, ilionyesha ya kwamba Yeye ni anamiliki vitu vyote. Alijua mahali palipokuwa na samaki aliyekuwa na senti kutosha kabisa kinywani mwake kulipia. . . Mtu fulani alikuwa ameziangusha mle, kisha huyo samaki akazichukua. Naye akasema, “Petro, nenda ukatupe ndoano, mnaona, kisha umchukue huyo samaki ukatoe hizo fedha kinywani mwake. Kisha nenda kawatosheleze, kulipia kodi.” Loo, naam!

²¹⁶ Mbweha wana matundu na ndege wa angani wana viota, bali Yeye alikuwa na Neno, alikuwa Neno, na akalithibitisha kuwa kweli. Yeye kila mara hulithibitisha Neno Lake. Atafanya vivyo hivyo sasa, katika kila kizazi hutenda vivyo hivyo.

²¹⁷ Baada ya siku ya tatu, baada ya kufa Kwake, kuzikwa, siku ya tatu, akafufuka tena, kuthibitisha Neno Lake, kwa maana nabii alisema, “Sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiachia nafsi Yake kuzimu,” siku ya tatu kabla uharibifu haujaanza katika masaa sabini na mawili. Mnaona, kwa hivyo hazikumalizika siku tatu nzima, kwa sababu uharibifu huingia katika masaa sabini na mawili. Mnaona, kwa hiyo hakumaliza muda huo kwa kuwa nabii alisema, mnaona, nabii alisema, “Sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Yeye alithibitisha Neno Lake.

²¹⁸ Aliwaponya wagonjwa, viwete, kuthibitisha Neno Lake ambalo Isaya na manabii wale wengine walikuwa wamenena.

²¹⁹ Alimtuma Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste, kuthibitisha Neno Lake. Unataka kupata baadhi ya Maandiko haya sasa, Yoeli 2:28, Yeye alisema, “Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na watumishi Wangu wanaume na wanawake nitawamwagia Roho Yangu. Na vijana wenu wataona maono, wazee wenu wataota ndoto, na kadhalika.” Yeye alithibitisha hilo kwa kuimwaga! Pia alikuwa amesema kabla ya wakati huu, katika Luka 24:49, ukitaka kuandika, Yeye alisema, “Na tazama, nawaletrea juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini kaeni humu, mjini Yerusalemu hata mvikwa uwezo utokao Juu.” Ndilo hilo, Yeye alilitimiza, akamtuma Roho aendeleo kuthibitisha Neno Lake. Bali tazama alichosema. Je, alilitimiza? Vema

²²⁰ Marko 16, Yeye alisema, “Enedeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Umbali gani? Ulimwenguni mwote. Nani? Kila kiumbe. “Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yeye alisema katika Marko 4, akasema katika Yohana 14:12, pia alisema, “Yeye aniaminiye Mimi,” si ajifanyaye

kama kwamba anaamini, “bali yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Inachukua Roho yule yule aliyekuwa ndani Yake kufanya kazi zile zile. Kwa nini? Roho alikuwa akija kudhihirisha Neno lililoahidiwa katika siku za usoni. Mnaona, Yeye alifanya matayarisho, kwa kuwa alijua ya kwamba mambo haya yangetendeka.

²²¹ Sasa, baada ya miaka elfu moja mia tisa, huku nyakati za kanisa zimepita, na mambo yote aliyomtabiria Luther, Wesley, tumekwisha kuyafafanua na kuona zikichorwa, na mwezi ukashuka ukazichora, kisha Bwana akatuchorea ubaoni hapa, akazionyesha, kisha akashuka yeye Binafsi akaithibitisha kuwa kweli. Baada ya miaka elfu moja na mia tisa, nasi tuko katika mwisho wa wakati wa kanisa la Laodikia, Yeye aliahidi, katika Luka 17:30, ya kwamba Mwana wa Adamu yuyu huyu (aliahidi hivyo) atafunuliwa katika siku hizo kama ilivyokuwa katika Sodoma, juu ya nchi. Je, Yeye alifanya hivyo? Je, ni lazima litimie? Haiwezekani. . . Sasa, kumbuka, Yeye alikuja katika majina matatu: Mwana wa Adamu, nabii; Mwana wa Mungu, Roho; Mwana wa Daudi, kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini humo katikati, hiki kiunganisho, sasa kulingana na maneno Yake Binafsi katika siku ile atakapofunuliwa Mwana wa Adamu akijifunua kama (nani? si Mwana wa Mungu) Mwana wa Adamu. Atajifunua katika njia tofauti. Sasa, hilo lafanyaje? Malaki 4, kweli kabisa. Tazama, Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe, si katika madhehebu makubwa na kadhalika, kama tulivyoona katika nyakati zote, bali angejifunua kama Mwana wa Adamu tena, kudhihirisha Malaki 4, “Na katika siku hiyo, nitawapelekea Eliya nabii, naye ataigeuza mioyo ya watoto ielekee Imani ya baba wa kimitume, mbali na huu udhehebu, kurudia Neno la asili tena,” kuutoa ule Mti wa Bibi-arusi wa siku za mwisho ambao aliuahidi. “Wakati wa jioni kutakuwako Nuru,” si katika siku yenye ukungu, itakuwa nuru; itakuwa siku isiyoweza kuitwa mchana ama usiku. Mnaona, ni kuutengeneza ule Mwili. Bali Kichwa kile kile kilichokuwa hapa Mashariki, kiko Magharibi tena, “Wakati wa jioni kutakuwako Nuru.” Lo, jamani, najisikia kama niimbe wimbo!

Kutakuwako Nuru wakati wa jioni,
Mapito ya utukufu hakika mtayapata;
Katika njia ya maji, ndiko kwenye Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina Lake la dhamani.
Vijana kwa wazee, tumbuni dhambi zenu zote,
Ndipo Roho Mtakatifu ataingia hakika;
Nuru za jioni zimekuja,
Inajulikana na kuthibitishwa kuwa Mungu na
Kristo ni mmoja.

²²² Naye Mwana Adamu anajifunua katika nguvu zile zile alizokuwa (si katika nyakati za kanisa, katika kuhesabiwa haki, kutakaswa, mambo haya yote hapa) bali Mwana wa Adamu.

Mwana wa Adamu ni nani? Neno! Na Neno li jepesi kuliko, lina nguvu kuliko upanga wo wote ukatao kuwili, na linatambua mawazo yaliyo moyoni. Ilimlazimu kufanya nini? Hana budi kuthibitisha hilo Neno. Atafanya nini? Itazame tunapoona ikitendeka, itazame katika hali ile ile ambayo Yeye alikuwa hapo mwanzoni, ile Nguzo ya Moto. Jamani! Akithibitisha ya kwamba yeye ni Waebrania 13:8, ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ilikuwa nini? Yesu Kristo, yeye yule jana, huyo alikuwa Kristo aliyekuwa jangwani pamoja na Musa. Wangapi wanajua Biblia inasema hivyo? Jana! Huyo alikuwa Kristo wakati Paulo alipokuwa akinena hapa kwa ajili ya leo (mnaamini hayo?) katika Agano Jipya. Kisha Mwana wa Adamu, Kristo yule yule, katika siku za mwisho. Mnaona? Vema.

²²³ Tazama pia Yohana 14:12, Yeye alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Maandiko haya yote, Yeye hufanya nini? Yeye yuko hapa sasa akithibitisha (si wakati wa Luther, si wakati wa Wesley, si wakati wa Kipentekoste, si wakati wa Kibatisti, si wakati wa Kipresbeteria, tumepitia hayo na kuyathibitisha kwa historia katika Biblia; lakini nini?) ule wakati wa kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu, kuleta mambo haya kutimiza Neno wakati yote hayana budi kutimizwa. Mnaona? Tunaliona, na ni Kweli!

²²⁴ Na, wazia, kwa njia ile ile aliyofanya hapo kwanza, haijathibitishwa tu kati yetu, bali imethibitishwa na sayansi. Hawana budi kukubali kwamba ni kweli. George J. Lacy, mkuu wa FBI, wa hati zilizotiwa alama za vidole, kasema, “Nuru iligusa kile kioo cha kupigia picha. Mimi mwenyewe niliita saikolojia, lakini,” kasema, “Bw. Branham, kamera hii haiwezi kupiga picha saikolojia. Iko kule.”

²²⁵ Ni Nini? Ushuhuda, ya kwamba miaka mingi iliyopita wakati hiyo Nguzo ya Moto ilipokuwa imesimama kule katika kile kijiti kama upepo wa kisulisuli, ikinena, Yeye alisema, “Usivute sigara kamwe wala kunywa pombe, kuna kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mkubwa.”

²²⁶ Watu walisema, “Mvulana huyo amerukwa na akili.” Mamangu alitaka kumwita daktari, nilikuwa na wasiwasi.

²²⁷ Lakini ilikuwa nini? Yeye alishuka papa hapa mtoni pale, katika Mto Ohio na akasema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kuwatayarisha watu kusudi Neno lidhihirishwe, vivyo hivyo Ujumbe wako.”

²²⁸ Jinsi Dk. Davis na wengineo walivyoniita “alierukwa” na “akili,” alitaka kunifukuza kanisani, kwa sababu nilipingana naye juu ya wahubiri wanawake na mambo hayo yote yasiokuwa ya kimaandiko. Akasema, “Ati unasema utahubiri na kusababisha ufufuo ulimwenguni?”

Nikasema, “Si mimi, lakini Yeye alisema hivyo.”

Akasema, “Billy, ulipatwa na jinamizi.”

Nikasema, “Nitairudisha kadi yangu sasa hivi, mimi si wenu tena.”

229 Yeye alisema Hilo, naliamini, amelithibitisha. Hiyo ndiyo sehemu iliyo nzuri, amelithibitisha, akathibitisha Neno Lake kwa Neno, kwa kuwa Yeye ni Neno. Mnaona? Nalo Neno hufanya nini? Linajua siri za moyo. Sivyo? Vema, linathibitisha hilo katika Waebrania 13:8

230 Naye atakuwa na Kanisa-Bibi-arusi aliye tayari katika siku za mwisho. “Atafanyaje hivyo, Ndugu Branham?” Sijui. Lakini Yeye alisema atafanya hivyo. Atalithibitisha. Aliyeitwa kutoka katika mengine yote, hiyo ni kweli, ndege mwenye madoadoa kwa Damu Yake. Mnaona? Walioitwa watoke, kundi lingine lote linampinga. Yeye anadharauliwa na kukataliwa.

231 Lakini yule ndege mwenye madoadoa, sasa, sijali jinsi yule mwandishi alitaka kupinga hilo, amekosea. Kumbukeni, yule ndege alifanyiwa nini? Yule ndege mwenye madoadoa? Waliwachukua wawili, mmoja akauawa, yule mwenziwe, akamwagiliwa yule ndege mwingine, na ilikuwa kwa ajili ya kutakasa ukoma, na madoadoa ya damu, na kupasa sauti, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana.” Na huyo alikuwa Mume wetu, Yesu Kristo, ambaye aliuwawa, na Damu Yake juu yetu ikilia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana.” Hao ndege wengine wote. . . Nina furaha kwamba Jina langu limo katika Kitabu chake; si humu duniani, bali kule juu; si katika ngozi ya mbuzi, bali katika ngozi ya Mwana-kondoo. Hiyo ni kweli.

232 Kutakuweko na ufufuo wa wafu. Yeye atathibitisha hilo. Hiyo ni kweli. Atathibitisha. Kutakuweko na kunyakuliwa kwa Kanisa. “Itakuwaje?” Sijui, bali atathibitisha hilo. Neno Lake ni kweli. Kutakuweko na ule Utawala wa Miaka Elfu. Atalithibitisha, ni Neno Lake. Kutakuweko na mbingu mpya na nchi mpya. Atathibitisha hilo, kwa sababu Neno Lake lilisema hivyo. Na ni wenye haki tu watakaokuweko huko. Atalithibitisha hilo pia. Hiyo ni kweli. Ni wale tu ambao wamekwisha kufanywa sehemu ya hili Neno (mwaona, watakaokuwa sehemu yao na mahali pao katika hili Neno la wakati wao) ndio pekee watakaokuweko kule. Maana, hivyo ndivyo tu ilivyo, Yeye ni Neno. Na mwanamke ni nini? Mfano wa mwanamume. Na Kanisa ni—Kanisa ni nini? Mfano wa Neno, hivyo ndivyo hasa. Mnaona? Kwa hivyo itakuweko, sawa kabisa. Ni waamini tu wa kweli katika Neno Lake wanaojua Hili na wanaweza kuliadini. Naye Mungu huwasaidia kuithibitisha, hiyo ni kweli, hivyo ni kweli.

233 Mnaamini hiyo sasa? Mnaamini? Ikiwa ndivyo, nyosheni mikono yenu kwa imani mkaliguse vazi Lake, kwa sababu yuapita hapa. Yeye atathibitisha ya kwamba ni yeye yule jana leo, na hata milele, Waebrania 13:8. “Na tazama, Mimi nipo

pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mathayo. Naye ni Kuhani Mkuu, kulingana na Waebrania, Kitabu cha Waebrania, sura ya 4 na kifungu cha 15, “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu.” Je, unaamini hilo? Nyosha mkono wako ukamguse Bwana. Yeye yupo daima, “Na tazama, niko pamoja nanyi siku zote.” Tazama kote katika zile nyakati. “Jaribu mambo yote. Shikilia yaliyo mema.”

²³⁴ Sasa, ikiwa wewe ni mfuasi wa kanisa ambalo haliamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo na hata milele, yeye yule katika kila njia, ondoka kwake. Thibitisha!

²³⁵ Sasa, tunasema Yeye amefufuka kutoka kwa wafu. Sisemi hivyo, Neno hapa lilisema hivyo. Wao walisema, “Yeye alifufuka kutoka kwa wafu.” Anasema ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? Yeye aliahidi mambo haya yatatendeka katika siku za mwisho, ya kwamba Mwana wa Adamu yule yule atadhihirishwa.

²³⁶ Sasa, kumbuka, huyo hakuwa Yesu akinena na Ibrahimu pale, ambaye angeyatambua mawazo rohani mwa Sara nyuma yake. Huyo hakuwa Yesu, hakuwa amezaliwa bado. Bali alikuwa mtu katika mwili; ambaye Ibrahimu alimwita “Elohim, yule Mkuu Mwenyezi.” Ikionyesha...Naye Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” sasa tazama kwa makini, “katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu atakapokuja, Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.” Si tena kama kanisa, unaona, si tena; Bibi-arusi amekwisha kuitwa, mnaona. “Katika siku hiyo Mwana wa Adamu atafunuliwa.” Nini? Kuliunganisha Kanisa kwa kile Kichwa, kuliunganisha, arusi ya Bibi-arusi. Wito wa Bwana Arusi utakuja hapa, wakati Mwana wa Adamu atakaposhuka aje katika mwili wa mwanadamu kuunganisha hivyo viwili pamoja. Kanisa halina budi kuwa Neno, Yeye ni Neno, na hivyo viwili vitaungana pamoja, na kufanya hivyo, itachukua dhihirisho la kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu. Si kasisi. Si—Sijui, mimi . . . Mnaona lile ninalomaanisha? Mnaona, ni Mwana wa Adamu, Yesu Kristo, atakayeshuka katika mwili wa mwanadamu kati yetu, naye atafanya Neno Lake dhahiri sana hata litaunganisha Kanisa pamoja Naye kama mmoja, Bibi-arusi, kisha ataenda Nyumbani kwenye Karamu ya Arusi. Amina. Tayari amekwisha tunaunganishwa. Unaona, tunaenda kwenye Karamu ya Arusi, si kwenye arusi “. . . jishibisheni. . . wenyewe, na nyama zote za watu hodari sababu arusi ya Mwana-Kondoo imekuja.” Lakini, kule kunyakuliwa, ni kwenda kwenye Karamu ya Arusi? Wakati Neno hapa, liunganikapo na mtu, na hao wawili huwa mmoja. Ndiposa linafanya nini basi? Linamdhihirisha Mwana wa Adamu tena, si wanathelogia wa kanisa. Mwana wa Adamu! Neno na Kanisa wanakuwa mmoja. Lo lote afanyalo Mwana wa Adamu, Yeye alikuwa Neno, Kanisa linafanya jambo lile lile.

²³⁷ Je, Yeye alijithibitishaje katika nyakati zote? Kupitia kwa manabii, ambao wangenena Neno, kujua mawazo yao. Hivyo ndivyo Yeye alivyojulikana, hivyo. Aliahidi kwenye ule wakati wa kanisa, tuliopitia “si usiku wala mchana,” bali katika wakati wa jioni wakati Mwana wa Adamu angefunuliwa. Itarudi tena. “Kutakuwa Nuru wakati wa jioni.” Mnaona? Yeye hufanya nini? Anathibitisha Neno Lake.

²³⁸ Sasa tazama nyuma je, Yeye alikuja kama bikira, je alikuja kama walivyosema, kupitia kwa bikira, hasa? Je, Yeye alikuja jinsi hasa alivyosema? Tazama siku hizi, Yeye alithibitisha Neno Lake haidhuru wasiosadiki Mungu wangepi, makafiri, wasiojali, Yeye alikuja tu moja kwa moja, akathibitisha Neno Lake. Tuko hapa, tumepitia wakati huu wa makanisa yote na kadhalika, wakaondoka kama walivyofanya tangu Malaki hata kule kuja kwa Kristo. Manabii wote na kadhalika waliisha koma, na wajifanya watu mashuhuri na kadhalika, lakini, sawa sawa kabisa, tazama aina ya mtu aliyemtuma. Kama tu Eliya, anayechukua wanawake walio watovu wa uadilifu, na waliojipaka rangi nyingi sana, poda na madawa ya kujirembesha na takataka kama hizo pale. Nao makasisi, akawaua kulia na kushoto. Akija kutoka jangwani, hakumchezea hata mmoja wao, kisha akasema, “Masihi yuko njiani. Nitamjua atakapokuja, nitamjulisha. Amina. Msianze kuwazia ninyi ni wa *hiki* ama *kile*.” Jinsi tu alivyofanya Eliya!

²³⁹ “Na katika siku za mwisho, itakuwa, kabla haijaja ile siku ya Bwana, iliyo kuu na ya kuogofya nitawapelekea, kabla haijaja hiyo siku iliyo kuu na ya kuogafya, nitawapelekea nabii Eliya, naye atairudisha Imani ya watoto kwa baba zao.” Basi tazameni, Imani ya baba iwaelekee watoto, Wayahudi. Mnaona? Ahadi yao ya Maandiko, Mataifa na pale walipoangukia. Tazama hao wawili kikamilifu kabisa, sawa kabisa. Na hapa tunalionga, Mungu akithibitisha Neno Lake.

²⁴⁰ Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi. Mungu mpenzi, uliyemfufua tena Bwana Yesu katika wafu, kuthibitisha Neno Lako, naye yuko hai leo, anathibitisha Neno Lako. “Lo, niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari,” anathibitisha Neno Lake. “Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.” (Kama haikuwa “milele,” labda huenda—huenda ukakwazwa na baadhi yake.) Sikuchukua muda kulieleza, Bwana. Lakini, *milele*, wao wanajua, ni “mu—muda wa wakati.” Na sasa baada ya wakati huu, hakutakuweco na wakati mwingine milele, itakuwa Umilele. Kwa hivyo Yeye alikuwa Mungu yule yule aliyekuwa katika Musa na katika manabii. Kisha akaja baada ya muda fulani, akajifanya mtu, akajidhihirisha kama Mungu-nabii. Kisha tulikuwa na muda fulani, kisha akaja tena. “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²⁴¹ Tunawazia hili, Sulemani, katika ule utawala mkuu wenye ufanisi wa Wayahudi, ambapo hapana taifa lililothubutu

kuwagusa, na kile kipawa kikuu cha Mungu kilikuwa katika nabii huyo hata akamwambia yule malkia siri zote za moyo wake, hamna neno lililofichwa. Huo wakati mkuu, ukionyesha na kuonyesha kwa mfano kwamba Wakati mkuu unakuja.

²⁴² Na sasa, Baba, huyo alikuwa Wewe, si Sulemani. Huyo alikuwa Wewe katika Yesu, kwa kuwa Yeye alisema, “Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba.” Mwili Wake ulikuwa kiumbe kilichokombolewa. Na sasa katika nyakati zote kanisa lilipoteza upendo wake wa kwanza, na sasa katika siku za mwisho Wewe uliahidi kuwaita walio wachache sana, lile kundi ndogo, kwenye siku za mwisho.

²⁴³ Baba, mioyo yetu inarukaruka, na moyo wangu unapigapiga, ninapowazia hayo na kujua ya kwamba maneno yako ni kweli, hamna hata moja linaloweza kushindwa. Hebu na watu hawa leo wafahamu hilo na mwenye dhambi akutafute saa hii, kabla milango haijafungwa kisha hakutakuwa na wakati tena. Hebu na Bibi-arusi, anapoanza kupiga hatua vibaya toka *hili*, na *lile*, hebu yeye ashike mwendo vizuri kama vile lile ono lilivyoonyesha majuma machache yaliyopita.

²⁴⁴ Nakuomba, Ee Baba, kubariki sasa, na kuwaponya wagonjwa. Hapa kuna nguo zilizowekwa hapa, na lesu kutoka...vimetoka sehemu mbalimbali. Na sasa, katika Maandiko, ilisemwa, “Kulichukuliwa nguo na vitambaa, lesu, toka katika mwili wa Paulo, nazo zikapelekewa wagonjwa, kisha Mungu akawaponya.” Sasa, tunajua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali tunajua ya kwamba haikuwa Mtakatifu Paulo, ilikuwa imani ya watu kwamba yeye alikuwa mtumishi Wako. Bwana, hawa watu hawangeliendesha magari haya mamia ya maili kama hawakuamini. Wakirimie imani yao, Bwana, huku mimi...si kuzitia mafuta hizi lesu (Paulo hakuzitia mafuta kamwe, alizitoa mwilini mwake), na kama ninapozishika lesu hizi, Bwana, si kwamba mwili wangu (kwa kuwa haufai kitu), bali ni mali yako iliyokombolewa, kwa hivyo naomba, Mungu, ya kwamba utaiheshimu imani yao. Na kila mmoja wao aponywe, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sasa, Bwana, Ujumbe mrefu, sikukusudia kuuhubiri zaidi ya dakika chache, bali sasa masaa mawili au zaidi yamepita. Basi na wagonjwa waponywe, Bwana, hebu na watu waone ya kwamba Wewe uko hapa, ya kwamba sikusema tu haya mimi mwenyewe. Ni wewe, Bwana. Nami naomba katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴⁵ Sasa, kwa yapata dakika kumi tu. Sijui...(Je, uli—ulisambaza zo zote humu, zilikuwa zipi? Billy alisema alisambaza baathi yake. Nilimuuliza afanye hivyo asubuhi ya leo. Nami niliingia tu dakika chache zilizopita kule nyuma, nami sikupata nafasi ya kumuliza, kwa maana nilikuwa nikiongea na Ndugu Ben na wengineo humu. Sikupata nafasi ya kumwambia. Aliniambia tu alisambaza kadi za maombi. Kadi ya maombi B,

mia moja. . . (Moja mpaka mia moja?) B. Vema, hebu, naamini, kadi ya maombi nambari moja, B. Nani aliye na B? Waweza. . . Kama unaweza kusimama, inua mkono wako, kama unaweza kutembea. Wanawake fulani walio kule nyuma. Vema, B, namba moja, namba mbili, tatu, nne, tano, njoni *huku*. Nami nitawauliza watoto hawa iwapo wanaweza tu kuja hapa nyuma ya jukwaa waketi hapa. Sasa, vema. Sasa, sasa nawaambieni, watumeni, pitieni kwenye yale marefu pale, ninyi watu kutoka moja hadi tano, pitieni pale na mje huku. Hebu na wale walio kwenye yale marefu kule, wakiweza, waje moja kwa moja upande huu kuelekea kwenye viti vyao. Sasa, watoto wadogo wanaoketi hapa, njoni huku nyuma ya jukwaa. Nami nataka wapitie hapa karibu, hao watu, nipate kuwaomba.

²⁴⁶ Sasa, hebu tuone sasa. Naona. Niliita zipi, moja mpaka tano, sivyo? Moja mbili, tatu, nne, tano. Moja. . . Kila mtu aliye na kadi ya maombi pale, moja hadi tano, inua mkono wako, angalia kama hao wote wamesimama. Kuna moja, mbili, tatu, nne. Mmoja amekosekana. Moja, mbili, tatu, nne, katika B. Nyote ni moja, mbili, tatu, nne? Moja, mbili, tatu nne? Iko wapi tano, B? Tano, rudi hivyo, bibi. Vema, bwana, rudi hivyo. Naam. Zunguka moja kwa moja kisha urudi, tano. Sita, saba, nane, tisa kumi. Vema, B, kadi ya maombi sita, saba, nane, tisa, kumi. Mnaona, tunafanya hivi, ndipo basi hutasumbuliwa kamwe. Sita, saba, nane, tisa, kumi. Sasa nina. . . Nafikiri. Je, una kadi, bwana unayesimama hapa. Saba? Vema, nenda pale, uende pamoja nao. Nina mbili tu, nafikiri, hapo. Vema, sita, saba, nane, tisa, kumi, kadi ya maombi sita, saba, nane, tisa, kumi. Nina mbili pkee, hapa kuna. . . Una moja, bwana? Ndivyo hivyo. Ndizo hizo. Kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Sasa hiyo ingekuwa moja, mbili, tatu, nne, tano. Vema, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini. Moja, mbili, tatu, nne, hivyo. Sawa, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano. Moja, mbili, tatu, zunguka hivyo, bwana, zunguka, simama mstarini, ishirini na tano, ishirini na tano. Msaidie pale, hebu aende po pote anapotaka. Hapa basi, ndugu, papa hapa, wamekufungulia njia. Hao watu wamekufungulia njia hapa. Mtu fulani amsaidie papa hapa, ukiweza. Hebuni azunguke aingie mstarini pale. Nakwambia, mketishe chini pale, na nambari yake itakapoitwa, mweke pale. Mnaona? Atakapokuja katika namba, mweke mstarini. Vema, nafikiri hao ni idadi ambayo—wangeenda sasa.

²⁴⁷ Sasa, ni wangapi hapa wasio na kadi ya maombi, nanyi mna matumaini, mna—mna hakika kabisa ya kwamba Mungu anaweza kuwaponya wagonjwa? Inua mkono wako. Mnaamini? Wangapi wenu hapa wametoka. . . ambao wanajua ya kwamba sijui lo lote juu yenu, sijui magonjwa yenu? Kuna—kuna watu hapa sasa, Maskani yangu, kwa mmoja wenu mlio wageni, ni

vigumu kumwona mtu ye yote, isipokuwa hawa wahudumu. Kule chini namwona mtu fulani ninayeweza kumtambua. Sikai hapa vya kutosha, mnaona, nao ni watu tu wanaotoka kila mahali. Wangapi humu ndani. . . Hebu niwathibitishieni. Wangapi hapa wanajua sijui lo lote kuwahu? Inueni mikono yenu hapa. Mwaona, huo ni mkono wako mbele ya Mungu, mnaona. Sijui neno kuwahu. Sasa, sijui kwamba huenda nikampata mtu atakayeitwa katika mstari wa maombi kama huu, ambaye nilimjua, bali singejua kwa nini wako hapa. Mnaona, singejua kilichowaleta hapa.

248 Sasa ninalojaribu kufanya ni kuwafanya muone hili, sasa tazama, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Je, mnaamini hilo? Je, mnaamini Yeye atalithibitisha hilo Neno? Vema. Je, Yeye alisema angejifunua kama Mwana wa Adamu mwishoni mwa wakati wa kanisa? Wangapi? Na ulimwengu ungeonekana, uwe katika hali ya Sodoma na Gomora? Je, mnaamini hilo?

249 Sasa, Billy, mbona usiwaache wapitie hapa? Naam, vema. Vema, sawa, vema.

250 Mwi—mwishoni mwa wakati, Yeye atajifunua Mwenyewe. Sasa, tazama, mnatambua kwamba, basi, hapa kuna kutowezekana kabisa? Sasa, hapa kuna watu wanaosimama katika huu mstari, ambao sijapata kuwaona maishani mwangu. Kuna watu wanaoketi kule, ambao kamwe sijapata kuwaona. Lakini, kumbukeni, Waebrania 4:15, naamini ndipo ilipo, ambayo ilisema ya kwamba “Yeye ni Kuhani Mkuu sasa awezaye kuchukuliana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.” Hilo ni kweli? Sasa, iwapo Yeye ni Kuhani Mkuu, basi Yeye ni Waebrania 13:8, basi. “Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Hilo ni kweli? Yeye angejifunua? Kama nilivyowaambia, Yeye kila mara hunena kupitia kwa manabii Wake. Yeye kila mara hutuma u—u—ujumbe kabla ya hukumu. Sasa, haya yote, habadili kamwe njia Zake.

251 Yeye aliamua katika Bustani ya Edeni, jinsi angemwokoa mwanadamu, kwa damu ya a si ye na hatia, Yeye hajabadili hilo kamwe. Sisi hujaribu kuyageuza, kwa elimu, kwa minara ya Babeli, kwa miji mikubwa, na kila kitu kama hicho. Tunajaribu kuigeuza, bali haitafaa kitu. Sisi hujaribu kugeuza, kwa kuwaelimisha walimwengu Kwake. Tunajaribu kuyageuza, kwa dhehebu la watu. Haijafaulu kamwe. Ni mahali pamoja tu ambapo mwanadamu hukutanika kuabudia, chini ya Damu. Madhehebu yenu yatawatenganisha, bali chini ya Damu ninyi mko sawa. Yeye habadiliki kamwe.

252 Sasa, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu asiyebadilika, na ni yeye yule jana leo, na hata milele, basi Yeye anapaswa kutimiza Neno hilo. Si kwa sababu tulisema Yeye alifanya hivyo, kwa sababu Yeye alisema angefanya hivyo. Mnaona? Sasa, sasa, kama

atafanya hivyo. . . Sasa, hebu ngoja dakika moja, wazia. Sasa, wangapi wenu katika huu mstari wa maombi wanajua kwamba sijui hata jambo moja kuwahusu, ugonjwa wako? basi inua mkono wako, unajua ninacho- . . . Ni wangapi kwenye huo mstari wa maombi wanaojua siwajui? Inueni mikono yenu.

²⁵³ Angalia katika umati, unaona. Sasa, ninyi mlio huko nje, hamhitaji mwe hapa, ninyi tu guseni vazi Lake. Nena tu, sema, “Bwana Yesu, nakuamini Wewe.” Sasa wewe sema, “Ninaamini Hilo. Na ni—ninaamini kwamba—kwanba Wewe unaweza kumfunulia Ndugu Branham, kwa sababu . . .”

²⁵⁴ Naam, si kwa sababu eti ni Ndugu Branham, yeye in mtu wa kawaida tu. Na labda kama Kunyakuliwa kungalitukia asubuhi ya leo. . . Wazia juu ya kunyakuliwa. Kunyakuliwa kukitukia asubuhi ya leo, nasema hili kwa unyenyekevu, hapana shaka kwamba nusu ya kusanyiko hili, tungaliamua kulingana na viwango, kulingana na viwango, kulingana na mahali tunapopaswa kuwa, nusu yenu mngalinitangulia. Hiyo ni kweli. Mimi si. . . Tazameni jukumu nilio nalo, na jinsi—jinsi ninavyolitekeleza kwa ulegevu. Mimi ni mtumishi wa Kristo asiyeftaa, kujua yale nijuayo kumhusu kisha kuishi ninavyoishi, si kizinzi, si mchafu, si vitu kama hivyo, Mungu anajua hilo ni kweli. Mnaona? Mimi hujaribu kuishi sawa, lakini na—na—naonekana kama kwamba siwezi kupata njia ya kulieleza. Labda kama ingalikuwa mtu mwingine, labda mwenye elimu sana ama cho chote kile, wangeliwaeleza watu. Lakini wengine watadhani, si watu wote watakaopata, kwa vyo vyote. Mnaona? Mnaona! Mnaona, Yeye anajua atakachofanya. Kwa hivyo najitolea Kwake tu na kusema, “Bwana, mimi nimo mikononi Mwako, fanya nami unachooka kinafaa.” Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. . .

²⁵⁵ Sasa, naamini ninamjua mwanamke huyu. Siwezi kukumbuka yeye ni nani, bali namjua. Namjua kwa namna fulani. Lakini nimekwishaona uso wake, sijui ni nani sasa hivi. Lakini na—namjua, kwa namna fulani. Je, hunijui? Aha. Ni—niliwazia, nikimtazama usoni, nilidhani namjua, bali siwezi kukumbuka yeye ni nani. Bali naamini yeye. . . Si mume wako. . . Wewe si mwanamke yule anayefanya kazi. . . Mumewe anafanya kazi katika Saba-Saba-Saba, ama Saba-Kumi na Moja, una kitu kama hicho, kule New Albany. Bi. Agan, hiyo ni kweli. Sasa, umekuwa hapa nawe huja kanisani. Roy, huyo ndiye tuliyemtembelea siku moja kwenye. . . Huyo—huyo ndiye aliyekuwa huko mlimani? Unasemaje? Dada yake. Huyo alikuwa, hivyo ndivyo, mnaona. Nakumbuka mimi na Roy tulipokuwa tukiendesha gari, naye akataja jina hilo, kisha Bwana akanituma huko na akamponya huyo mwanamke papo hapo. Naam, bwana, nami nilikumbuka tu.

²⁵⁶ Sasa, ila kujua shida yako ni nini, sina neno. Unajua hilo. Lakini ikiwa Bwana Yesu anaweza kuniambia jambo fulani

alilotenda. Au ikiwa yeye—yeye ana shida ya kifedha. Labda yeye na mumewe walikuwa na shida, labda yeye na watoto wake, labda mmoja wa watoto wake, iwapo ana watoto, sijui. Lakini kama yeye anao, labda baadhi ya watoto wao wako—wako nje. Labda anasimama hapa kujua neno juu ya hayo. Sijui. Sina njia ya kujua neno juu ya hayo. Sijui. Sina njia ya kujua. Si—si—siwezi kuwaambieni. Bali anajua. Mnaona? Kwa hivyo, mwaona? Mnaona

²⁵⁷ Sikizeni, sasa shikeni hili kwa makini sana. Sijapata kusema hili mkutanoni kabla, bali najisikia kuongozwa kulisema sasa. Neno ni nini? Ni wazo lililotamkwa. Sasa, nawezaje kutamka wazo lake, nawezaje kumweleza wazo lake ni nini? Haina budi kuwa baadhi ya mawazo mengine yaliyotolewa, naye hawezi kufanya hivyo. Kwa hivyo sina budi kutamka wazo Lake, na kama ni kweli. . . Kama ni wazo la Mungu, litakuwa sahihi; iwapo si wazo la Mungu, basi halitakuwa sahihi; atajua mtajua, wote watajua. Mnaona, hamna njia ya kuliepa. Itakuwa ni Mungu au si Mungu. Neema Yake yatosh. Sasa mnaamini, sasa, kila mtu.

²⁵⁸ Ni wangapi wataamini? Vema, labda haujawahi kuona mmoja wa mikutano hii hapo kabla, lakini mtaamini kama Mungu akifanya hivyo? Halafu ninyi huko sasa, hamtakuwa katika mstari wa maombi, ninyi—ninyi ombeni, pia, mnaona. Ama hata kama mnakuja katika maombi, sijali wewe ni nani, omba tu.

²⁵⁹ Bwana Yesu, sasa nimechukua wakati mwingi, bali ni ibada yako, Bwana. Nami nimefanya yote niwezayo kufanya kama mwanadamu, lakini Wewe ni Mungu, sasa yaliyobaki yako mikononi mwako, Baba. Hubu na ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu, Neno Lako ni Kweli. Thibitisha Neno Lako, Bwana, la siku hizi za mwisho wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa. Yeye alijidhihirishaje? Alikuwa Neno. Neno ni nini? Mpambanuzi wa mawazo na maksudi ya moyo. Yeye alitambua mawazo yao, akamwambia Petro, Filipo, Nathanieli, yule mwanamke kisimani, hao wengine wote kule, wakati walipomjia, alijua yule msichana mdogo alikuwa amelala, hajafa. Naomba, Mungu, ya kwamba utayatumia maskani yetu manyanyekevu leo, ya makao ya hapa duniani, upate kujidhihirisha Mwenyewe. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁶⁰ Sasa kuponya, siwezi, mnajua hilo. “Karama ni nini, Ndugu Branham, kitu unachochukua?” La. Ni jambo ambalo unajua jinsi ya kujiondosh. njiani. Mnaona? Mradi tu uko pale haitafaulu. William Branham ndiye adui mkubwa sana niliye naye. Mnaona? Bali nikimwondoa, njiani, mnaona, basi Yesu Kristo anaweza kuutumia huo mwili. Mnaona? Mnaona sasa, naja kwa mwanamke huyo. Nini basi? Sasa tuseme kama—kama yeye—kama alikuwa mgonjwa.

²⁶¹ Hapa yupo bibi aliyeulaza mwili wake juu ya—ya kiti. Sasa, kama mimi. . . kama Yesu alikuwa hapa, naye aende amwekee huyo mwanamke mikono, mwili huo ungepona. Hapana shaka kuhusu hilo. Lakini, mnaona, sisi ni binadamu walio na mikono michafu. Mikono Yake ni mitakatifu, Mungu alimthibitisha. Yeye alikuwa Neno. Mnaamini hilo? Hakika, Yeye hakuwa na mashaka. Angemwekelea mikono Yake, aseme, “Binti, upate afya,” naye angepata afya. Lakini basi Yeye alituagiza tutende jambo lile lile. Nafikiri amelidhihirisha wazi.

²⁶² Naam, vipi kama Yeye angenipa ono, na nimwambie mwanamke huyu jambo la kufanya? Kwamba, vema, naamini basi kama nilimwekea mikono, yeye angepata afya, Mnaamini hilo? Lakini vipi kama Yeye hakunipa hilo ono? Ono hilo lingefanyaje? Lingenipa tu imani. Kupeleka imani yangu, ile nguvu isiyoonekana ya Mungu. Mnaona? Sasa, kama ninyi, kila mmoja wenu akifa dakika ii hii, haungalijiona *wewe* mwenyewe ukiondoka mwilini. Fahamu zako zote, vyote ulivyo vingendoka, bali hungaliviona vikienda. Mnaona? Ingekuwa. . . Ile nguvu inayonifanya nisogeze mikono yangu, hiyo ni nguvu, sivyo? Ile nguvu ambayo ingenifanya niwazie, nguvu inayonifanya nihubiri, nguvu inayonifanya niishi, nitende, nguvu hiyo hiyo inayoweza kuuendesha mwili huu ingeuacha nawe hungaliona hiyo nguvu ikiondoka. Ni nguvu isiyoonekana. Vivyo hivyo imani nayo! Msikose hili. Imani! Naye Yesu alisema, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa.” Sasa, unaona kama niliondoka nikapata ono na kumwekelea mikono, naamini atapata afya, kwa kuwa niliona ono, tumaini langu liko katika hilo ono. Lakini na Neno je? Weka mikono kwa imani ile ile. Ono linatolewa tu kuhuisha imani yangu pamoja na imani yako. Kwa imani ile ile bila ono, itafanya kazi vivyo hivyo. Watu wengine wamepewa imani kuu. Wengine hawana imani ya namna hiyo, wao hupewa ono lipate kuwapa imani hiyo. Mnaona? Sasa, mnaona, ingekuwa mikono ile ile michafu, iwe mtu yule yule, bali kumwekea tu mikono.

²⁶³ Sasa, hebu na Roho Mtakatifu athibitisha uwepo Wake, athibitisha Neno Lake aliloahidi. Sasa, nilisahau jina lako lilikuwa nani. Jina lako nani, sasa? Agan. Vema, Yeye angeliniambia hilo kama alitaka, waona, bali nasema tu ya kwamba na—nakujua. Sasa, hebu njoo papa hapa kidogo, sokea karibu, kuna watu wanaosimama hapo wakiomba, mnaona. Huyu ni. . . Sasa, Bi. Agan, kama ni—kama mimi ni mtumishi wa Kristo, nami nimehubiri Neno ambalo ninaamini ni kweli, unaamini hivyo? [Bi. Agan asema, “Naam.”—Mh.] Unaamini hivyo. Sasa, iwapo una haja ya jambo fulani, singelikupa, kwa sababu sina nipate kukupa; isipokuwa labda iwe ni fedha kidogo ama cho chote kile, ama ningaliongea na mumeo ama watoto ama watu unaowapenda ama cho chote kile, ningefanya hivyo. Bali kama ukihitaji upanyaji, singalikupa, huo tayari

umekwisha kununuliwa. Bali kwa karama, naweza kukufanya utambue, kama una imani, ya kwamba huo tayari umekwisha kununuliwa, kwa sababu Yeye Yule aliyeununua, Yeye Yule ambaye ungemwamini, ndiye Mwana wa Mungu. Yule Mnunuzi anasimama hapa. Unaona? Sivyo? Mnunuzi yuko hapa.

²⁶⁴ Sasa, unanijua kama ndugu, muhudumu, nami nakujua kama dada. Tunamjua yeye kama Mungu. Sasa, kama huyo Mtu asiyeonekana, kwa karama niliyo nayo ya kujiondosha njiani, anaweza kuniambia, akwambie wewe kupitia kwangu, kinywa changu, waona. Sasa, wakati ninapooomba, Mungu hanioni, anasikia tu sauti yangu kupitia kwa Damu ya Yesu. Mnaona, hanioni, husikia tu sauti yangu. Na hiyo Damu pale ni ya kuwakilisha yale ninayoomba. Mnaona? Ndipo Yeye husikia sauti yangu, bali Yeye huona tu Damu. Mnaona, yeye hanioni, kwa hivyo siwezi kuwa mchafu ninapokuwa chini ya ile Damu. Damu husafisha. Waona, Yeye ndiye ile kinga kati yangu na Mungu, naye aliahidi, “Mkimuomba Baba lo lote, nitalifanya.” Je, unaamini hiyo ni kweli?

²⁶⁵ Sasa, kama kila mtu...yaonekana kama kwamba...Je, maweza kuona hilo linalotendeka? Tazama, hapa inakuja, mnaona, Nuru, ya majano, ikizungukazunguka.

²⁶⁶ Sasa, yeye hangalijificha hata kama ingalimlazimu kufanya hivyo. La, la. Uko hapa kwa ajili ya jambo fulani lililokupata. Umekuwa na ugojwa wa pafu, nawe umekuwa hospitalini. Umekuwa chini ya hema la oksijeni. Nawe unaugua kwa ajili yake. Utaona. Yesu Kristo atakuponya, waona, nawe utapata nafuu. Endelea, ukiliamini. Dada Agan. Nitakuwekelea mikono yangu, katika Jina la Yesu. Mungu akubariki, dada. Nenda, ukifurahi, usitilie shaka aliyosema.

²⁶⁷ Washindaje, dada? Si—sidhani nakujua. Sisi ni wageni. Sasa, hapa pana mwanamke ambaye simjui. Sikujui. Sina njia ya kukujua. Lakini unaamini ya kwamba Mungu angenifunulia, kwa Neno Lake, waona, kwa sababu yeye aliahidi? Je, unaamini ya kwamba yeye angeniambia jambo fulani kukuhusu? Na hiyo ingekufanya ulikubali, sivyo, ukijua ya kwamba haingekuwa mimi, ndugu yako, ingekuwa yeye, Mwokozi wako. Je, unaamini hilo? Unangojea kufanyiwa upasuaji. Umekwisha ambiwa inakubidi ufanyiwe upasuaji. Unaamini Yeye anaweza kuniambia upasuaji ni kwa ajili gani? Ni katika tumbo, na kwenye matumbo. Hiyo ni kweli hasa. Unataka kuupea. Je unaamini sasa, huyu Roho akiwa humu, huku Roho wa Kristo ametuzunguka na akisimama juu yangu. Unajua ilipasa kitu fulani kikwambie, kwa maana sikujui. Unaamini, kwa kuwekewa mikono, hiyo ingepitisha imani ninayoamini, pamoja na imani yako, na mbele za Mungu, Baba yetu, ungeponywa? Basi, Bwana Yesu, natii amri Zako, uliposema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapona,” hebu dada yetu aponywe kwa utukufu wa

Mungu; katika Jina la Yesu, amina. Nenda zako nyumabni, sahau huo, unaona, endelea kuamini kwa moyo wako wote.

268 Washindaje? Nasema hilo ili tu nipate roho yako, mama. Kama tu vile Yesu alivyofanya pale kisimani, kasema, “Nipe maji ninywe.” Naam, naamini. . . sidhani nimewahi kukuona, naamini wewe ni mgeni kwangu. Sivyo? Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako ili kusanyiko lipate kuona. Simjui huyu bibi.

269 Sasa, huu ni uponyaji halisi, ni imani halisi, Maandiko halisi, Neno la Mungu lisilotiwa najisi likidhihirishwa na kuthibitisha kuwa Yeye si mfu, yu hai hata milele. “Naye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, naye atazifanya, na huyu mwamini ataweka mikono yake juu ya wagonjwa nao watapata afya.” Lo, unawezaje kulitilia shaka? Unaona? Sasa, Yeye alijua ni nani angalifanya hivyo na ni nani hangefanya hivyo, sijui. Hayo ni juu yake.

270 Lakini sasa ikiwa huyu mama ni mgeni, sasa, simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye ni kijana mwanamume, mchanga sana kuliko—kuliko mimi. Bali mimi—mimi sijapata kumwona. Naye yuko hapa kwa kusudi fulani. Je, unaamini kwamba mambo haya ambayo nimefundisha katika Biblia, bibi, kuwa ni Kweli? Unaamini ni Kweli. Na unayakubali, si kwa sababu niliyasema, kwa sababu Mungu aliyasema?

271 Je, unaamini tunaishi katika siku za mwisho Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa? Hilo lingekuwa Neno lililokusanywa kupitia kwa Luther, Wesley, Batisti, na hao wote, na Wapentekoste, yote yakisha kukusanywa katika ufunuo wa yale yote yaliyokuwemo. Yule malaika wa saba alipaswa kufungua ile siri ya muhuri sita. Yote yamekusanywa katika Mwana wa Adamu, utimilifu Wake wa wakati umefikia utimilifu wa Neno Lake, kudhihirisha utimilifu wa Mwili Wake. Huo ni hili Neno, basi, hilo ni Neno lililonenwa likidhihirishwa na Neno, kufunua Neno.

272 Sasa, kama Mungu anaweza kuniambia shida zako, au ni nini, hasa. . . Yeye alikufanya, anajua habari zako zote. Na kama anaweza kuzifichua. . . Unaonekama kama mtu mwenye afya nzuri. Bali kama anaweza kunifunulia, utajua iwapo ni kweli ama si kweli. Utaikubali? Sasa, nitazame. Bila shaka, unavalia miwani imekulazimu—imekulazimu kuivaa. Hilo silo lililokuleta hapa. Naona hilo lilirudi nyuma kabisa, unaona. Sasa uko hapa kwa ajili ya damu kugandamana. Unaona? Unaona? Je, unaamini Yeye anaweza kuniambia ilipo? Miguuni. Je, unaamini huyo anayefanya hivyo ni Mungu? Unaamini Mungu anaweza kunipa habari zaidi juu yako? A-ha? Ni sawa kwamba wewe ni mgeni, nami. . . kuzungumza nawe kwa dakika moja. Je, unaamini Yeye anaweza, je, unaamini ya kwamba Yeye anaweza kuniambia ulikotoka? Unatoka Gary, Indiana. Je, unaamini ya kwamba

Yeye anaweza kuniambia wewe ni nani? Bi. Ogden. Hiyo ni kweli. Sasa rudi nyumbani ukapate afya, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁷³ Umeshindaje? Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine, pia. Sikujui mimi, unaona. Bali je, unaamini ya kwamba Bwana Yesu anaweza kunionyesha shida yako? [Yule dada anasema, “Najua.”—Mh.] Unajua hivyo. Asante, dada. Hilo ni zuri sana. Vema, kwa kuwa unajua hivyo, basi, huo ni mshipa utakwisha. Nawe una—nawe una ki—kivimbe ubavuni mwako. Hiyo ni kweli, sivyo? Wataka nikwambie kiko upande gani? Kiko upande wako wa kulia. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa nenda zako ukaamini, nawe utapata afya.

²⁷⁴ Unaamini? Hakika, ni Kweli. Je, unaamini ya kwamba Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu, ameshuka katika nyakati zote kama alivyoahidi? Bali tu, je, unaamini ya kwamba ulimwengu umo katika hali ya Sodoma, tayari kuharibiwa kwa moto, kama Sodoma ilivyoharibiwa? Wasodoma walikuwa Mataifa, kumbukeni. Bali kule chini, katika Sodoma, kulikuweco na watu wenye haki, Mungu alimtuma mjumbe kuwaita watoke; baadhi yao wengine, wengine hawakutoka, wengi wao walibaki mle. Bali kulikuweco na kundi lililoketi mlimani, Ibrahimu, na kulikuweco Mjumbe aliyemjia kumwonyesha yatakayotendeka. Yeye hakupaswa kuwa mle, kwa vyo vyote. Lakini ulimwengu umo katika hali iyo hiyo leo, na Yesu Kristo ni Mwana Mungu, Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, naye alikuja kujidhihirisha Mwenyewe.

²⁷⁵ Naona jambo fulani likitendeka kwa mwanamke huyu. Yeye yuko hapa kwa sababu kuu. Hayuko hapa kwa ajili ya ugonjwa. Mwajua anachotaka kuomba? “Nimuwekee mikono,” naye “atapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Mnaona? Mnaona? Hilo si kweli? Inua mkono wako juu iwapo hiyo ni kweli. Mnaona? Mnaona, yeye ana jambo kuu. Mpenzi Baba wa Mbinguni, mpe huyu mtoto wako hamu ya moyo wake, hebu aupokee uabtizo wa Roho Mtakatifu. Basi ataupokea. Amina. Utaupokea. Mungu akubariki.

²⁷⁶ Unaamini? Nawe pale je, waamini, pia? Ukiamini, mambo yote yanawezekana. Wewe unayeonekana mwaminifu sana kwa hayo, je, unaamini ya kwamba huko kugandamana kwa damu kunaweza kuondoka, pia? Ewe unayeketi pale mwenye shati la kijani kibichi. Inua mkono wako ukiamini itaondoka itaondoka. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu, ni ngeni kabisa kwangu. Sijapata kumwona.

²⁷⁷ Mnaamini hilo, wengine wenu, kusanyiko? Sasa, je, hamwoni, haina budi kuwa ni Yeye?

²⁷⁸ Kansa si jambo baya kwa Mungu kuponya. Anaweza kuiponya, sivyo? Unaamini ataiponya? Vema, basi nenda zako, upokee, katika Jina la Yesu Kristo. Amini tu kwa moyo wako wote.

279 Salamu, kipenzi. Unajua, Yesu alimwaga Damu Yake, ku—kusudi damu yako iwe sawa. Unaamini hilo. Mungu Mpenzi, nambariki mtoto huyu, hebu na apate kutiwa damu mpya kutoka Kalvari. Ondoa sukari yote, Bwana, hebu apone, katika Jina la Yesu Kristo. Mungu akubariki.

280 Umeshindaje? Je, unaamini Yeye anaweza kuuponya huo mgongo kuupa afya? [Yule Ndugu anasema, “Najua anaweza.”—Mh.] Vema, nenda zako, amini, uwe na imani. Hebu tukuwekee mikono upate kuomba. Mungu akubariki, ndugu.

281 Unaamini? Yeye alitengeneza chakula kipate kuliwa, aliumba tumbo lipate kukisaga. Na kitu fulani kikiharibika mle tumboni, Yeye ndiye mponya wake. Waamini hilo? Vema, hayo tu ndiyo unayopaswa kujua, amini kwa moyo wako wote.

282 Kwa kuwa ulikuwa na shida ile ile, nenda zako ukiamini kwa moyo wako wote, pia.

283 Sawa, mleteni huyo bibi. Umeshindaje? Msichana mdogo mzuri, yeye ni mdogo sana kupata shida ya wanawake. Unaamini Yesu atakuponya huo? Mungu mpenzi, msichana huyu mdogo, namlaani huyu adui huku tukiwa katika Uwepo wa Yesu Kristo, hebu na amwache, na apate afya. Katika Jina la Yesu. Amina. Akubariki.

284 Je, unaamini? Sasa kivuli cheusi kinajitokeza, mauti. Kansa si... Mungu anaweza kuiponya kansa na kukupa afya. Je, unaamini hilo kwa moyo wako wote? Je, unaamini Yeye atakuponya hilo? Katika Jina la Yesu Kristo, nalaani kitu hiki atakuponya kilicholaaniwa chini ya wale samaki waliopitana, Msalaba wa Kristo na ukiondoe. Kifanye kiondoke katika Jina la Yesu. Usitilie shaka, nenda zako, amini kwa moyo wako wote. Amina. Ukiamini, mambo yote yanawezekana.

285 Umeshindaje? Bila shaka, yabisi kavu yako itaondoka, nawe utapata afya ukiamini. Je, unaamini ya kwamba utakuwa hivyo upate kutembea kila mahali tena na upate afya? Bwana ambariki huyu dada mpendwa, na ampe afya, katika Jina la Yesu Kristo. Nenda zako, ukuiamini kwa moyo wako wote.

286 Je, unaamini jambo lile lile linaweza kutendeka kwako? Vema, naamini limetendeka. Utakuwa... Kama unaamini umekwisha kuponywa sasa hivi. Naamini umekuondokea, mimi mwenyewe. Katika Jina la Yesu Kristo, hebu na ndugu yetu aende zake apate kuwa mzima na mwenye afya, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

287 Hatimaye ilitendeka. Wewe unayeketi hapo, ukilia, je, unaamini hizi bawasiri zitakuondokea? Yeye alikaa papa hapa hadi nusu saa ya mwisho, ilionekana, papa hapa mbele zangu, Yeye anasimama kando kabisa ya mtu huyu. Umekuwa ukiamini, sivyo? Amini kwa moyo wako wote, nawe waweza kurudi Texas upate afya. Sijamwona mtu huyo maishani mwangu.

288 Unaamini ya kwamba maskini mgongo huo utapona nawe utakuwa tayari kuponywa? Bwana Yesu, gusa hicho kitu kidogo na ukiponye, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Amini kwa moyo wako wote.

289 Sasa huyo Roho anasonga karibu, yuko kote jengoni. Ni vigumu kusema huo ulitoka wapi, wasiwasi. Hebu niwaonyeshe jambo fulani. Wangapi wana wasiwasi, kule nje, inua mkono wako. Unaona, vigumu kusema yupi ni yupi. Bali Mungu anajua habari zake zote, haja zenu zote. Umejaribu yote, kwa bidii, kuyashinda. Umejaribu kuyaacha mambo mengi maishani, nawe unataka kumtumikia Mungu kwa kila kilicho ndani yako. Yaonekana kama jambo fulani limekuzuia daima. Je, unaamini itatendeka sasa hivi, asubuhi hii, utafanywa huru kwa mambo haya? Je, utaamini?

290 Baba yetu wa Mbinguni, ili kwamba hawa wengine wapate kuona ya kwamba Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu, mponye huyu mwanamke mpendwa anayesimama hapa, Baba mtulize. Sote tunajua anaumwa nini, Bwana, nasi tunaomba ya kwamba utamponya. Ninapoweka mikono yangu juu yake kwa imani yote, mimi, pia, ninashambuliwa hivi sasa, ni mchofu, Shetani, kufanya kazi kupita kiasi, neva zinaharibika. Shetani, mwache. Naiweka mikono yangu juu yake kwa imani yote niliyu nayo, mwache, katika Jina la Yesu. Nenda zako, ukimwamini Yeye. Hilo ndilo ulilotaka nifanye.

291 Sikujui, wewe ni mgeni kwangu. Huo mshipa, ukiamini, utapona. Na jambo lingine, una yabisi kavu. Ukiamini, utapona. Kuumwa na mgongo kumeacha. Nenda zako ukiamini.

292 Je, unaamini kwa moyo wako wote? Hapa, hiyo...ni wangapi...Hao ndio tu walio mstarini? Je, kuna wengine wengi katika mstari uliobakia? Ninyi nyote pitieni hapa niweke mikono yangu juu ya wagonjwa. Hebuni tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi, ni baada ya saa saba. Mungu Mpenzi, naiweka mikono yangu juu ya dada yangu, huku upako wa Roho Mtakatifu uko hapa. Mponye, katika Jina la Yesu. Mpenzi Baba wa Mbinguni, naweka mikono yangu juu ya ndugu yangu... [Nafasi tupu kwenye ukanda, Ndugu Branham anaendelea kuwaombea wagonjwa—Mh.]... amini.

293 Lo, hukuombewa, ndugu? [Nafasi tupu kwenye ukanda—mh]...ndugu mnajua alivyofanya? Yeye ni mzee mwindaji wa kulungu. Alisema alikuwa na bunduki aliyoitumia kila wakati kwa kuwinda kulungu, alisema alikuwa mzee sana kwenda kuwinda. Alitaka kuileta hiyo bunduki anipe mimi. Amina. Hebu na tu seme, Bwana asifiwe. [Kusanyiko linasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.]

Ni nampenda, (Msisahau maswali yenu madogo, yahifadhini. Usipolipata leo, lilele Jumatano ama Jumapili)

Kwa kunipenda kwanza
 Kaninunulia... (Je, ninyi, nyote mlikuwa
 katika mstari wa maombi, mstari wa
 maombi?)... wokovu
 Kalvari.

²⁹⁴ Wazia jinsi alivyomwema kwetu, sasa. Wazia tu, Yeye huthibitisha Neno Lake! Mnaona? Angalia sasa, kama ningaliweza kuponya, ingekuwa tofauti, mnaona, bali Yeye ndiye ambaye amekwisha kufanya hivyo tayari. Mnaona? Kwa hivyo Yeye huthibitisha tu uwepo Wake hapa, "Nami nilikuwa nimekufa, na ni hai hata milele na milele." Hapajakuwepo mtu kama Yeye. Yeye alikuwa mtu wa kipekee. Alikuwa Mungu. Mnaona? Hamna mtu aliyepata kuishi jinsi alivyoishi. Hamna mtu aliyezaliwa kama alivyojaliwa... Hamna mtu angalifanya yale... kama alivyofanya. Hapakuwa na mtu aliyepata kufa kama alivyokufa Yeye. Hapakuwa na mtu aliyefufuka katika wafu kama alivyofanya. "Lo," mnasema, "ngoja kidogo, Ndugu Branham, wengine walifufuliwa katika wafu." Naam, bali walikufa tena. Bali Yeye yu hai milele na milele. Mnaona? Hamna mtu aliyefufuka kama Yeye alivyofanya. Yeye alifufuka katika wafu, milele na milele.

²⁹⁵ [Ndugu Branham avumisha "Nampenda"—Mh.] Hebu tumwimbie sasa.

Lo, ni nampenda, ni nampenda
 Kwa kunipenda kwanza
 Kaninunulia wokovu
 Kalvari.

²⁹⁶ Hebu tuinamishe vichwa vyetu. Bwana Yesu, nawapenda hawa watu. Nami nimewakawisha Bwana, sikutaka kufanya hivyo. Lakini hapa, wengi wao walingoja na watoto wadogo, wana njaa, hawaelewi. Lakini wameketi tu papa hapa, kwa maana wanajua mtu hawezi kuishi, ila kwa Neno la Mungu. Halafu wakati Neno linaponenwa, halafu linajulikana, linadhihirishwa, likathibitishwa, ndipo wao wanajua ya kwamba hapana budi ni Wewe pekee. Namwombea kila mmoja. Wabariki, Baba. Na wapate afya na wawe na nguvu kwa ajili ya safari iliyo mbele yetu. Wabariki juma hili lote. Na yakiwa ni mapenzi Yako, Bwana, ya kwamba tunaweza kukutanika hapa Jumapili ijayo, Sabato ijayo, kuja hapa na kuabudu, naomba, Mungu, ya kwamba utawapa nguvu. Wengine wao huenda wasiweze, wengine wao hawana budi kuenda makwao sehemu mbalimbali nchini, labda nchi za ng'ambo, ama nje ya Marekani. Tunaomba ya kwamba utakuwa pamoja nao na utawasaidia. Labda tukutane miguuni mwa Yesu, siku moja. Tujalie, Baba. Tusaidie sasa, kwa kuwa tunapendana, na kukuamini, tukitarajia siku moja ya kwamba kile kifungo kinachofunganisha mioyo yetu pamoja sasa kitakuwa kifungo

cha Milele, hebu na tuishi katika Mji huo ambao ni wa mraba, Milele yote. Katika Jina la Yesu. Amina. Vema.

Peleka Jina la Yesu
 Ko kote . . . (sasa salimianeni kwa mikono) . . .
 uendapo;
 Litafurahisha . . . (Geukeni mkasalimiane na
 mtu fulani, mkasema, “Nina furaha kuwa
 pamoja nawe, asubuhi ya leo”)
 Peleka uendako.
 Thamani, na tamu! (Mungu awabariki)
 Ni Jina Lake Yesu.
 Thamani na tamu!
 Ni Jina Lake Yesu

Sasa, sikizeni hili sasa, sasa imbeni hivi:

Peleka Jina la Yesu
 Liwe silaha zako;
 (Sasa sikiliza kwa makini) Utakapojaribiwa
 (Ufanye nini?) Lilia Jina hilo.
 Thamani (thamani), na tamu!
 Ni Jina Lake Yesu;
 Thamani (thamani), na tamu!



KUTHIBITISHA NENO LAKE SWA64-0816

(Proving His Word)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Agosti 16, 1964, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsihi hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org